

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

HISTORIA, MAANA NA LENGO LA USALAFI

السلفية
تاریخاً و مفهوماً و هدفاً

Kimeandikwa na:

Sheikh Ja'far Subhani

Kimetafsiriwa na:

Alhaji Hemedi Lubumba (Abu Batul)

Kimehaririwa na:

Al-Hajj Ramadhani S. K. Shemahimbo

ترجمة

السلفيّة

تاريχاً و مفهوماً و هدفاً

تألیف

العلامة المحقق الشيخ جعفر السبحاني

من اللغة العربية الى اللغة السواحلية

© Haki ya kunakili imehifadhiwa na:

Al-Itrah Foundation

ISBN No: 978 - 9987 - 17 - 033 - 3

Kimeandikwa na:

Allama Sheikh Ja'far Subhani

Kimetafsiriwa na:

Alhaji Hemedi Lubumba (Abu Batul)

Kimehaririwa na:

Al-Hajj Ramadhani S. K. Shemahimbo

Kimepangwa katika Kompyuta na:

Al-Itrah Foundation

Toleo la kwanza: Julai, 2013

Nakala: 2000

Kimetolewa na kuchapishwa na:

Alitrah Foundation

S.L.P. - 19701, Dar es Salaam, Tanzania

Simu: +255 22 2110640 / 2127555

Barua Pepe: alitrah@raha.com

Tovuti: www.ibn-tv.com

Katika mtandao: w.w.w.alitrah.info

YALIYOMO

Neno la mchapishaji	v
Dibaji.....	7
Umoja wa Kiislamu	12
Je Usalafi ni Madhehebu? Je Usalafi ni Madhehebu ya Kifiqhi au ni Njia ya Kiiitikadi?.....	17
AS-SALAF Katika Lugha ya Kiarabu.....	19
Uchambuzi juu ya hadithi ya karne bora.....	21
Je Usalafi ni Madhehebu?	27
Je Usalafi ni Mfumo wa Kifikra?.....	34
Mpasuko katika safu za Wanahadithi	40
Itikadi za at-Twahawiyyah ni mpasuko wa pili	43
Mabadiliko katika itikadi za Wanahadithi	45
Usalafi wa Misri.....	52
Usalafi na kundi la Ukh'wanul-Muslimuna	53
Usalafi katika zama za Mtume (saww).....	54
Kutofautiana kwao kuhusu mateka wa Badri	54
Kutofautiana kwao katika sulhu ya Hudaibiya	56
Kutofautiana kwao kuhusu kufunga safarini	57
Kutofautiana kwao kuhusu maandiko ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww)	58
Kutofautiana kwao kuhusu kifo cha Mtukufu Mtume (saww)	59
Tukio la Saqifa	61
Kutofautiana kwao katika Itikadi na Sharia	67
Watawala wa karne tatu bora	70
Maswali ambayo yanahitaji majibu kutoka kwa Masalafi	90
Swali la Kwanza: Kujisahaulisha Ahlul-Bait (as)	90
Swali la Pili: Kuhusu kauli ya Sahaba kuwa hoja	92
Swali la Tatu: Je sharti lao wanaposema: 'Watangulizi wema' ni sharti la kufafanua au ni la kuzuia?.....	94
Utetezi wa ajabu	95
Msiba uliompata Tabari aliyefariki mwaka 310 A.H	102
Fitna ya Mahanbali huko Baghdad katika mwaka wa 323 A.H. na kupingwa na ar-Radhi	104
Fitna ya kusoma Bismillahi kwa sauti, iliyotokea katika mwaka 447 A.H	106
Fitna baina ya Maashairah na Mahanbali katika mwaka wa 469 A.H.....	107
Swali la Nne: Je akili ni hoja kwa Masalafi?	108
Swali la Tano: Masalafi wa leo na tabia yao ya kuwakufurisha Waislamu	112
Hatar za uchochezi wa kimadhehebu	114
Tutakabiliana vipi na hatari hizi?.....	116

NENO LA MCHAPISHAJI

Kitabu ulichonacho mikononi mwako ni tarjuma ya Kiswahili ya kitabu cha Kiarbu kwa jina la, *al-Salafiyyah Tarikhan wa Mafhumin wa Hadafan*, kilichoandikwa na Sheikh Ja'far Subhani. Sisi tumekiita, *Historia, Maana na Lengo la Usalafi*.

Baada ya kufariki Mtukufu Mtume (s.a.w.w) Masahaba walihitilafiana katika baadhi ya mambo; na kubwa kuliko yote lilikuwa kuhusu kiongozi wa Waislamu baada yake (s.a.w.w). Hili lilileta mzozo mkubwa sana ambao bado unafukuta mpaka sasa. Mzozo huu ulisababisha kutokea kwa makundi mawili makubwa: 1) Wanaouna mkono Makhalifa waliochaguliwa na Waislamu, na 2) wanaomuunga mkono Imam Ali bin Abu Talib (a.s) kwa madai kwamba ye ye ali-teuliwa na Mtume mwenyewe kwa amri ya Mola kuwa mrithi wake. Kundi hili la pili lilijulikana kwa jina la **Shia wa Ali**. Matapo haya mawili yaliendelea kuwepo kwa muda yakijulikana kwa majina yao hayo. Baadae, kundi hili la kwanza (la Makhalifa) likagawanyika katika makundi mengi ya kifikihi, katika hayo manne ndio maarufu sana: Hanafi, Maliki, Shafii na Hanbali. Haya hayakutokea mara moja; kila moja lilitokea kwa wakati wake (ukisoma historia ya Uslamu utauona uk-weli huu). Ama Mashia wao wamebakia na jina lao hilohilo mpaka leo (soma historia ya madhehebu za Kiislamu). Baada ya muda kupita, yakajitokeza matapo mengine kwa majina tofauti tofauti. Kwa mfano, Wahabi, Ansar Sunna, Salafia, n.k.

Mwandishi wa kitabu hiki anaelezea kuhusu tapo hili la mwisho (Usalafi). Anaelezea kwa kina maana ya Usalafi (*Salafiyyah*), ulianzaje na lini, na athari yake kwa Waislamu. Tafadhali ungana naye ili upate kujua yaliyojiri katika historia ya Uislamu.

Tumekiona kitabu hiki ni chenye manufaa sana, hususan wakati huu wa maendeleo makubwa ya elimu katika nyanja zote, ambapo uwongo, ngano za kale na upotoshaji wa historia ni vitu ambavyo havina nafasi tena katika akili za watu.

Kutokana ukweli huu, taasisi yetu ya Al-Itrah imeamua kukichapisha kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili kwa madhumuni yake yaleyale ya kuwashudumia Waislamu, hususan wazungumzaji wa Kiswahili.

Tunamshukuru ndugu yetu Alhaji Hemedi Lubumba (Abu Batul) kwa kazi kubwa aliyofanya ya kukitarjumi kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili. Vilevile tunawashukuru wale wote walioshiriki kwa namna moja au nyingine hadi kufanikisha kuchapishwa kwake. Allah awalipe wote malipo mema hapa duniani na kesho Akhera – Amin.

**Mchapishaji
Al-Itrah Foundation**

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

**Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema
Mwenye kurehemu**

DIBAJI

Umoja wa umma wa Kiislamu ni jambo muhimu sana ambalo wanafikra na maulamaa wa Kiislamu wamekuwa waki-fanya jitihada kubwa tangu zama za awali za Uislamu kwa ajili ya kufikia umoja huo. Hadi sasa kumetolewa fikra ny-ningi na kuitishwa vikao na mikutano chungu nzima kujadili kadhia ya udharura wa kuwepo umoja na mshikamano kati ya Waislamu wote. Udharura wa umoja na mshikamano wa Kiislamu umesitisitwa mno katika maandiko ya kidini na dalili za kimantiki na kiakili. Hata hivyo inasikitisha kwamba Waislamu wanapokaribia kuungana na kuimari-sha umoja na mshikamano wao hujitokeza vizuizi chungu nzima ambavyo kunahitajika juhudhi kubwa, tadbiri (mazin-gatio) na mwamko wa Waislamu ili kuweza kukabiliana na-vyo na kuviondoa. Baadhi ya vizuizi na vikwazo vya umo-ja wa Waislamu vinatokana na hitilafu za ndani ya umma wa Kiislamu japokuwa hapana shaka kwamba wakoloni na madola ya kibeberu daima yamekuwa yakifanya njama za kuzusha hitilafu na mifarakanano katika umma wa Kiislamu. Maadui wa Uislamu wamekuwa wakitumia mbinu mbal-

imbali katika kuzuia umoja na mshikamano wa Kiislamu. Maadui hao hufanya jitihada za kutia chumvi na kukuza hitilafu ndogondogo za kimitazamo zinazotokea kati ya Waislamu na baadaye kuzitumia kwa ajili ya kuzusha mifarakano kati yao. Maadui hao hutumia hitilafu au tofauti za kimadhehebu, kilugha, kikaumu na kikabila na kadhalika kama nyenzo za kuzusha fitina na kuwatenganisha Waislamu. Ni wazi kuwa jiografia ya ulimwengu mkubwa wa Kiislamu inajumuisha makabila, kaumu, lugha, madhehebu na mataifa tofauti. Hata hivyo tofauti hizo za kimaumbile au hitilafu ndogondogo hazipaswi kuwa tatizo kubwa au kizuizi cha umoja na mshikamano.

Katika upande mwingine nchi za Magharibi zinaanzisha au kuhamasisha makundi yenye misimamo ya kupindukia na bandia katika ulimwengu wa Kiislamu kwa lengo la kuzuia umoja na mshikamano wa Waislamu. Kwa mfano sisi sote tunaelewa ni kwa kiwango gani makundi mawili ya Kiwahabi na Kibahai yalivyowasababishia Waislamu matatizo na mashaka makubwa mno katika kipindi cha karne mbili zilizopita.

Historia ya sasa ya dunia ya Kiislamu inaonesha kwamba madola ya kikoloni mara nyingi huwatumia watu ambao kidhahiria ni Waislamu lakini hakika yao ni watu waliopotoka na wanaotumiwa kuzusha mifarakano na hitilafu katika umma wa Kiislamu. Watu wa aina hii wamekuwa wakijitokeza wakiwa na anwani na sura mbalimbali, lakini sifa inayowakutaniha pamoja wote ni kuzua itikadi zinazokwenda kinyume na misingi ya awali ya Uislamu ambazo lengo lake kuu ni kuzusha mfarakano na hitilafu. Watu hawa wenye mitazamo potofu na isiyokuwa sahihi wanapatikana katika nchi mbali-

imbali. Baada ya kukithiri mitandao ya intaneti katika miaka ya hivi karibuni mwenendo wa kuzusha mijadala na kueneza itikadi zisizokuwa sahihi dhidi ya Uislamu na kukuza maudhui zinazozusha mifarakanano na hitilafu, imeongezeka zaidi. Hii ni moja ya mbinu zinazotumiwa na wakoloni kwa ajili ya kueneza hitilafu na kuzuia umoja na mshikamano kati ya Waislamu.

Juhudi za mkoloni Mwingereza za kupandikiza kansa katika jamii ya Waislamu zimezaa matunda, na hatimaye leo hii Mawahabi na Masalafi wanawakufurisha Waislamu kila kukicha, na si kuwakufurisha tu bali makundi mengine ya Kiwahabi na Kisalafi hayatosheki na kutoa tuhuma tu, bali yanachukua hatua za kutoa dharba na kuuangamiza upande wa pili; hali ambayo ni ya kusikitisha zaidi. Mfano wa wazi wa hali hiyo ni mwenendo wa maulamaa wa Kiwahabi wa kuwakufurisha Waislamu wa madhehebu nyingine.

Licha ya kwamba mashekhe hawa wa Kiwahabi na Kisalafi wanaelewa vyema kwamba Waislamu wa madhehebu ya Shia wanakubali na kuamini misingi na nguzo zote za Uislamu na hawatofautiani na Waislamu wenzao katika masuala mengi mno ya kisheria na kifiqhi, lakini bado wanawaita kuwa ni makafiri na wanahalalisha kumwaga damu ya watoto, wanawake na wafuasi wote wa madhehebu ya Shia. Fatuwa kama hizo zinazotokana na chuki za kimadhehebu na mitazamo finyu zimesababisha mauaji ya maelfu ya raia wasiokuwa na hatia katika nchi za Iraq, Afghanistan na Pakistan. Hivyo Maulamaa wa Kiislamu wanapaswa wajihadhari sana. Wachukue tahadhari mbele ya makundi haya ya Kiwahabi na Kisalafi, ambayo ni madhehebu bandia na ya kupandikiza ambayo lengo lake ni kuvuruga umoja kati ya Waislamu.

Wawe makini sana mbele ya dola hizi za mafuta (Saudia na Qatar) zinazotumika kwa ajili ya kuzusha mizozo na mifarakano. Wajihadhari na mikono hii michafu ya vibaraka wanaolenga kuvuruga umoja wa Kiislamu na kuivunja «غَرْوَةُ الْوُثْقَى» (kishikio madhubuti) ambapo Mwenyezi Mungu anasema katika sehemu moja ya aya ya 256 ya Sura ya Pili {al Baqarah} kwamba:

فَمَنِ يَكُفُرُ بِالظَّاغُوتِ وَيُؤْمِنُ بِاللَّهِ فَقَدِ اسْتَسْكَنَ بِأَنْعُرْوَةِ الْوُثْقَى لَا إِنْفِضَامَ لَهَا وَاللَّهُ سَيِّعُ عَلَيْهِ

Basi anayemkataa taghuti (Shet'ani) na akamwamini Mwenyezi Mungu, hakika ye ye ameshika kishiko madhubuti kisichovunjika. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia Mjuzi. (Surat Al-Baqarah 2 : 256) Pambaneni na watu wa aina hiyo wasiopenda umoja na mshikamano kati ya Waislamu. Kupambana na mikono hiyo kutawezekana tu kama Waislamu tutashikamana na umoja na kufuata njia ya kutuunganisha. Bila ya kufanya hivyo hakuna mafanikio yoyote tutakayopata.

Bila ya shaka njia za muda mrefu za hitilafu na mivutano ambazo zimekuwepo kwa miaka mia moja, au mia mbili au mia tano huweza kuleta dini ya kikoloni ili kuutia jeraha kubwa mwili wa ulimwengu wa Kiislamu jeraha ambalo kutibiwa kwake huwa si jambo rahisi. Mfano wake ni kama makundi ya Kiwahabi na madhehebu na dini nyinginezo za kupandiki za ambazo ndizo zinazoleta na kushadidisha mifarakano katika ulimwengu wa Kiislamu.

Tangu mwanzo Uwahabi ulizuka kwa lengo la kuutia pigo umoja wa Kiislamu na kuzusha kambi mithili ya Israel katika jamii ya Waislamu. Kama ambavyo wameipandikiza Israel ili

kupambana na Uislamu, wameleta pia serikali ya Kiwahabi na watawala hawa wa Najd (Saudia) ili waweze kupata kituo cha usalama ndani ya jamii ya Kiislamu ambacho kitakuwa ni tegemezi kwao na hivyo ndivyo tunavyoshuhudia.

Umoja na mshikamano wa umma wa Kiislamu ndio nguvu kubwa isiyoshindika ya umma huu ambayo inaweza kutumiwa na Waislamu kukabiliana na madola yanayoingilia masuala yao na kutaka kupora utajiri na maliasili zao. Pamoja na hayo yote tunapaswa kuelewa kwamba lengo kuu la wakoloni na madola ya kibeberu ni kuuondoa Uislamu katika maisha ya kawaida na kuidhoofisha dini hiyo inayopambana na dhulma na uonevu ambayo daima imekuwa kizuizi kikubwa dhidi ya siasa za kibeberu na tamaa za madola ya kikoloni.

Hemedi Lubumba

UMOJA WA KIISLAMU

Islamu umejengeka juu ya maneno mawili: Tamko la Tauhidi, na Nguvu moja. Ama kuhusu Tauhidi hilo ni jambo ambalo waliamrishwa Mitume wote wa Mwenyezi Mungu katika vizazi vyote, kama alivyosema Mwenyezi Mungu:

وَلَقَدْ بَعَثْنَا فِي كُلِّ أُمَّةٍ رَسُولًا أَنْ اعْبُدُوا اللَّهَ وَاجْتَنِبُوا الطَّاغُوتَ مَنْ هَدَى
اللَّهُ وَمَنْ هُمْ مِنْ حَقٍّ حَقَّتْ عَلَيْهِ الضَّلَالُ لَا فِي الْأَرْضِ فَسِيرُوا فِي الْأَرْضِ فَانظُرُوا كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ
الْمُكَبِّرِينَ

“Na kwa hakika tulimtuma Mtume kwa kila umma kwamba: Mwabuduni Mwenyezi Mungu, na mumwepuke taghuti. Basi mionganini mwao wapo aliowaongoa Mwenyezi Mungu. Na mionganini mwao wapo ambao uliwathibitikia upotovu. Basi tembeeni katika ardhi, muone ulikuwaje mwisho wa wale waliokadhibisha.” (Sura An-Nahl 16 : 36).

Hivyo Aya inaonesha kuwa kuwaita watu kwenye ibada ya kumwabudu Allah peke yake na kukataa ibada ya kumwabudu kila Shetani, ilikuwa ni kanuni ya kwanza katika mfumo wa Manabii na Mitume (as), na ummah wa Kiislamu kwa fadhila za Nabii wao Muhammad ulifika kileleni katika jambo la Tauhidi.

Ama kuhusu neno la pili, yaani kuwa na Nguvu moja na ummah mmoja wa Kiislamu, hilo ni jambo ambalo Mwenyezi Mungu amelisisitiza katika Aya kadhaa za Qur'ani tukufu, kati ya hizo ni kauli yake Mtukufu:

وَاعْتَصِمُوا بِحَبْلِ اللَّهِ جَمِيعًا وَلَا تَقْرُفُوا وَإِنْكُرُوا نِعْمَتَ اللَّهِ عَلَيْكُمْ إِذْ كُنْتُمْ أَعْدَاءً
فَالَّذِينَ بَيْنَ قُلُوبِكُمْ فَاصْبَحْتُمْ بِنِعْمَتِهِ إِخْرَانًا

“Na shikamaneni na kamba ya Mwenyezi Mungu nyote wala msifarikiane; Na kumbukeni neema ya Mwenyezi Mungu juu yenu mlipokuwa maadui, naye akaziunganisha nyoyo zenu; hivyo kwa neema yake mkawa ndugu;”

(Sura Al- Imran 3 : 103).

Hivyo kuwepo amri ya kushikamana na kamba ya Mwenyezi Mungu kunaonesha kuwa ummah umesambaratika mfano wa mtu anayetapatapa ndani ya kisima na hataraji kuokoka isipokuwa kwa kushikilia kamba aliyotupiwa, hivyo ikiwa haya ndio matokeo ya mfarakano basi kila mwenye akili hana shaka kuwa kuna ulazima wa kuepukana nao na kukimbilia kwenye umoja.

Hakika Mwenyezi Mungu ameuweka mfarakano wa ummah katika jumla ya adhabu zitokazo mbinguni, Mwenyezi Mungu amesema:

قُلْ هُوَ الْفَالِدُ عَلَىٰ أَنْ يَبْعَثَ عَلَيْكُمْ عَذَابًا مِنْ فَوْقِكُمْ أَوْ مِنْ تَحْتِ أَرْجُلِكُمْ أَوْ
يَلْسِكُمْ شِيَعًا وَيُنِيقَ بَعْضَكُمْ بَأْسَ بَعْضٍ انْظُرْ كَيْفَ نُصَرِّفُ الْآيَاتِ لِعَاهُمْ
يَقْهُونَ

“Sema: Yeye ndiye awezaye kuwaleta adhabu kutoka juu yenu au kutoka chini ya miguu yenu; au awavuruge (muwe) makundi, na awaonjeshe baadhi yenu jeuri ya wenzao. Tazama jinsi tunavyozieleza Ishara kwa njia mbali mbali ili wapate kufahamu.” (Sura Al-An'am 6 : 65).

Aya hizi mbili na nyinginezo ambazo zahusu maudhui hii zinapasa kuwapa Waislamu ari ya kuungana na kuwa kitu kimoja, ili wasimame safu moja katika kukabiliana na maadui wenyewe tamaa na mabeberu wavunja haki ambao wanavamia na kunyang'anya nchi zao, ambao wanawapangia njama na hila, ambao wanatawala mustakbali wao na maslahi yao.

Hakika yale yanayowaunganisha Waislamu na kuwafanya kitu kimoja ni mengi zaidi kuliko yale yanayowatofautisha na kuwagawa, hivyo sote kwa pamoja tufanye kazi ya kutilia nguvu mshikamano na kuimarisha misingi ya umoja na kutupilia mbali ikhtilafu, tuzike chuki zetu binafsi ambazo zinapandikizwa na kuenezwa na kuchochewa na kundi ovu ambalo pia limefanya kazi ya kuanzisha kundi jipya kwa jina la Salafiyyah ili lizidi kuongeza maji penye tope, na mdundo penye ngoma, hivyo Waislamu katika kila nchi wamekuwa ima Salafiyyah au Khalafiyyah, ima mtu wa Sunna au mtu wa Bidaa, na majina mengineyo ambayo Mwenyezi Mungu hakuyateremsha.

Utamuona mmoja wao akijisifu kuwa yeye ni “**Mwasisi wa daawa ya Salafiyyah na muhudumu wake**”¹ na anajifakharisha kwa hilo, na mwengine anaghani na kusema: “Kheri yote inapatikana katika kuwafata Masalafi, na kila shari inapatikana katika kuwafuata waliokuja baada yao.”

Hivyo anaugawa ummah wa Kiislamu katika makundi mawili, kundi bora linalopasa kufuatwa, na lingine ovu lin-alopasa kuepukwa, kana kwamba hajasikia kauli ya Mwenyezi Mungu isemayo:

¹ Muhammad Nasib Rifai katika kitabu chake: *At-Tawaswuli Ilaa Haqiqatit-Tawasuli*, Chapa ya Bairut ya mwaka 1394 A.H.

كُنْتُمْ خَيْرَ أُمَّةٍ أُخْرِجْتُ لِلنَّاسِ

“Mmekuwa ni umma bora mliotolewa kwa watu,”
(Sura Al-Imran 3 : 110).

Au kauli ya Mwenyezi Mungu:

وَكَذَلِكَ جَعَلْنَاكُمْ أُمَّةً وَسَطًا لِتَكُونُوا شُهَدَاءَ عَلَى النَّاسِ

**“Na kama hivyo tumewafanya kuwa umma wa wastani, ili
muwe mashahidi juu ya watu wote,”**
(Sura Al-Baqarah 2: 143).

Hivyo Ummah wa Kiislamu (bila kutofautisha baina ya wale waliotangulia na wale waliofutilia) ni ummah bora na wakati huo huo ni ummah wa wastani na ni kundi bora. Basi nini maana ya mgawanyiko na mfarakano huu!? Watu hawa badala ya kuunganisha pamoja ummah au kujituma katika kuukurubisha pamoja, wao wanatumia juhudhi zao katika kuleta mfarakano na kutengeneza vikundi ili kwa njia hiyo wawahudumie maadui wa ummah na marafiki zao.

Hakika hali hii ya Waislamu yenye kuumiza imenifanya niweze kukisoma kisa cha Usalafi, historia yake, maana yake na malengo yake. Na kwa rehema za Mwenyezi Mungu imebainika kuwa Usalafi si madhehebu ya kifqhi wala si mkondo wa kiitikadi, na kwamba Masalafi hawakuwa katika kamba moja hata watu waweze kuchukua kauli zao na kufuta vitendo vyao, na wao hawakuwa bora kushinda wale wal-

iokuja baada yao. Hivyo namuomba mpenzi msomaji azitizame kurasa hizi kwa mtazamo ulio mbali na kila aina ya rai aliyokuwa nayo hapo kabla, hivyo kama yaliyomo humu ni haki basi hiyo ni kutoka katika fadhila za Mwenyezi Mungu, na kama yaliyomo ni makosa basi hayo ni kutokana na hawaa (matamano) ya nafsi yangu.

Mwenyezi Mungu atulinde sisi na nyinyi dhidi ya upotovu wa majaribu na hawaa za nafsi, na atuongoze kwenye haki iliyowazi. Amin.

Ja'far Subhani

Qum Tukufu.

JE USALAFI NI MADHEHEBU YA KIFIQHI AU NI NJIA YA KIITIKADI?

Madhehebu za Kiislamu sawa ziwe za KiTheolojia (Kama vile Ash'ariyyah na al-Matridiyyah) au Kifiqhi (kama vile Mahanafi, Mashafi na Mahanbali) zinatofautiana kwa sababu ya kila madhehebu kuwa na mfumo bayana wanaou-fuata katika kukifahamu Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunna ya Mtume wake (saww). Kila mfumo husika unategemea kanuni na misingi ambayo ni maarufu kwao, licha ya kwamba zinaafikiana katika misingi mingi lakini zinatofautiana katika baadhi ya misingi hiyo, (na hata katika ile misingi ambayo zinaafikiana kwayo bado zinatofautiana katika kufahamu na kutafsiri baadhi ya vipengele vyake), na tofauti hizi ndizo zinazoitofautisha madhehebu moja na nyingine.

Na hapa tunajiuliza: Je usalafi unaingia chini ya mfumo huu ambaeo Waislamu wote wameafikiana juu yake, ili kwamba usalafi nao ufae kuingia chini ya mwamvuli wa madhehebu za Kiislamu, Kifiqhi au KiTheolojia? Na je Usalafi unategemea misingi thabiti iliyotokana na matendo ya Watangulizi na jinsi wao walivyoyafahamu maandiko ya Qur'an na Sunna katika karne tatu za mwanzo ambazo kwa mtazamo wao (Masalafi) wanaona kuwa kusudio la Mtukufu Mtume (saww) aliposema katika hadithi wanayoipokea kutoka kwake: "Watu bora ni watu wa karne yangu, kisha ni wale watakaowafuatia, kisha ni wale watakaofuatia hao.." ilikuwa ni watu wa karne hizo tatu, na kwamba kwa kauli hiyo alithabitisha ubora wao?

Je usalafi uko hivyo? Au wenyewe ni mkusanyiko wa fikra na dhana zinazotengeneza njia maalumu ya kundi maalumu ambalo limejipa istilahi hii, na wala halina uhusiano wowote na mfumo tulioutaja wa madhehebu za Kiislamu? Maswali haya na mengineyo tutajitahidi kuyadurusu na kuyajibu katika uchunguzi huu kama maudhui ilivyo bila upendeleo, na yote yatajibiwa kupitia faslu zifuatazo.

Mwandishi.

AS-SALAF KATIKA LUGHA YA KIARABU

Mwandishi wa kamusi la *Lisanul-Arab* amesema: as-Salaf: Ni jamaa walio tangulia, Mwenyezi Mungu amesema:

فَجَعَلْنَاهُمْ سَلَفًا وَمَثَلًا لِلْآخِرِينَ

“Kisha tukawafanya kuwa watangulizi na mfano kwa wa baadaye.” (Sura Zukhruf 43 : 56).

al-Qawmu as-Salaf: Ni watangulizi.

Salafur-Rajul: Ni wahenga zake walio tangulia.²

Maana kama hiyo imepatikana pia katika kamusi nyingine za Kiarabu, hatutarefusha mambo kwa kutaja maneno yao.

Kuuza kwa *as-Salaf* na *as-Salam* ni kuuza bidhaa kwa ahadi ya kulipwa thamani yake baadaye. Hii ndio maana ya neno hili kilugha na kifiqhi.

Lakini katika zama zetu hizi neno *Salaf* linatumika kumaanisha wafuasi wa Imam Ahmad bin Hanbal ambaye - kwao wao – ndio Imam mashuhuri zaidi aliyeinusuru Sunna na kuitetea, na akashikamana na mwenendo waliokuwa nao Watangulizi mionganoni mwa Masahaba na Tabiina. Na wala hajafuata rai zilizozuka baada yao, na katika hilo alipatwa na maudhi kutoka kwa baadhi ya Makhalifa wa Kibani Abbas lakini alivumilia na kusubiri.³

² *Lisanul-Arab* Juz. 9.

³ *Al-Mawsuatu ad-Dhahabiyyah Lil-Ulumil-Islamiyyah*: 29 / 503.

Hakika Masalafi wa leo ni wafuasi wa Imam Ahmad, am-baye huwasilisha yale yaliyopokewa kutoka kwa Masahaba na Tabiina katika tasnia ya Theolojia na Sharia bila kujumui-sha rai na fikra ambazo zilizuka katika zama za mwanzo na za baada yake. Imam Ahmad amekusanya wanayoyaamini watu wa athari katika tasnia ya Theolojia katika kitabu chake ambacho kakinukuu mwanawewe kutoka kwake.

Hakika jambo lililompelekea Ahmad bin Hanbal kutege-mea wanayoyaamini Masahaba, Tabiina na waliokuja baada ya Tabiina, bila kuithamini rai au fikra ya mwingine asiyeku-wa wao ni hadithi ambayo kaipokea Bukhari zaidi ya mara moja kutoka kwa Abidah, kutoka kwa Abdullah bin Masuud, amesema: "Watu bora ni watu wa karne yangu, kisha ni wale watakaowafuatia, kisha ni wale watakaofuatia hao, kisha watakuja watu ambao yamini ya mmoja wao itatanguliwa na ushahidi wake na ushahidi wake utatanguliwa na yamini yake."⁴

Ahmad bin Taymiyyah na wafuasi wake wamefasiri mael-ezo yaliyomo ndani ya hadithi kuwa yanamaanisha miaka mia tatu, na hivyo kuwavisha nguo safi na iliyo mbali na makosa ya wale walioishi katika miaka hiyo, na wakafanya maneno yao, vitendo vyao na ridhaa zao kuwa ni hoja juu ya zama nyingine, na ingawa hawajatamka wazi kuwa watu hawa ni maasumu lakini wao wanaamiliana nao kama vile wao ni maasumu.

⁴ *Sahih Bukhari*, Hadithi ya 2652.

UCHAMBUZI JUU YA HADITHI YA KARNE BORA

Mazungumzo hapa ni kuhusu hadithi hii inavyoonesha Usafi wa kutokukosea wala kujikwaa wa mtu atakayeishi ndani ya karne tatu. Ibnu Hajar amesema kuhusu sua la hili: "Imeshatangulia katika sifa za Mtume (saww) kuwa alisema: 'Nilitumwa katika karne bora kushinda karne zote za wana wa Adam.' Na katika riwaya ya Buraydah kwa Ahmad ni kuwa alisema: 'Karne bora katika ummah huu ni ile ambayo mimi nimetumwa mionganini mwao!' Na imedhihiiri kuwa muda uliyopo baina ya tangu alipoletwa Mtume na alipofariki, Sahaba wa mwisho kufariki ni miaka mia moja na ishirini au chini kidogo au zaidi kidogo kutokana na tofauti iliyopo kuhusu kufariki kwa Abu Tufayli.

"Na kama ataanza kuhesabiwa kuanzia baada ya kufa kwake basi itakuwa ni miaka mia moja au tisini au tisini na saba. Ama karne ya Tabiina ikiwa itaanza kuhesabiwa kuanzia mwaka wa mia moja basi itakuwa ni miaka sabini au themanini. Ama ya wale waliokuja baada ya Tabiina ikianza kuhesabiwa kuanzia mwaka huo (wa themanini) basi itakuwa ni miaka hamsini.

"Hivyo inadhihiiri kuwa muda wa karne hizi unatofautiana kutokana na tofauti ya umri wa watu wa kila zama. Lakini wameafikiana kuwa aliyekuwa wa mwisho kati ya wale wal iokuja baada ya Tabiina, ambaye kauli yake inakubalika, ni yule aliyeishi mpaka mwishoni mwa mwaka mia mbili na ishirini. Katika wakati huu ndipo ilipodhihiiri na kuenea bay-

ana bidaa, Mu'utazilah wakaachia huru ndimi zao, wanafal-safa wakanyanya vichwa vyao na watu wa elimu wakatahi-niwa ili waseme Qur'ani imeumbwa, na hali ikabadilika sana na bado jambo lina upungufu mpaka sasa.”⁵

Nasema: Aliyoyaeleza kuhusu maana ya karne kuwa ni muda, sawa iwe ni wa miaka mia moja au chini ya hapo au zaidi ya hapo, maana hiyo inapingana na Kitabu na lugha. Ama Kitabu ni kuwa kitabu kimetumia neno karne kwa maana ya kizazi -na si muda- ambacho kinaletwa pamoja na muda mmoja au utawala mmoja au anwani moja, sawa iwe waliishi miaka mia moja au zaidi au chini ya hapo, Mwenyezi Mungu anasema:

أَلَمْ يَرُوا كُمْ أَهْلَكْنَا مِنْ قَرْنِ مَكَانَهُمْ فِي الْأَرْضِ مَا لَمْ نُمَكِّنْ لَكُمْ
وَأَرْسَلْنَا السَّمَاءَ عَلَيْهِمْ مَدْرَارًا وَجَعَلْنَا الْأَنْهَارَ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهِمْ فَأَهْلَكْنَاهُمْ
بِذُنُوبِهِمْ وَأَنْشَأْنَا مِنْ بَعْدِهِمْ قَرْنًا آخَرِينَ

“Je, hawaoni karne ngapi tuliziangamiza kabla yao? Tuli-wamakinisha katika nchi tusivyowamakinisha nyinyi; tukawapelekeea mvua nyingi; na tukaifanya mito inapita chini yao. Kisha tukawaangamiza kwa dhambi zao; na tukaanzisha baada yao karne nyingine.” (Sura Al-An'am: 6 : 6).

Neno karne ndani ya Qur'ani limekuja katika sehemu saba, na katika sehemu hizo zote Qur'ani haijatumia neno hilo kwa maana ya muda, sawa iwe ni miaka mia, chini au zaidi, bali imetumia kwa maana ya kizazi cha watu ambao wanaishi ndani ya zama moja katika ardhi makhususi.

⁵ *Fat'hul-Bari*: 6 / 7.

Amesema ndani ya kamusi *Lisanul-Arab*: Karne ni ummah unaokuja baada ya ummah. Imesemekana kuwa muda wake ni miaka kumi. Na imesemekana ni miaka ishirini. Na imesemekana ni miaka thelathini. Na imesemekana ni miaka sitini. Na imesemekana ni miaka sabini. Na imesemekana ni miaka themanini, na ndio muda wa umri wa wastani wa watu wa zama Fulani. Na imenukuliwa kutoka kwa al-Azhariy kuwa alisema: ‘Na ninachogundua mimi, na Mwenyezi Mungu ndiye ajuaye zaidi, ni kuwa karne ni kipindi cha watu wa kila muda ambao humo alikuwemo Nabii au lilikuwemo tabaka fulani la maulamaa, sawa iwe ni miaka sitini au zaidi.’⁶

Si *Lisanul-Arab* pekee ndiyo iliyotoa tafsiri hii, bali hata mwandishi wa kamusi la *al-Qamusi ameafikiana* naye, pale alipofasiri kwa maana ya watu wa zama moja na ni ummah baada ya ummah. Na ushahidi juu ya hilo ni kauli ya mshairi: “Ikipita karne ambayo wewe umo humo na ukarudishwa katika karne nyingine basi wewe ni mgeni.”

Na kwa ajili hiyo hadithi inajulisha heshima ya vizazi vitatu vyenye kufuatana vitakavyoishi katika kigezo kimoja na kufungamanishwa na anwani moja, lakini ni upi muda wa kila kizazi? Hadithi haijataja.

Cha kustaajabisha ni kuwa Ibn Hajari aligundua haki mwanzo wa maneno yake hivyo akasema katika kutafsiri kauli: “Walio bora katika ummah wangu ni karne yangu. Yaani watu wa karne yangu, na karne ni watu wa zama moja walio karibu walioshirikiana katika jambo moja lilokusudiwa. Na inasemekana kuwa hilo (neno) ni makhususi pale wanapokusanyika katika zama za Nabii au Rais anayewakusanya pamoja katika mila moja au madhehebu moja au kazi moja.”⁷

⁶ *Lisanul-Arab*: 13 / 333, Madda: Karne.

⁷ *Fat'hul-Bariy*: 7 / 5.

Kutokana na maelezo yaliyotangulia tunapata mambo yafuatayo:

Kwanza: Hakika karne haimaanishi miaka mia moja, bali humaanisha kila ummah ambao watu wake wanaishi juu ya ardhi moja kwa kigezo makhususi, kama vile unabii, utawala, utamaduni na vigezo vingine ambavyo hukusanya watu wengi na kuwafanya kitu kimoja na ummah mmoja. Hivyo, kuna wakati, muda wa kuishi kwa baadhi ya ummah hufikia mamia ya miaka, kama vile ilivyokuwa kwa mafaraao na baadhi ya ummah zilizopita, na baadhi ya ummah muda wake wa kuishi huwa ni chini zaidi ya hapo, kama vile ummah unaoishi chini ya utawala wa muda mfupi au unaoishi chini ya kigezo kingine cha muda mfupi mionganoni mwa vigezo vyenye kukusanya watu wengi.

Ndiyo, katika istilahi ya watu wa sasa neno karne linatumika kumaanisha muda usiopungua miaka mia moja, hivyo Waislamu wa leo wanaishi katika karne ya kumi na tano Hijiriya. Lakini ni kwamba istilahi ya hadithi haina uhusiano wowote na lugha na Kitabu kitakatifu.

Pili: Hakika hadithi imeonesha ubora wa ummah tatu, ambazo zinakusanywa pamoja na kufanywa ummah mmoja na anwani mionganoni mwa anwani za tauhidi. Wa kwanza kati ya hizo tatu ni ule wenye kuishi pamoja na Mtukufu Mtume (saww) ambao ye ye ameufanya kitu kimoja na ummah mmoja. Ama wa pili na a tatu ambao Mtukufu Mtume (saww) ameuzungumzia kwa kauli yake: "Kisha ni wale watakaowafuatia, kisha ni wale watakaofuatia hao," hajaainisha muda wake wala kigezo kitakachowaleta pamoja katika kila ummah, hivyo huenda makusudio ya kipengele cha pili – kwa mujibu wa itikadi zao - yakawa ni kipindi cha ukhalifa

ambao ulikoma kwa kumwengua Hasan bin Ali (as) kwa shinikizo na njama za watoto wa Abu Sufiyan na wa Marwani.

Ama kipengele cha pili chenyewe kina dhana nyingi ambazo hakuna hata moja tunayoweza kuitegemea isipokuwa kwa dalili bayana, na dalili hiyo haipo. Na kwa kuwa dalili ni dhaifu na dhana ni nyingi basi kutafsiri vipengele hivi viwili kwa maana ya tabiina na wale waliokuja baada ya tabiina, inakuwa ni tafsiri itokanayo na rai binafsi, tafsiri ambayo haina dalili wala mashiko isipokuwa msimamo alionao mtu kuhusu haki yao.

Na hata tukijaalia kuwa ni sahihi kauli isemayo kuwa muradi wa vipengele vitatu vya hadithi ni muda ambao aliishi humo Mtume, walioishi tabiina na walioishi wale waliokuja baada ya tabiina, bado ni lazima kuchunguza kwa kina katika kuainisha kigezo kilichofanya zama zao ziwe bora. Huenda kwa karibu sana kigezo kikawa ni kule kuenea Uislamu katika zama zao katika sehemu kubwa ya ardhi, na kuushinda ushirikina, na hatimaye Ahlul-Kitabi wengi wakaingia katika heshima ya Uislamu, kwani upanuzi mwangi wa himaya ya Uislamu ultokea katika karne tatu za mwanzo na hapo watu wakaingia katika dini ya Mwenyezi Mungu makundi kwa makundi na mtu mmoja mmoja, na hili ni jambo lisilo na shaka kwa mtu mwenye kuijua historia ya Uislamu na Waislamu.

Lakini kitendo cha Masalafi wanatafsiri ubora kwa maana ya usafi wa watu wa karne tatu na kuwa wao wameepukana na kila jambo ambalo linaweza kutia dosari au kuchafua dini yao na matendo yao, na hivyo wao ni marejeo katika uwanja wa Itikadi na Sharia, kwani – kwa mujibu wa madai yao - ni

toka kwao wao huchukuliwa yale yanayopasa kuitikadiwa, na ni kwao wao mtu hurejea katika yale ambayo ni wajibu kuyafanya kazi. Zaidi ya hapo, ni kuwa wao ndio marejeo katika kutoa tafsiri ya Qur'ani na kutambua maana yake na malengo yake, wala haichukuliwi tafsiri ya watu wengine iwapo itajitokeza tofauti.

Haya ndio wanayodai Masalafi juu ya nafsi zao. Lakini je hadithi inajulisha hivyo? Itakuwaje ijulishe hivyo wakati tayari Mtukufu Mtume (saww) ameuelekeza ummah wote kuanzia Watangulizi mpaka waliofuatia, lile ambalo wana-pasa kushikamana nalo na kulirejelea baada ya kufa kwake, akasema: "Hakika mimi nawaachieni vizito viwili: Kitabu cha Mwenyezi Mungu na kizazi changu." Bila ya kuungani-sha kitu kingine. Inakuwaje sasa pamoja na kuwepo rejea hii tena tuwafanye wale ambao hatukuelekezwa kwao kuwa rejea na chimbuko la misingi ya Itikadi na Sharia?

JE USALAFI NI MADHEHEBU?

Hakika ili kukipa kitu jina ‘Madhehebu’ kinahitaji kwanza kiwe na misingi katika Theolojia na kanuni katika Sharia, misingi na kanuni ambazo wameafikiana juu yake watu wote wa madhehebu husika, hivyo Ashairiya na Matardiya ni madhehebu mbili zilizo kamili, kila moja ina misingi na vigezo vinavyojulikana, mwasisi wa madhehebu ya kwanza ametaja misingi ya madhehebu yake ndani ya kitabu *Maqalatil-Islamiyiina*. Na pia Matardiya licha ya kwamba ni madhehebu iliyo karibiana sana na madhehebu ya Ashairiya lakini inatofautiana nayo katika mas’ala arubaini na tano.

Na ni hivyo hivyo kuhusu madhehebu za kifiqhi, kila madhehebu ina misingi makhususi inayoitofautisha na madhehebu nyingine. Ama wanahadithi ambao Masalafi wanajiona kuwa wanafuata athari zao, wenyewe hawakuwa na misingi inayowakusanya pamoja katika uwanja wa Theolojia, wala hawakuwa na kanuni zenye kuwaainisha katika uwanja wa Sharia, bali walikuwa na fikra tofauti na rai zenye kugongana, na walikuwa na madhehebu tofauti.

Na kama una shaka na hili tulilosema – kuwa wanahadithi walikuwa wametofautiana katika rai na madhehebu katika upande wa Theolojia – basi sikiliza asemayo Suyuti kuhusu idadi ya madhehebu ya wanahadithi, kutofautiana rai zao na mwenendo wao, amesema hayo pale alipokuwa akitaja majina ya wale waliotuhumiwa kwa bidaa - kama alivyosema mwenyewe - mionganoni mwa wapokezi wa Bukhari na Muslimu au wa mmoja wao, hiyo ni ukiachilia mbali

wanahadithi wengine ambao ni wapokezi wa waandishi wa vitabu vingine vya Sunan na Musnad na ensaiklopidia ny- ingine za hadithi.

Yafuatayo ni majina ya wale aliowahesabu mionganoni mwa Mur'jia, na itikadi ya Ir'jai kama alivyosema mwenyewe ni kusita kutamka kuwa ni mtu wa motoni yule mwenye kuten- da madhambi makubwa. Na hao wanahadithi walio Mur'jia ni:

1. Ibrahim bin Twahamani.
2. Ayubu bin Aidhu at-Twaiy.
3. Dhar bin Abdullah al-Marhabiy.
4. Shababah bin Siwari.
5. Abdul-Hamid bin Abdurahman, Abu Yahya al-Ha- maniy.
6. Abdul-Majid bin Abdul-Aziz, Ibn Abi Rawud.
7. Uthman bin Ghiyath al-Basriy.
8. Umar bin Dhari.
9. Umar bin Murah.
10. Muhammad bin Khazim.
11. Abu Muawiya ad-Dhariru.
12. Warqau bin Umar al-Yashkariy.
13. Yahya bin Salih al-Wahadhiy.
14. Yunus bin Bakiri.

Na ametaja pia majina ya Manawasibu, akasema: Maana yake ni kumchukia Ali (as) na kumtanguliza mwingine juu yake, na hao wanahadithi Manawasibi ni:

1. Is'haqa bin Suwaydul-Adawiy.
2. Bahzu bin Asad.
3. Harizi bin Uthman.
4. Haswin bin Numairu al-Wasitwiy.
5. Khalid bin Salamah al-Faafau.
6. Abdullah bin Salim al-Ashariy.
7. Qaysu⁸ bin Abi Hazim.

Na ametaja pia majina ya Mashia, na kama alivyosema yeye: Ushia ni kumtanguliza Ali juu ya Masahaba wengine, na hao wanahadithi Mashia ni:

1. Ismail bin Aban.
2. Ismail bin Zakariya al-Khalqaniy.
3. Jariri bin Abdul-Hamid.
4. Aban bin Taghlab al-Kufiy.
5. Khalid bin Muhammad al-Qat'waniy.
6. Said bin Fayruz Abul-Bakhtariy.

⁸ Nasi hatukubaliani na kitendo cha kumjumuisha Qaysu mionganoni mwa Ma-naasibu, kwa sababu al-Khatibu al-Baghdadiy ndani ya Taarikh Baghdad Juz. 12 Uk. 452 amemtaja na kusema kuwa alihudhuria vita vya Nahruwani akiwa pamoja na Ali (as) dhidi ya Makhawarij, kama ambavyo pia riwaya zake zinabitisha kuwa hakuwa hivyo.

7. Said bin Ashuu.
8. Said bin Afir.
9. Ibad bin Awam.
10. Ibad bin Ya'qub.
11. Abdullah bin Isa bin Abdurahman bin Abi Layla.
12. Abdurazaq bin Hamam.
13. Abdul-Malik bin Aayun.
14. Ubaydullah bin Musa al-Abasiy.
15. Adiy bin Thabit al-Ansariy.
16. Ali bin al-Ja'di.
17. Ali bin Hashim bin al-Baridu.
18. al-Fadhl bin Dakin.
19. Fadhilu bin Marzuqu al-Kufiy.
20. Fataru bin Khalifah.
21. Muhammad bin Jihadah al-Kufiy.
22. Muhammad bin Fadhilu bin Ghazawani.
23. Malik bin Ismail, Abu Ghassan.
24. Yahya bin al-Jazzari.⁹

Pia ametaja majina ya al-Qadiriyah, na maana yake kama alivyosema mwenyewe ni: Kudai kuwa shari inatokana na kiumbe, na hao Wanahadithi al-Qadiriyah ni:

⁹ Yeye kamwandika kama al-Khazzar, na hayo ni makosa.

1. Thawru bin Zaidi al-Madaniy.
2. Thawru bin Yazid al-Hamswiy.
3. Hassan bin Atwiyyah al-Muharibiy.
4. Hasan bin Dhakawani.
5. Daud bin Haswin.
6. Zakariya bin Is'haqa.
7. Salim bin Ajalaniy.
8. Salam bin Miskini.
9. Saifu bin Salman al-Makiy.
10. Shubali bin Ibad.
11. Shariku bin Abi Namru.
12. Salih bin Kisani.
13. Abdullah bin Amru.
14. Abu Maamaru Abdullah bin Abi Labidi.
15. Abdullah bin Abi Najih.
16. Abdul-Aala bin Abdul-Aala.
17. Abdurahmani bin Is'haqa al-Madaniy.
18. Abdul-Warith bin Said Thawriy.
19. Atau bin Abi Maymanuh.
20. al-Alau bin al-Harith.
21. Amru bin Zaidah.
22. Imrani bin Muslim al-Qasiru.

23. Umairu bin Haniy.
24. Awfu al-Aarabiy.
25. Kahamasu bin al-Min'hali.
26. Muhammad bin Sawau al-Basriy.
27. Harun bin Musa al-Aawar an-Nahawi.
28. Hisham ad-Dastawaiy.
29. Wahab bin Munabihu.
30. Yahya bin Hamza al-Hadhramiy.

Na amemtaja Bashar bin as-Siriy na kusema: "Alituhumiwa kwa rai dhaifu, nayo ni kukanusha sifa za Mwenyezi Mungu Mtukufu na kusema kuwa Qur'an ni kiumbe."

Na amewataja pia Akrimah mtumishi wa Ibn Abbas na Walid bin Kathiri mionganoni mwa Maharuriyah, na akasema: "Nao ni Makhawariji ambao walipinga Ali kufanya mazungumzo na kundi la Muawiya na wakajitenga naye na kujitenga na Uthman na kizazi chake."

Na amemtaja Ali bin Abi Hashim, na amesema: "Alituhumiwa kwa kutokuwa na msimamo, nako ni kutokutoa msimamo juu ya Qur'ani je ni kiumbe au si kiumbe."

Na amemtaja Imrani bin Hatani, amesema: "Ni mionganoni mwa Maqaadiyyah ambao wanaona inaruhusiwa kuwapiga vita Maimamu lakini hafanyi hivyo."

Kutokana na maelezo yaliyotangulia inabainika kuwa Watangulizi ambao wanajiita Masalafi – ambao ni wanahadithi - walikuwa na rai zenye kupingana, nadharia zenye kutofautiana na fikra zenye kupishana. Na pia hawakuwa na misingi

na vigezo makhususi vyenye kuwakusanya pamoja katika nyanja yoyote ile ya dini na Sharia. Sasa inakuwaje Masalafi wa sasa wadai kuwa wamechukua misingi yao kutoka kwao na hali wao wenyewe hawana misingi hiyo? Na inakuwaje wadai kuwa wanawafuata na hali wao ni makundi tofauti, Watangulizi ambao hawana misingi itakuwaje wawe kiigizo cha waliokuja baada yao?!

JE USALAFI NI MFUMO WA KIFIKRA?

Meshabainika kutokana na tuliyoyataja kuwa Usalafi si madhehebu mionganini mwa madhehebu ya Kiislamu, si KiTheolojia wala Kifiqhi. Na sasa mazungumzo yamebakia kuhusu je wenyewe ni mfumo wa kifikra kwa kuwa unashikamana na mfumo wa Watangulizi, ambao walikuwa mbali na makosa na karibu zaidi na haki katika kutafsiri maneno ya lugha ya Kiarabu yaliyokuja ndani ya Qur'an Tukufu, kwa hoja kwamba wao walikuwa ni Waarabu asili waliokuwa mbali na mazingira yanayoweza kuwafanya wasiielewe lugha na kuyatoa maneno kwenye maana yake halisi.

Dhana hii si sawa na dhana ya kwanza katika ubatili wake na ubovu wake, isipokuwa ni kwamba nayo hatuvezi kuiafiki, hiyo ni kwa sababu Watangulizi – tangu zama za Mtukufu Mtume (saww) - hawakuwa katika mfumo mmoja katika msimamo wao kuhusu maandiko ya kidini, wapo ambao waliyafuata yaliyovo bila kujitenga nayo hata kidogo, na wapo waliyoyachezea kwa kuongeza rai zao na hawa walikuwa mashuhuri kwa jina la 'Watu wa rai binafsi na tashbihi' na wa kwanza wao ni Umar:

1. Talaka tatu kwa mara moja: Umar bin Khattab akasema: "Hakika watu wameharakisha katika jambo ambalo lilikuwa na uvumilivu kwao, naona ni vizuri tulipitishe juu yao. Akalipitisha juu yao."¹⁰

¹⁰ *Sahih Muslim*: 4 / 184, Mlango wa talaka ni tatu, Hadithi ya 1 – 3.

2. Bukhari ameandika kutoka kwa Imran bin Huswin (r.a), amesema: "Aya ya Muta iliteremshwa ndani ya Kitabu cha Mwenyezi Mungu na tukafanya Muta pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), na haikuteremka Qur'ani kuja kuifuta, na wala (Mtume) hakuikataza mpaka kufa kwake, lakini mtu mmoja (Umar) akasema atakayo kwa rai yake."¹¹
3. Ameandika Muslim kutoka kwa Abu Nadrah, amesema: "Nilikuwa kwa Jabir bin Abdillah, na mara alikuja mtu na kusema: 'Ibn Abbas na Ibn Zubairi wametofautiana kuhusu Muta mbili.' Jabir akasema: 'Tulifanya Muta pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), kisha Umar akatukataza...'"¹²
4. Umar alitamka bayana katika hotuba yake kuwa anakataza Muta mbili zilizotajwa (ya Wanawake na ya Hijja), akasema: "Muta mbili zilikuwepo katika zama za Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) na mimi nazi-kataza na kutoa adhabu juu yake."¹³

Na hebu tusome pia mazungumzo haya, kwanza kuhusu Muta ya wanawake, na pili kuhusu Muta ya Hijja.

Ibn Abbas: "Mtukufu Mtume alifanya Muta."

Ur'wah bin Zubair: "Abu Bakr na Umar walikataza Muta."

Ibn Abbas: "Ur'wah anasemaje?"

Msemaji: "Anasema: Abu Bakr na Umar walikataza Muta."

¹¹ *Sahih Bukhari*: 3 / 154, Kitabu cha Tafsiri, Mlango wa 33, Hadithi ya 4158.

¹² *Sahih Muslim*: Kitabu cha Nikahi, Mlango wa 3, Hadithi ya 17.

¹³ *Ahkamul-Qur'an* cha al-Jaswas: 2 / 152. *as-Sunanul-Kubra* cha al-Bayhaqiy: 7 / 206.

Ibn Abbas: Naona wataangamia, mimi nasema Mtukufu Mtume, yeeye anasema: Abu Bakr na Umar walikataza.”¹⁴

Tirmidhiy amepokea kwa njia yake kutoka kwa Ibn Shihab kwamba Salim bin Abdullah alimsimulia kwamba alimsikia mtu mmoja kutoka Sham akimuuliza Abdullah bin Umar kuhusu Muta ya Hijja, Abdullah bin Umar akasema ni halali. Mtu yule wa Sham akasema: Lakini baba yako alikataza. Abdullah bin Umar akasema: “Hivi kama baba yangu alikataza wakati Mtume wa Mwenyezi Mungu alifanya, je inapasa ku-fuatwa amri ya baba yangu au amri ya Mtume wa Mwenyezi Mungu?” Mtu yule akasema: “Amri ya Mtume wa Mwenyezi Mungu.” Akasema: “Basi Mtume wa Mwenyezi Mungu ali-fanya.”

Tirmidhiy anasema: “Hadithi hii ni sahihi na nzuri.”¹⁵

Laajabu ni kuwa Umar hata katika zama za Mtukufu Mtume (saww) alikuwa akisema kwa rai yake kinyume na alivyokuwa akitaka na kuamrishaa Mtume, kana kwamba yeeye alikuwa anajua maslahi ya mambo kuliko Mtume. Yeye mwenyewe alizungumzia hilo siku moja kama itakavyokuja huko mbele, pale alipofichukiwa na maslahi ya kweli ambayo Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikuwa amey-aainisha.

Na sasa mazungumzo yamebakia kuhusu maslahi ambayo Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikuwa ameyaainisha lakini Umar akakhalfu amri yake na kamwe hakujua ukweli

¹⁴ *Musnad Ahmad*: 1 / 337.

¹⁵ *Sunan-Tirmidhiy*: 259, Kitabu cha Hijja, Mlango wa 12, Yaliyokuja kuhusu Muta, Hadithi ya 825, imesahihishwa na Swadqiyu Jamilul-Atari, Darul-Fikra- 1425 A.H.

wake kwa kuwa haiwezekani au ni vigumu kuziona athari zake chanya, au kuziona athari hasi zitokanazo na kupinga amri husika, kwani athari nyingi kama hizi hazionekani isipokuwa baada ya muda mrefu.

Amepokea Ibn Saad kwa njia yake kutoka kwa Miqdad bin Amru, amesema: "Mimi ndiye niliyemteka al-Hakam bin Kisani, kiongozi wetu akataka kumkata shingo, nikamwambia muache tumpeleke kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), tulipompeleka kwa Mtume, Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alianza kumlingania Uislamu, akatumia muda mrefu kumlingania, Umar akasema: 'Kwa kitu gani unazungumza na huyu ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu? Wallahi kamwe milele asilimu huyu, niache nimkate shingo yake na aingie katika shimo la moto.' Lakini Mtume hakumjali Umar, mpaka al-Hakam akasilimu. Umar alisema: 'Mara nikamuona amesilimu kiasi kwamba likanishughulisha lile lililotokea mwanzo na lile lililofuata baadaye, nikasema: Inakuwaje namzuia Mtume kutenda jambo ambalo yeye alijua zaidi kuliko mimi kisha baadaye nasema, kwa hilo nilitaka kumnasihi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake?'

"Umar alisema: 'Alisilimu na wallahi ukawa mzuri Uislamu wake, akapigana jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu mpaka akauwawa shahidi katika kisima cha Mauna huku Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akiwa radhi naye, na akaingia peponi."¹⁶

Imam Abu Hanifa (80 – 150 A.H.) alikuwa akitumia Tashbihi na Istihsani katika kiwango cha hali ya juu zaidi, wakati

¹⁶ *At-Tabaqat al-Kubra*: 4 / 137, Darul-Bairuti, na Daru Swadiru, Chapa ya mwaka 1377 A.H.

ambapo Imam Shafii alikuwa akitumia Tashbihi bila Istihsani na akiona kuwa ni mzushi yule mwenye kutumia Istihsani.

Wakati ambapo Abu Hanifa alikuwa akiona kuwa inaruhusiwa kutumia rai binafsi inapokosekana dalili, Malik alikuwa akiona kuwa hairuhusiwi kufanya hivyo, na nyinginezo mionganoni mwa sura za tofauti iliyopo baina ya madhehebu ya Kifiqhi au KiTheolojia. Sasa je baada ya yote haya inasihi kudai kuwa Watangulizi wana mfumo mmoja wa kifikra ambao ni wajibu kuufuata?

Mwandishi mmoja wa Kisyria ana maneno kuhusu hili, anasema: "Lakini ilipokuwa hakuna vigezo na mipaka bayana inayotenganisha baina ya rai itokanayo na dalili za maandiko na hitimisho lake na ile rai ilioiasi iliyo nyuma ya ukuta, ndipo ulipozuka mtikisiko mkubwa kuhusu msimamo ambao unatakiwa kuchukuliwa kuhusu rai binafsi, wakati ambapo kundi kubwa la wanafiqhi mionganoni mwa Masahaba na Tabiina lilikimbilia kwenye rai binafsi kila pale maslahi yalipopelekea kufanya hivyo, ni wakati huo huo kundi jingine kubwa la wanafiqhi mionganoni mwa Masahaba na Tabiina lilikimbilia upande mwingine kabisa, hivyo wao wakafunga mlango wa kutumia rai binafsi na wakajizua kuingia humo, na wala hawakusita kutangaza upingaji wao juu ya matendo ya kundi hilo lingine.

"Na mionganoni mwa vinara wa kundi hili (lililopinga rai binafsi) ni Abdullah bin Abbas, Zubair, Abdullah bin Umar bin Khattab, Abdullah bin Amru bin Aswi, hao ni mionganoni mwa Masahaba. Ama katika Tabiina ni Ur'wah bin Zubairi, Atau bin Abi Rabah, Aamir bin Sharahil maarufu kwa jina la Shaabiy. Na imepokewa kuwa Shaabiy alikuwa akisema: 'Yale waliyokuleteeni hawa kutoka kwa Masahaba wa Mtume wa

Mwenyezi Mungu (saww) yachukueni, ama yale yatokanayo na rai zao binafsi yatupeni chooni."¹⁷

Na la kushangaza ni kuwa hao Watangulizi wema, katika kutatua tatizo hili ambalo lilileta mpasuko baina ya Waislamu, hawakurejea kwa Maimamu wa Ahlul-Bait (as) ambao Mtukufu Mtume (saww) aliwafanya pacha wa Kitabu na rejea ya kufuatwa, kana kwamba wao si katika Watangulizi wema.

Pamoja na tofauti yote hii, bado tunakuta kuwa: "Yule anayelingania Usalafi anaudhihirisha kana kwamba Usalafi ni nadharia na matendo yenye kuafikiana, wakati uhalsia ni kwamba ni matendo zaidi ya moja yenye kupingana, na una mitazamo zaidi ya mmoja yenye kupingana. Na Watangulizi si wenye rai moja, mwelekeo na msimamo mmoja, hata mtu aweze kujinasibisha nao."¹⁸

¹⁷ As-Salafiyyah Marhalah Zamaniyyah La Madh'habu Islamiy, cha Dkt, Muhammad Said Ramadhan al-Bawtiyyu: 51.

¹⁸ Qiraatu Fi Kutubil-Aqaid cha Hasan bin Farhan al-Malikiy: 187, Kituo cha masomo ya historia huko Oman, chapa ya mwaka 1425 A.H.

MPASUKO KATIKA SAFU ZA WANAHADITHI

Wavuka kipimo miongoni mwa wanahadithi walichukua kauli na rai za Imam Ahmad na kuzifanya misingi isiyokubali kujadiliwa – licha ya kuwemo humo mambo ambayo yanakhilfu akili salama – mpaka pale Abul-Hasan al-Ash'ariy (260 – 324) alipojiunga na wanahadithi kwa kutangaza bayana kujitenga kwake na madhehebu ya Muutazila, madhehebu ambayo alidumu nayo mika mingi, kwani alipanda kwenye kiti katika msikiti mkuu wa Basra na akanadi kwa sauti ya juu kabisa: "Anayenijua basi ameshanijua, na asiyenijua basi mimi ni fulani bin fulani, nilikuwa nikisema kuwa Qur'ani ni kiumbe, na kwamba Mwenyezi Mungu haoni kwa macho, na kwamba vitendo viovu mtendaji wake ni mimi mwenywewe. Lakini sasa natubu na kung'oa itikadi hiyo kwa kuwapinga Muutazila, nazitoa nje fedheha zao na aibu zao."¹⁹

Na kuna dhana kadhaa kuhusu sababu iliyomfanya Sheikh al-Ash'ariy kujunga na wanahadithi, hapa tutataja dhana mbili tu katika hizo:

Ya kwanza: Ni kuwepo mgandamizo dhidi ya Muutazila kutoka kwa Makhalifa wa Bani Abbas, tangu al-Mutawakil al-Abasiy aliposhika utawala, na hapo akawasaidia wanahadithi na hivyo wao wakawa na nguvu katika zama zake na katika zama za watawala waliofuata baada yake kama

¹⁹ *Al-Fahrastu cha an-Nadim*: 231, Fani ya tatu katika makala ya tano. Na pia *Wafayatul-Aayan*: 3 / 285.

vile al-Mustansiru, al-Mustainu, al-Muutazu, al-Muhtadi, al-Muutamadu, al-Muutadhadu, al-Muktafi, al-Muqtadiru, am-baye alichukua hatamu ya utawala kuanzia mwaka 295 AH. Mpaka mwaka 320 A.H. ni katika kipindi hicho ndipo Abul-Hasan al-Ash'ariy alitangaza toba yake na kujitenga kwake na Muutazila na hatimaye kujiunga na kundi la wanahadithi.

Ya pili: Alijiunga na wanahadithi kwa lengo la kufanya marekebisho katika itikadi zao ambazo zilijaa batili na upotovu, hivyo mfumo wa al-Ash'ariy ukaja kama mfumo wa kati baina ya mifumo miwili: Mfumo wa wanahadithi na wa Muutazila.

Vyovyote vile iwavyo, sawa sababu iwe ni kujinasua na mgandamizo wa utawala uliokuwa dhidi ya Muutazila, au iwe ni kufanya marekebisho katika itikadi za wanahadithi, bado ni kwamba msimamo wake haukupata bahati ya kukubalika na mashekhe wa wanahadithi ambao hujiita ‘Wafuasi wa Watangulizi wema’. Kwani katika kitabu *Tabaqat* cha Ibn Abi Ya’la kuna hikaya hii:

“Abu Abdullah al-Hamraniy amesema: al-Ash’ariy alipointia Bagdad alikuja kwa al-Barbahariy²⁰ na akaanza kusema: ‘Nimemjibu al-Jabaiy na Abu Hashim, nimevunja hoja zao, za Mayahudi, Manasara na Majusi, nilijadiliana nao.’ Alikithirisha maneno na aliponyamaza, al-Barbahariy alisema: ‘Sijui chochote katika uliyosema, si katika machache wala si katika mengi, na wala hatutambui isipokuwa yale aliyosema Abu Abdullah Ahmad bin Hanbal.’

²⁰ Yeye ni Hasan bin Ali bin Khalaf, alikuwa ni Shekhe wa Mahanbali katika zama zake, ni mtu wa Bagdad, ana Sharhu juu ya *Kitabus-Sunnah*, alifariki mwaka 329 A.H. Tazama *al-Aalam*: 2 / 201.

"Abu Abdullah al-Hamraniy anasema: Basi akatoka kwake na akaandika kitabu al-Inabah, lakini (al-Barbahariy) hakuki-kubali, na hakuonekana tena Baghdadi mpaka alipoondoka humo."²¹

Vyovyote iwavyo ni kwamba rai za al-Ash'ariy zilizua mpasuko katika safu za wanahadithi, hivyo wakagawanya-ka makundi mawili, yupo aliye mfuasi wa Hanbali ambaye haendi nje ya yale aliyoandika Imamu wake katika misingi, na yupo yule aliye mfuasi wa al-Ash'ariy ambaye anachukua rai ya kati katika itikadi za wanahadithi, na anasema kuwa akili ni hoja katika maarifa. Hakika baada ya kufariki al-Ash'ariy ulitokea mgongano baina ya makundi mawili katika maudhui zaidi ya moja, analitambua hilo yule aliyesoma kitabu *Tabaqatus-Shafiiyyah*.²²

²¹ *Tab'yin Kidhibul-Muftariy*, Sehemu ya maelezo: 391.

²² *Tabaqatus-Shafiiyyah* cha as-Sabkiy: 3 / 391.

ITIKADI ZA AT-TWAHAWIYYAH NI MPASUKO WA PILI

Kitabu *al-Aqidah at-T wahawiyyah* kinahesabika miongoni mwa vitabu vya msingi kwa Masunni, nacho ni mionganoni mwa vitabu vya kiada vya Chuo kikuu cha Madina mpaka leo hii, na mwandishi wake ambaye aliishi zama za Sheikh al-Ash'ariy na akafariki mwaka 321 A.H. ananasibisha kila kilichomo humo na Abu Hanifa na Abu Yusuf na Muhammad bin Hasan as-Shaybaniy.

Itikadi hii ambayo inapingana na itikadi ya Ashaira katika mas'ala kumi na tatu, ilizua mpasuko wa pili katika safu za wanahadithi, kwa kuwa iliathirika na kauli za Imam Abu Hanifa ambaye ndiye kiongozi wa rai binafsi na si kiongozi wa nukuu za maandiko.

Mpasuko wa tatu ulidhihiri katika safu za wanahadithi kwa kudhihiti madhehebu ya al-Matridiyyah huko Mashariki, ambapo hawa waliwakhalifu wanahadithi (ambao hujita wafuasi wa Watangulizi wema- Masalafi-) katika mas'ala kadhaa ya kiitikadi, kama ambavyo waliwakhalifu Ashaira katika mas'ala arubaini na tano.

Hali iliendelea kuwa hivyo bila kuwepo mabadaliko makubwa mpaka alipodhihiri Ahmad bin Taymiyyah (661 - 728 A.H) akayapa umuhimu mahususi madhehebu ya wanahadithi na akamfuata Ahmad bin Hanbali katika yale yaliyopokewa kutoka kwake katika upande wa Theolojia na Sharia. Lakini pamoja na hali hiyo alikuwa hatumii jina 'Us-

alafi' kama istilahi, bali alikuwa akinasibisha rai zake kwa Watangulizi au kwa Masunni.

Katika upande huu kaandika risala na vitabu kadhaa, vyote vikiwa na lengo la kuelezea kwa maana ya neno kwa neno (sisisi - ya kilugha) zile sifa za Mwenyezi Mungu zilizomo ndani ya Kitabu na Sunna, kiasi kwamba akadai kuwa Mwenyezi Mungu ana upande, yuko juu, anatikisika, anapanda na kushuka, na mengineyo mionganini mwa sifa za vitu vyenye umbile.²³

²³ *Majmuatur-Rasail al-Kubra*: Juz. 1, *al-Aqidah al-Wasitiyyah*: 398, 399, 401, Maktaba ya machapisho ya Muhammad Ali Swabihu na watoto wake, Cairo.

MABADILIKO KATIKA ITIKADI ZA WANAHADITHI

Hakika Ibn Taymiyyah hata kama atadai kuwa yeye Hanafuata mfumo wa Ahmad bin Hanbal, lakini ni kwamba ameachana naye katika mas'ala mengi ambayo Ibn Taymiyyah ametegemea katika mas'ala hayo habari za Mahashawiyah, jambo ambalo lilileta mpasuko katika itikadi zao na kuwagawa makundi mawili. Mionganoni mwa itikadi hizo ni itikadi yake kuhusu sifa za Mwenyezi Mungu, kuharamisha kwake safari ya kwenda kulizuru kaburi la Mtukufu Mtume, kuharamisha kwake kujengea kaburi na kuharamisha kwake kutawasali kupitia Mtukufu Mtume (saww).

Ulamaa wa zama zake kama vile as-Sabkiy aliyefariki mwaka 756 A.H. Na Ibn Jahbal aliyefariki mwaka 733 A.H. na wengineo walimpinga, kama ambavyo pia aliwekwa gerezani zaidi ya mara moja kwa sababu ya baadhi ya itikadi zake na fatwa zake. Alialikwa Misri mwaka 705 A.H. na akawekwa gerezani huko Misri muda wa mwaka mmoja na nusu kwa sababu ya kudai kuwa Mungu ana umbile. Kama ambavyo aliwekwa kizuzini kwa kulazimishwa kuishi huko Damascus mwaka 726 A.H. kwa sababu ya fatwa yake ya kuharamisha watu kusafiri kwenda kuyazuru makaburi ya Manabii, al-iendelea kuwa kizuzini hapo mpaka alipofariki mwaka 728 AH. Na hakuna aliyeathirika na mfumo wa Ibn Taymiyyah isipokuwa watu wachache kama vile ad-Dhahabiy aliyefariki mwaka 747 A.H. na Ibn Qayyimu al-Jawziyyah aliyefariki mwaka 751 A.H. na Ibn Kathir aliyefariki mwaka 774 A.H.

Pamoja na hivyo bado ad-Dhahabiy alimkhalifu katika baadhi ya misingi, na akamwandikia barua ambayo humo alipinga baadhi ya madai yake na fikra zake, na kwa ajili hiyo mfumo wake haukuwa na jina kubwa baada ya kufa kwake na ulikaribia kufutika kama si Muhammad bin Abdul-Wahabi kuunadi katika ardhi ya Najda, ambapo alijitolea kwa juhud zake zote katika kuhuisha itikadi yake kuhusu Manabii na mawalii bila kugusa itikadi yake kuhusu baadhi ya mas'ala yanayohusu sifa za Mwenyezi Mungu, itikadi inayolazimu Mungu kuwa na upande na mtikisiko.

Kwa kweli kudhilihiri kwake katika nchi iliyo mbali na elimu, iliyoenea ujinga na ukosefu wa elimu, kulimsaidia sana katika kufanikisha lengo lake, hasa baada ya kuungana na watawala wa nchi ya Wasaudia kwa sharti kwamba wao wawe na utawala na yeye awe na mamlaka ya kutoa fatwa na kusimamia mambo ya Sharia, na pia khumsi za ngawira ziwe zake – ngawira zilizokuwa zikiletwa na jeshi lake pindi linapoyavamia makabila ya Yemen, Iraq na kwingineko.

Pamoja na hayo bado yeye hakuwa na sauti, na hata yule aliyekuja baada yake, mpaka Wasaudia walipoziteka Haramu mbili tukufu kwa mbinu za marafiki zao – na kinara wao ak-iwa ni Uingereza - ambao waliugawagawa vipande utawala wa Uthmaniya na kuufanya vinchi vidogo vidogo ambavyo ni rahisi kuviteka na kuvipora milki zake na kuzifanya zitii mbele ya dola kubwa, na hapo ndipo neno Salafiyyah (Usalafi) lilipoenea katika vyombo vyaya habari viliwyokuwepo zama hizo yakiwemo majarida, magazeti, vitabu vyaya kiada na idhaa mbalimbali.

Istilahi ya Usalafi kwa hawa watu ni sawa na kuwakufurisha, kuwatuhumu kwa bidaa na kwa ufasiki Waislamu wen-

gine wasiokuwa wao. Japokuwa Watangulizi wao hawakuwa na ujasiri na uthubutu wa kumwaga damu, kupora mali na kuuwa watu kiholela lakini mfumo aliouweka Ibn Taymiyyah na kuurudisha upya Muhammad bin Abdul-Wahab hau-na matokeo isipokuwa misiba hii mikubwa katika maisha ya Waislamu, kwani bado tunaendelea kusikia kila siku matukio makubwa na mengi ya kujilipua (Boko Haramu, al-Shabab, al-Qaida, nk) yakilenga kuwauwa watu wasiokuwa na hatia mionganoni mwa wazee, watoto na wanawake, kwa hoja kwamba wao ni mushrikina, na hawana dhambi yoyote isipokuwa ni kwa sababu wao wanashikamana na Mtukufu Mtume (saww) na Ahlul-Baiti wake, na wanapata heshima ya kuzizuru sehemu ambazo hapo ilizikwa miili ya hao watakasifu, au wanapata heshima ya kufanya hafla na sherehe za kuzaliwa kwa hao watakasifu, na mengineyo mengi mionganoni mwa ada za kawaida ambazo Waislamu walikuwa wakizifanya karne zote bila yejote mionganoni mwa ulamaa kuharamisha walau kwa neno moja, mpaka alipokuja Ibn Taymiyyah katika karne ya nane ndipo akaanza kukataza.

Na ili msomaji aone jinsi Ibn Taymiyyah alivyoyakhilifu madhehebu ya Sunni katika mas'ala haya na mengineyo - ukiachilia mbali alivyoukhalifu Ushia - tunaleta hapa mistari michache tu iliyoandikwa na Taqiyud-Din as-Sabkiy as-Shafiy akimjibu Ibnu Taymiyyah katika mas'ala ya kufunga safari kwa ajili ya kwenda kuzuru makaburi, amesema katika mlango wa tatu, chini ya anwani: Yaliyopokewa kuhusu safari ya kwenda kufanya ziara yanatamka wazi na bayana kuwa jambo hilo lilikuwepo na bado linaendelea:

"Mionganoni mwa Masahaba ambao jambo hilo limepokewa kutoka kwao ni Sahaba Bilal bin Abi Riyaha, mwadhini wa

Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), alisafiri kutoka Sham mpaka Madina kwenda kulizuru kaburi la Mtume (saww). Tumepokea hilo kwa sanadi safi inayokomea kwake, na miongoni mwa watu waliotaja hilo ni al-Hafidh Abul-Qasim bin Asakir, na pia limetajwa na al-Hafidh Abu Muhammad Abdul-Ghina al-Muqadasiy katika kitabu *al-Kamal* katika wasifu wa Bilal, amesema: 'Na kwa mujibu wa maelezo yaliyopokewa ni kuwa hakumuadhinia yeoyote baada ya Mtukufu Mtume (saww), isipokuwa aliadhini mara moja tu alipofika Madina kwenda kumzuru Mtukufu Mtume (saww)." Na miongoni mwa waliotaja hilo ni al-Hafidh Abu al-Hajaj al-Maziy.

Pia zimepatikana habari kutoka kwa Umar bin Abdul-Aziz kuwa alikuwa akimtuma mjumbe kutoka Sham na kumwambia: 'Nifkishie salamu zangu kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww).' Na miongoni mwa waliotaja hilo ni Ibn al-Jawziy ndani ya kitabu *Muthirul-Gharam as-Sakin*, na pia amelitaja hilo Imam Abu Bakr Ahmad bin Amru bin Abi Aswim an-Nabil katika kitabu *Manasiku* bila kutaja sanadi na hivyo inalazimu kuthibitishwa, humo amesema: "Umar bin Abdul-Aziz alikuwa akimtuma mjumbe anayetoka Sham kwenda Madina ili akamfikishie salamu zake kwa Mtukufu Mtume (saww) kisha arejee."

Hivyo safari ya Bilal mwanzoni mwa zama za Sahaba, na safari ya mjumbe wa Umar bin Abdul-Aziz kutoka Sham hadi Madina mwanzoni mwa zama za Tabiina, haikuwa na lengo lingine isipokuwa kufanya ziara na kumtolea salamu Mtukufu Mtume (saww), na hawakuwa na sababu nyingine ya safari isipokuwa hiyo.

Ama wale ambao walisafiri kwenda Madina kwa ajili ya haja fulani, na wakawa wamekwenda kufanya ziara baada

ya kufika Madina au katika safari yao walikuwa na kusudio la kufanya ziara pamoja na kufanya jambo lingine, hao ni wengi:

Watangulizi wametofautiana kuhusu suala la kuanza kufanya ziara (kwa yule aliyekwenda kufanya Hijja) je ni bora kuanzia Madina kabla ya Makka au ni bora kuanzia Makka kabla ya Madina? Na mionganoni mwa watu ambao wameandika kuhusu mas'ala hii na kutaja tofauti iliyopo ni Imam Ahmad katika kitabu chake *al-Manasiku al-Kabiru*. Na mionganoni mwa watu waliochagua kuanzia Makka kisha kuja Madina na kwenye kaburi ni Imam Abu Hanifa.

Abu Bakr bin Husain al-Ajariy katika kitabu chake *as-Sharia* katika mlango 'Abu Bakr na Umar wazikwa pamoja na Mtukufu Mtume,' amesema: "Hakuna aalimu yeoyote wa mwanzo hadi wa sasa aliyejiandikia kitabu kutoka kwa mafaqihi wa Kiislamu na kukinasibisha kwake, anapoandika kitabu cha ibada ni lazima amwamuru kila anayefika Madina..... na kutaka kulizuru kaburi la Mtukufu Mtume (saww) na kuka Madina kutokana na ubora wake (Madina), isipokuwa ni lazima kila aalimu atakuwa amemwamuru, ameandika ndani ya kitabu chake, na amemfundisha namna ya kumsalimu Mtukufu Mtume na Abu Bakr na Umar (r.a.), hiyo ni kwa ulamaa wa Hijazi wa zamani na wa sasa, ulamaa wa watu wa Iraq wa zamani na wa sasa, ulamaa wa watu wa Sham wa zamani na wa sasa, ulamaa wa watu wa Khurasan wa zamani na wa sasa, ulamaa wa watu wa Yemen wa zamani na wa sasa, na ulamaa wa watu wa Misri wa zamani na wa sasa."

Na as-Sabkiy ameongeza kuwa: "Na ibara nyingi za wanafiqhi wa madhehebu ambao tumenukuu maneno yao katika mlango wa ziara zinapelekea safari (ya kumzuru Mtume)

kuwa mustahabu, kwa sababu wameonesha kuwa ni mustahabu kwa alhaj kufanya ziara baada ya kumaliza Hijja, na bila shaka mionganoni mwa mambo ya lazima katika kufanikisha ziara ni safari."

Kisha katika mlango wa nne amenukuu maelezo ya mafaqihi wa Kishafi, Kihanbali na Kimaliki yakionesha kuwa ni mustahabu kulizuru kaburi la Mtukufu Mtume (saww), bali ni mionganoni mwa Sunna na mustahabu bora kama ilivyo kwa Hanafi.

Miongoni mwa ulamaa ambao as-Sabkiy ametaja maelezo yao kuhusu hili ni: Husain bin Hasan al-Hulaymiy aliyefariki mwaka 403 A.H. na al-Mawrudiy aliyefariki mwaka 450 A.H. na Muhammad bin Mukrimu al-Karamaniy, na Abdullah bin Mahmud bin Baladahiy aliyefariki mwaka 683 A.H. na al-Qadhi Iyadh aliyefariki mwaka 544 A.H. na Abdul-Haqi bin Muhammad as-Swaqaliy aliyefariki mwaka 466 A.H. na wengineo.

As-Sabkiy amesema: "Na hilo limeelezwa pia na Mahanbali, Abul-Khitab Mahfudh bin Ahmad al-Kalwadhaniy amesema ndani ya kitabu *al-Hidayah* katika mlango wa mwisho wa sifa za Hijja: 'Atakapomaliza Hijja ni mustahabu kwake kulizuru kaburi la Mtukufu Mtume (saww) na kaburi la masahiba zake wawili."

Abu Abdullah Muhammad bin Ubaydullah bin Husain As-Samiriy amesema ndani ya kitabu *al-Mustaw'abu* katika mlango wa kuzuru kaburi la Mtukufu Mtume (saww): "Atakapofika katika mji wa Mtukufu Mtume ni mustahabu kwake kuoga....kisha atakwenda kwenye ukuta wa kaburi na kusimama pemberi, aliweke kaburi mbele ya uso wake na ak-

iweke kibla nyuma ya mgongo wake, na mimbari iwe kushotoni kwake.....” hapo ametaja namna ya kumtolea salamu na kuomba dua mpaka mwisho. Na mionganini mwa dua hiso ali-zotaja ni: “Ewe Mungu wangu, hakika mimi naelekea kwako kupidia Nabii wako (saww).” Hapo ametaja dua ndefu kisha akasema: “Na anapotaka kutoka atarudi kwenye kaburi la Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) na kuaga.

Hebu tazama mwandishi huyu ambaye ni mionganini mwa Mahanbali ambao mpinzani (Ibn Taymiyyah) anadai anafuata madhehebu yao, ni jinsi gani anaeleza jinsi ya kumweleke Mtukufu Mtume (saww).

Ibn al-Jawziy ndani ya kitabu chake kiitwacho *Muthirul-Gharam as-Sakin Ila Ashrafil-Amakin* ametenga mlango kamili unaozungumzia kulizuru kaburi la Mtukufu Mtume (saww), na humo ametaja hadithi ya Ibn Umar na hadithi ya Anas.²⁴

²⁴ *Shifaus-Siqam Fi Ziyarati Khayril-Anam* cha Taqiyud-Din as-Sabkiy: 53 – 67, kwa muhtasari.

USALAFI WA MISRI

Kaulimbiu ya Usalafi huko Misri ilidhihiri mwishoni mwa karne ya kumi na tisa na mwanzoni mwa karne ya ishirini, na huenda mtu wa kwanza kabisa kuitangaza ni mwanamageuzi Jamalud-Din al-Asadi Abadiy (1316 A.H.) na mwanafunzi wake mwaminifu kwake mwanamageuzi Sheikh Muhammad Abduh (1323 A.H.).

Ulamaa hawa hawakuitangaza kwa lengo la kuwadharau Waislamu wengine na kuwatuhumu kwa bidaa na ukafiri, bali wao waliitangaza kwa lengo la kuuamsha ummah pindi walipohisi udhaifu wa Waislamu, kudumaa kwao na kuwa kwao mawindo ya makafiri na walahidi, kwa sababu ya kujitenga kwao mbali na mafundisho ya Qur'an Tukufu na Mtume Mtukufu (saww).

Kuanzia hapa hawa wawili wakaanza kuuhimiza ummah wa Kiislamu juu ya kushikamana na Qur'ani, mafundisho yake matukufu na ghera na ushujaa mkubwa waliokuwa nao Waislamu wa mwanzo dhidi ya maadui na washambulaiji.

Hivyo Usalafi kwa maana hii si madhehebu wala si mfumo makhususi wa kifkra, bali ni sababu ya kuamshia hisia za ummah ili uweze kuutekeleza Uislamu kivitendo na ujitenge mbali na mipango inayowekwa na wakoloni inayopelekea kujitenga mbali na Uislamu, adabu zake na maadili yake.

USALAFI NA KUNDI LA UKH'WANUL-MUSLIMUNA

Kundi la Ukh'wanul-Muslimuna ambalo liliasiwa mwaka 1347 A.H. lilinyanya kauli ya kuwafuata Watangulizi wema na kurudi kwenye Uislamu katika mambo yote ya maisha, isipokuwa ni kwamba jamaa hawa walikuwa wazi kwa Waislamu wote, na lengo la kuundwa kundi hili lilikuwa ni kuwakusanya Waislamu katika hadhira moja na chini ya hema moja, na kuwakusanya pamoja kupitia kutenda kwa mujibu wa Kitabu, Sunna na yale waliyoafikiana Waislamu na yanayoafikiana na akili salama, na kupitia kitendo cha kupiga vita dhulma na uharibifu, na kufichua mipango inay-owekwa na ukoloni kwa lengo la kuitawala miji yao, na kuwapa mamlaka watawala wagandamizaji ambao wanatenda kwa maslahi ya maadui.

Na kwa ajili hii mwasisi wa jumuiya hii Hasan al-Bana, Mungu amsamehe, alitangaza kaulimbiu hii (ya kuwafuata Watangulizi wema na kurudi kwenye Uislamu katika mambo yote ya maisha) bila kulikufurisha kundi lolote wala kulinasibisha na bidaa au jambo jingine mionganoni mwa sifa mbaya.

Sasa kuna uhusiano gani kati ya hili na Usalafi wa Masalafi wa Masuudia ambao hawawaudhi wala kuwauwa isipokuwa Waislamu, na wala hawawapigi vita isipokuwa wanyonge mionganoni mwa Waislamu?!

USALAFI KATIKA ZAMA ZA MTUME (SAWW)

Huenda mtu akadhani kuwa ni baada ya kufariki Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) ndipo ilipotokea tofauti baina ya Masahaba kuhusu rai binafsi, na kwamba katika zama za Mtume wao walikuwa katika rai moja. Lakini ni kwamba kusoma maisha yao kunafichua tofauti iliyokuwepo baina yao kuhusu rai binafsi na maamuzi ya kisharia, licha ya kwamba Mtukufu Mtume (saww) alikuwa mionganini mwao, na ifuatayo ni mifano kuhusu hilo:

- 1. Kutofautiana kwoa kuhusu mateka wa Badri:**
Walitofautiana siku ya Badri kuhusu haki za mateka, Mtukufu Mtume (saww) alisema: "Mnasemaje kuhusu mateka hawa?" Abu Bakr akasema: "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Hao ni jamaa zako na ndugu zako, nenda kawaombe watubu huenda Mwenyezi Mungu atawakubalia toba." Umar akasema: "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Hawa wamekukadhibisha na kuku-fukuza, nenda kawakate shingo zao." Abdullah bin Rawaha akasema: "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Wewe uko katika bonde lenye kuni nyingi, washa moto katika bonde hili na uwatupe ndani ya moto." Mtume wa Mwenyezi Mungu akakaa kimya.²⁵

Na kutohana na kauli ya Mwenyezi Mungu:

²⁵ Tafsiri Ibn Kathiri: 2 / 325.

لَوْلَا كِتَابٌ مِّنَ اللَّهِ سَبَقَ لَمْسَكُمْ فِيمَا أَخْذَתُمْ عَذَابٌ عَظِيمٌ

“Lau isingelikuwa hukumu iliyotangulia kutoka kwa Mwenyezi Mungu, bila shaka ingeliwapata adhabu kubwa kwa yale mliyoyachukua.” (Sura Al-Anfal 8 : 68).

Inadhihiri kwamba wajibu waliokuwa nao Waislamu walioshiriki katika vita vya Badri ni kumuua kila wanayeweza kumuua (mionganini mwa mushrikina) na si kumteka na kumuweka kwa kusudio la kupata ghanima na fidia. Lakini wao hawakutekeleza wajibu wao bali kwa lengo tu la maslahi ya kidunia wao waliwafanya mateka maadui ambao walikuwa ndani ya uwezo wao wa kuweza kuwauwa, na kwa ajili ya kitendo chao hiki wakastahiki adhabu kubwa kama tu si kutanguliwa na majaaliwa ya Mwenyezi Mungu yaliyoinusuru dini yake na kumnusuru Nabii wake kuitia kundi dogo ambalo lilipigana pamoja na Mtume katika vita vya Badri. Na laiti pia kama si majaaliwa yake haya Mwenyezi Mungu angewaadhibu waumini ambao kwa ajili tu ya tamaa ya dunia waliwafanya mateka maadui wa Mwenyezi Mungu ambao walikuwa ndani ya uwezo wao wa kuweza kuwauwa.

Ikiwa huu ndio msimamo wa watu wa Badri ambao ni kutofautiana kuhusu haki waliyonayo mateka mionganini mwa mushrikina, na ikiwa huu ndio msimamo wa baadhi yao kati ya wale walioteka, kiasi kwamba kama si majaaliwa ya Mwenyezi Mungu basi wangestahiki adhabu, basi itakuwaje wawe ndio kiigizo na mfano wa kuigwa wa waliokuja baada yao?

2. Kutofautiana kwao katika sulhu ya Hudaibiya:

Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alitoka katika mwaka wa Hudaibiya akiwa na shabaha ya kuizuru Nyumba tukufu, na alikwenda pamoja na wanyama sabini wa sadaka ya kuchinja, Makuraishi walipogundua azma ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) na kuja kwake pamoja na Masahaba zake, walijaribu kumzuia asiingie Haram tukufu, na kuna mazungumzo yaliyofanyika mara kadhaa baina yake na Makuraishi, mpaka mwisho wakakubaliana kufanya sulhu na wakaandikiana mkataba ambao haya ndio maelezo yake:

“Wamekubaliana kuweka silaha chini kwa kuwaepusha watu na vita muda wa miaka kumi, muda ambao watu wataishi humo kwa amani na kuzuiana wao kwa wao (kufanya mashambulizi), kwa sharti kwamba ikiwa kuna mtu kutoka kwa Makuraishi atajiunga na Muhammad bila idhini ya walii wake basi atamrudisha kwao (kwa Makuraishi), na kama mtu mionganoni mwa walio pamoja na Muhammad atajiunga na Makuraishi basi hawatamrudisha kwake (kwa Muhammad). Na yeьте akipenda kuingia mkataba na makubaliano na Muhammad anaruhusiwa kuingia. Na yeьте akipenda kuingia mkataba na makubaliano na Makuraishi anaruhusiwa kuingia.²⁶

Ibn Hisham amesema: “Jambo lilipotimia na ikabakia tu kuandikwa, Umar alikurupuka na kumfuata Abu Bakr, akasema: ‘Ewe Abu Bakr hivi huyu si ni Mtume wa Mwenyezi Mungu?’ Akasema: ‘Ndio ni Mtume wa Mwenyezi Mungu.’ Umar akasema: ‘Hivi sisi si ni Waislamu?’ Akasema: ‘Ndio

²⁶ Siratu Ibn Hisham: 3 / 332, Daru Ihayi Turath al-Arabiyy.

ni Waislamu.' Umar akasema: 'Hivi wao si ni mushrikina?' Akasema: 'Ndio wao ni mushrikina.' Umar akasema: 'Basi ni kwa nini tunakuwa wanyonge katika dini yetu?' Abu Bakr akasema: 'Ewe Umar, Shikamana na amri yake, hakika mimi nashahidilia kuwa yeche na Mtume wa Mwenyezi Mungu.' Umar akasema: 'Na mimi nashahidilia kuwa hakika yeche na Mtume wa Mwenyezi Mungu.'

"Kisha Umar alimfuata Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) na kumwambia: 'Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu hivi wewe si ni Mtume wa Mwenyezi Mungu?' Akasema: 'Ndio mimi ni Mtume wa Mwenyezi Mungu.' Umar akasema: 'Hivi sisi si ni Waislamu?' Akasema: 'Ndio ni Waislamu.' Umar akasema: 'Hivi wao si ni mushrikina?' Akasema: 'Ndio wao ni mushrikina.' Umar akasema: 'Basi ni kwa nini tunakuwa wanyonge katika dini yetu?' Mtume akasema: 'Mimi ni mja wa Mwenyezi Mungu na Mtume wake, kamwe sintakhalifu amri yake na kamwe hatanibwaga.' Umar akawa anasema: 'Niliendelea kutoa sadaka, kufunga, kusali na kuwaacha huru watumwa kutokana na lile nililotenda siku ile, kwa kukhofia maneno yangu niliyotamka, mpaka nilipohisi sasa ni kheri."²⁷

Huu ndio msimamo wa Khalifa – ambaye Masuni wa naamini kuwa ndiye Sahaba wa pili kwa ubora – katika kujisalimisha mbele ya Mtume wa Mwenyezi Mungu, unadhani atakuwaje mbele ya asiyekuwa Mtume?

3. Kutofautiana kwao kuhusu kufunga safarini:

Muslim amepokea ndani ya Sahih yake kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alitoka mwezi wa Ramadhan na kwenda Makka siku ya ukumbozi wa Makka,

²⁷ Sirat Ibn Hisham: 3 / 331.

alifunga na watu wakafunga mpaka alipofika Kiraul-Ghamim, kisha aliomba birauli ya maji akaiinua juu kiasi kwamba watu wakaiona, kisha akanywa maji yale. Baada ya hapo akaambiwa: "Baadhi ya watu wamefunga." Mtume akasema: "Hao ni waasi, hao ni waasi."²⁸

Itaoana aje hali yao na kauli ya Mwenyezi Mungu:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تُقْدِمُوا بَيْنَ يَدَيِ اللَّهِ وَرَسُولِهِ وَاتَّقُوا اللَّهَ إِنَّ اللَّهَ سَمِيعٌ عَلِيمٌ

"Enyi ambao mmeamini! Msitangulie mbele ya Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia, Mjuzi."

(Sura Al-Hujurat 49 : 1).

Je kitendo chao hiki si ni kutangulia mbele ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake na kuutupilia mbali wahyi?

4. Kutofautiana kwao kuhusu maandiko ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww): Bukhari amepokea kutoka kwa Abdullah bin Abbas kuwa alisema: "Maradhi yalipomzidia Mtukufu Mtume (saww) alisema: 'Nileeteeni karatasi niwaandikieni maandiko ambayo kamwe hamtapotea baada yake!' Umar akasema: 'Maradhi yamemzidia, nasi tuna Kitabu cha Mwenyezi Mungu chatutosha.' Wakatofautiana na zogo likazidi, Mtume akasema: 'Ondokeni kwangu haipasi kuzozana

²⁸ Sahih Muslim: 129, Kitabu cha Swaumu, Mlango wa 15, Hadithi ya 1114, Uhakiki wa Swadqiyu Jamilul-Atari, Darul-Fikra- 1425 A.H.

mbale yangu.' Ibn Abbas akatoka huku akisema: 'Haki-ka msiba hasa ni msiba uliozuia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) asiandike maandiko yake."²⁹

Umar ameinasibisha na hali ya kuzidiwa na maradhi ile amri ya Mtume (saww) ya kutaka aletewe karatasi, lakini katika nukuu nyingine ni kuwa aliinasibisha na kubobokwa, licha ya kwamba Bukhari hajataja jina la msemaji. Bukhari amepokea kutoka kwa Ibn Abbas kuwa alisema: "Siku ya Alhamisi; ni ipi siku hiyo ya Alhamisi." Kisha akalia sana kiasi kwamba ndevu zake zikalowa machozi, akasema: "Mtukufu Mtume (saww) alizidiwa na maradhi siku ya Alhamisi, akasema: 'Nileteeni karatasi niwaandikieni maandiko ambayo kamwe hamtapotea baada yake hayo!' Wakazozana na haipasi kuzozana mbele ya Mtume, wakasema: 'Mtume wa Mwenyezi Mungu anabobokwa.'"³⁰

Hii ndio adabu ya watu waliokuwa wamemzunguka Mtukufu Mtume (saww), unawaona wakinasibisha maneno yake na hali ya kuzidiwa na maradhi au na kubobokwa na kutokujua asemalo.

5. Kutofautiana kwao kuhusu kifo cha Mtukufu Mtume (saww): Hao Watangulizi wema walitofautiana katika suala bayana na la wazi kabisa, pindi Mtukufu Mtume (saww) alipofariki na habari za kifo chake zikaenea Madina tukufu, Masahaba wakakusanyika kwenye nyumba ya Mtukufu Mtume (saww) ili wamuandae, huku ukimya na huzuni vikiwa vimetawala kwa waliokuwepo. Ni wakati huo mara alisimama Umar bin Khattab na kutoa hotuba, akasema:

²⁹ Sahih Bukhari, Namba 114.

³⁰ Sahih Bukhari, Namba 3053.

“Hakika watu mionganini mwa wanafiki wanadai kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) amefariki, na hakika wallahi Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) hajafariki, lakini amekwenda kwa Mola wake kama alivyokwenda Musa bin Imran, alitoweke mbali na watu wake muda wa siku arubaini kisha alirejea kwao baada ya kudaiwa kuwa amefariki. Wallahi Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) atarejea kama alivyorejea Musa na ataikata mikono na miguu ya watu waliodai kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) amefariki.”³¹

Maneno ya Khalifa yalikuwa na athari kubwa kwa wenye akili ndogo baina ya wale waliokuwepo, na khofu kubwa ya kutuhumiwa kwa unafiki, mpaka alipofika Abu Bakr baada ya kupata habari, alitua katika mlango wa msikiti huku Umar akiwa anawahutubia watu, Abu Bakr akasema: “Enyi watu hakika aliyekuwa akimwabudu Muhammad ajue hakika Muhammad ameshakufa, na aliyekuwa akimwabudu Mwenyezi Mungu ajue hakika Mwenyezi Mungu yu Hai Mzima wa milele.” Kisha akasoma Aya hii:

وَمَا مُحَمَّدٌ إِلَّا رَسُولٌ قَدْ خَلَتْ مِنْ قَبْلِهِ الرُّسُلُ أَفَإِنْ مَاتَ أَوْ قُتِلَ انْقَبَّتْمُ عَلَىٰ
أَعْقَابِكُمْ وَمَنْ يَنْقَلِبْ عَلَىٰ عَقِبَيْهِ فَلَنْ يَضُرَّ اللَّهُ شَيْئًا وَسَيَجْزِي اللَّهُ الشَّاكِرِينَ

“Hakuwa Muhammad ila ni Mtume; wamekwisha pita Mtume kabla yake. Je, akifa au akiuliwa mtarudi nyuma? Na atakayerudi nyuma hatamdhuru kitu Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu atawalipa wenye kushukuru.” (Sura Al-Imran 3:144) Anasema: Wallahi kana kwamba watu hawakuwa

³¹ Sirat Ibn Hisham: 4 / 305.

wanajua kuwa Aya hii iliteremka, mpaka alipoisoma Abubakr siku hiyo.

Anasema: Watu wakaichukua kutoka kwa Abu Bakr na ikawa katika vinywa vyao.

Anasema: Abu Huraira alisema: Umar alisema: "Wallahi sikuijua mpaka niliposikia Abu Bakr akiisoma, nikaingiwa na ganzi mpaka nikaanguka ardhini miguu yangu ikiwa haina nguvu ya kunibeba, na nikajua kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) amefariki."³²

Na si dhani kwamba Umar alikuwa ana shaka sana na kifo cha Mtukufu Mtume (saww), itakuwaje awe na shaka wakati kifo ni kawaida mionganoni mwa kawaida za Mwenyezi Mungu alizowawekea waja wake, na hakuna hata mtu mmoja kati ya waja wake aliyekwenda kinyume na kawaida hiyo, tena masikio ya Masahaba yamejaa kauli ya Mwenyezi Mungu: **"Kwa hakika wewe utakufa, na wao watakuwa."**

Na huenda kilichomfanya aanzishe mkanganyiko huu kuhusu kifo cha Mtukufu Mtume (saww) ni suala la kisia-ili Waislamu wasikongamane katika jambo la Ukhilifa na Uimamu juu ya mtu mmoja, mpaka atakapokuja Abubkri na wanaofuata rai yake na nadharia yake (katika ukhalifa), waungane na kuwa na msimamo mmoja kuhusu ukhalifa, kama hali ilivyokuwa baada ya kuja Abubkri, na yeye kuungana naye hadi ndani ya ukumbi wa Saqifa Bani Saad, kama utakavyosikia.

6. Tukio la Saqifa: Yeyote mwenye kusoma historia ya ukumbi wa Saqifa ambao humo yalikusanyika makabila mawili: Khazraji na Aws ili wadabiri suala

³² *Sirat Ibn Hisham*: 4 / 306.

la ukhalifa, kisha likaungana nao kundi dogo la Muhajirina lisilozidi watu wanne au watano, ataona uweupo wa mpasuko mkubwa baina ya Watangulizi wema kuhusu suala la ukhalifa, huku kila mmoja akivutia kamba upande wake.

Huyu hapa msemaji wa Ansari Sa'd bin Ubadah anainua sauti yake na kusema: "Enyi kundi la Ansari, ninyi ni watan-gulizi katika dini na mna fadhila katika Uislamu kushinda kabilia lolote lile la Kiarabu, hakika Muhammad (saww) aliishi na jamaa zake miaka kumi akiwalingania kumwabudu Rahman na kuachana na masanamu, hakuna aliyemwamini katika jamaa zake isipokuwa watu wachache, na walikuwa hawana uwezo wa kumlinda Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) wala kuipa nguvu dini yake, wala kujitetea wao wenyewe kama wakishambuliwa, mpaka Mwenyezi Mungu alipowaleteeni fadhila na kuwaleteeni heshima na kuwapeni neema, akawaruzukuni imani ya kumwamini yeye na Mtume wake na kumlinda yeye na Masahaba zake, kumpa nguvu yeye na dini yake, na kupigana jihadi dhidi ya maadui zake, ninyi mkawa wakali kuliko watu wote kwa walio maadui zake miongoni mwenu, na mkawa imara dhidi ya walio maadui zake miongoni mwa wasiokuwa ninyi, mpaka Waarabu wakafuata amri ya Mwenyezi Mungu kwa kupenda au kwa kutokupenda..."

Hii ndio mantiki ya Ansari, hebu sasa tusikie mantiki ya kundi la Muhajirina ambao walikuwepo Saqifa. Alisimama Abu Bakr na kusema:

"Hakika kati ya jamaa zake (saww) Mwenyezi Mungu amewateua Muhajirina wa mwanzo kwa kumwamini yeye, kumsaidia na kufanya subira pamoja naye wakati wa makali

ya adha za jamaa zao dhidi yao, wakati wa kuwakadhibisha kwao, na wakati ambapo watu wote walipokuwa nguvu moja dhidi yao. Hawakuogopa kwa sababu ya uchache wa idadi yao, kwa sababu ya kuchukiwa na watu na kuungana kwao dhidi yao. Hakika wao ndio watu wa kwanza kumwabudu Mwenyezi Mungu ardhini na kumwamini Mwenyezi Mungu na Mtume, na wao ndio vipedhi vyake na jamaa zake na ndio watu wenye haki zaidi na jambo hili baada yake na wala hata-wapinga katika hilo isipokuwa dhalimu.

“Nanyi enyi Maansari ni watu ambao haikanushiki fadhila yao katika dini wala kutangulia kwao katika Uislamu, Mwenyezi Mungu amewaridhia kwa kuwa watetezi wa dini yake na Mtume wake, na ni kwenu ndiko alikofanya sehemu ya kuhamia kwake, na ni kati yenu ndiko alikotoa wake zake wengi na masahaba zake. Hivyo baada ya Muhajirina wa mwanzo hakuna mwenye cheo kuwashinda ninyi, hivyo sisi tuwe maamiri na ninyi muwe mawaziri, msiache kutushauri nasi tusiamue mambo bila ninyi.”

Tabariy anasema: “al-Hubab bin al-Mundhir bin al-Jumuhi akasimama na kusema: ‘Enyi watu wa Maansari! Limilikini wenyejambo lenu, kwani hakika watu wako katika kundi lenu na chini ya kivuli chenu na hawezi yeyote kujaribu kwenda kinyume nanyi, na watu hawatofuata isipokuwa rai yenu, nyinyi ndio wenye nguvu na wenye mali na wenye idadi kubwa ya watu na wenye ulinzi na tajriba, wenye nguvu na ushujaa. Hakika watu wanatazama lile mtakalotenda nyinyi, hivyo msitofautiane ikaja kuharibika rai yenu na kumpunguka nguvu yenu. Bila shaka hawa wamekataa isipokuwa kwa yale mliyoyasikia, hivyo basi kwetu atoke amiri na kwao atoke amiri.’

“Umar akasema: ‘Hilo haliwezekani, panga mbili hazikai katika ala moja, Wallahi Waarabu hawakubali kuwatawalisheni na hali Mtume wao hatokani na nyinyi. Lakini Waarabu hawakatai kuwatawalisha jambo lao wale ambao unabii unatokana nao na walii wa mambo yao anatokana nao. Nasi juu ya hilo tuna hoja dhahiri na utawala bayana juu ya mwenye kupinga mionganoni mwa Waarabu. Ni nani atatupinga katika utawala wa Muhammad na uongozi wake wakati sisi ndio vipenzi vyake na jamaa zake!? Isipokuwa yule mwenye kuendekeza batili au mwenye kuelemea katika madhambi au mwenye kujikita katika maangamio.’

“al-Hubab bin al-Mundhir bin al-Jumuhi akasimama na kusema: ‘Enyi Maansari! Limilikini (jambo hili) kwa mikono yenu na wala msisikie aliyosema huyu na jamaa zake wakaja kuondoka na fungu lenu katika jambo hili, na kama waki-kataa kukufuateni basi watoweni nje ya mji (wenu) huu na waongozeni nyinyi katika mambo haya, kwani nyinyi wallahi ndio wenyе haki na jambo hili kuliko wao, kwa sababu kwa panga zenu wameingia katika dini hii walioingia wale waliokuwa hawana dini. Mimi ndiye kimbilio la mawazo na mwenye uwezo mkubwa wa mawazo, na wallahi mkipenda tutarudi kama mwanzo.’

“Umar akasema: ‘Mwenyezi Mungu akuuwe.’ Akajibu: ‘Akuuwe wewe.’ Abu Ubaydah akasema: ‘Enyi kundi la Maansari! Hakika ninyi ndio watu wa kwanza kuunusuru na kuupa nguvu, hivyo msiwe wa kwanza kubadili na kugeuza.’ Hapo akasimama Bashiri bin Saad (Abu Nuuman bin Bashir) na kusema: ‘Enyi kundi la Maansari! Kama sisi tulikuwa wenyе fadhila katika kupigana dhidi ya Mushrikina na kutangulia katika dini hii si kwa ajili ya jingine isipokuwa ni kwa ajili

ya kupata radhi za Mola wetu, kumtii Nabii wetu na kuzichumia nafsi zetu, hivyo hatupasi kuwaringia watu kwa hilo na wala hatupasi kuitafuta dunia kwa hilo, kwani hakika Mwenyezi Mungu ndiye aliyetuneemesho hilo. Fahamuni hakika Muhammad atokana na Makuraishi na jamaa zake ndio wenye haki zaidi na jambo hili, na ninamuomba Mwenyezi Mungu kamwe asinione nikiwa napingana nao katika jambo hili. Mcheni Mwenyezi Mungu na wala msiwakhalifu wala kuwapinga.”³³

Kila kundi likijiona kuwa ndio lenye haki zaidi na ukhalifa, na kila kundi likilitishia kundi jingine, lakini mwisho hali ilibadilika na kuwanufaisha Muhajirina katika hali isiyotegemewa. Hiyo ni kwa sababu Awsi waliona kuwa kumpa uamiri Saad bin Ubadah ambaye ni Khazraji kutawapa Makhazraji ubora na fadhila juu yao, hivyo kiongozi wao Usaydu bin Hadhir akasema: “Wallahi kama mtamtawalisha Khazraji juu yenu hata mara moja basi hali hiyo itaendelea kuwa fadhila yao juu yenu na kamwe hawatawashirikisheni pamoja nao kwa kuwapa fungu lolote (katika fadhila hiyo). Hivyo simameni na mumpe kiapo cha utii Abu Bakr.” Wakasimama na kumpa kiapo cha utii, hivyo wakamkataa Saad bin Ubadah na Makhazraji kwa kukhalifu yale waliyokuwa wamekubaliana katika jambo lao, wakasimama na kuanza kutoa kiapo cha utii.³⁴

Wakanyanya watu kutoka kila upande na kwenda kumpa kiapo cha utii Abu Bakr, na walikaribia kumkanya ga Saad bin Ubadah, ndipo baadhi ya watu mionganoni mwa wafuasi wa Saad wakasema: “Mwepukeni Saad msimkany-

³³ *Tarikh Tabari*: 2 / 457 – 458, Chapa ya Muasasatul-Aalamiy.

³⁴ *Tarikh Tabari*: 2 / 458, Chapa ya Muasasatul-Aalamiy.

age." Umar akasema: "Muuweni, Mwenyezi Mungu amuuwe." Kisha Umar alisimama juu ya kichwa chake na kusema: "Nimekusudia kukukanyaga kanyaga mpaka vinyofoke viungo vyako." Saad akazishika ndevu za Umar na kusema: "Wallahi uking'oa hata unywele mmoja hutarejea na meno yako yakiwa kinywani." Abu Bakr akasema: "Tulia ewe Umar, hapa upole ndio wenyewe kufaa zaidi." Ndipo Umar akaachana naye. Saad akasema: "Wallahi ningekuwa na nguvu ambazo kwazo naweza kusimama, basi katika njia zote na vichochoro vyote ungesikia mlionna kutoka kwangu, mlionna ambao ungeku-fukuza wewe na jamaa zako. Kwani wallahi ningekukutani-sha na watu ambao wewe ulikuwa mfuasi miongoni mwao na si kiongozi. Nibebeni toka sehemu hii." Wakambeba na kumwingiza ndani ya nyumba yake na akaachwa humo siku kadhaa."³⁵

Nasema: Hebu tuchukulie kuwa mtangaza haki (Mtume wa Mwenyezi Mungu) aliaachia Shura mamlaka ya kuteua Khalifa, je ni kweli aliipa mamlaka Shura kama hiyo ambayo mazingira yake yote yalienea hisia za chuki, husuda, ubaguzi, ushindani na ugomvi uliokuwepo baina ya wanashura hiyo huku wakizozana kama hivyo kiasi cha kuweza kila mmoja kumlani mwingine na kujitenga naye? Au mamlaka aliyaacha mikononi mwa Shura yenye akili na busara ambayo itadurusu maslahi na vigezo ambavyo ni lazima awe navyo yule aliye Khalifa wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), kisha itamsimika yule aliyekusanya sifa hizo?

Kwa kweli Shura iliyokaa katika ukumbi wa Saqifa Bani Saad haikuzingatia mambo haya, bali ni kila kundi lilidai kuwa lastahiki kuchukua ukhalifa kwa kutumia vigezo vyta

³⁵ *Tarikh Tabari*: 2 / 459, Chapa ya Muasasatul-Aalamiy.

zama za Ujahiliya. Hili hapa kundi la Maansari linadai kuwa wao ndio waliompokea na kumnusuru Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) pindi jamaa zake walipomtoa nyumbani kwake na nchini kwake. Mkabala na hao tunalikuta kundi lingine amba ni Muhajirina linadai kuwa wao ndio wastahiki ukhalifa kwa sababu wao ndio jamaa zake na asili yake.

Je kigezo cha mtu kupata ukhalifa wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) ni moja kati ya madai haya mawili? Kwa kweli vigezo vyote viwili havina sifa ya kufaa kuwa kigezo cha kumpa mtu ukhalifa wa Mtume na uongozi wa ummah katika mapambano ya maisha, kwani hakika anayefaa kuwa Khalifa ni yule mwenye sifa na fadhila za Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww). Kwa ibara nyingine ni kwamba mwenye sifa ya uadilifu, mwenye kuijua kikamilifu Qur'an na Sunna na yale ambayo ummah unayahitajia katika mustakbali wake, ikiwa ni pamoja na kuwa na uwezo kamili wa kuedesha mambo, siasa ya ummah na mengineyo mionganoni mwa sifa alizokuwa nazo Mtukufu Mtume, ndiye anayefaa kuwa Khalifa.

Vyovyote iwavyo ni kwamba limeshapita suala la Saqifa ambalo lilizua mjadala na ugomvi hadi watu wakaweza kuwanyaaga wengine kwa miguu yao, na hiyo inaonesha kuwa watangulizi wema amba wanachukuliwa kama kiigizo che-ma, hawakulijadili suala la ukhalifa kwa mtazamo wa maslahi ya ummah yaliyo mbali na maslahi binafsi, na wala Khalifa hakuchukua ukhalifa isipokuwa chini ya kivuli cha ugomvi, hila na sera za kijahiliya.

- 7. Kutofautiana kwao katika Itikadi na Sharia:** Mifano ya kutofautiana kwa watangulizi tulioitaja huko nyuma ni ile iliyotokea katika zama za Mtukufu Mtume

(saww) na muda mchache baada ya kufariki kwake, ama kutofautiana kwao katika tasnia ya Theolojia na Sharia baada ya kufariki Mtukufu Mtume (saww), ni mingi.

Ama upande wa itikadi inakutosha kwamba makundi ya Kiislamu ambayo yameorodheshwa na wanatheolojia hadi kufikia makundi sabini na tatu, yote yalizalika na kukua katika karne tatu za kwanza.

Huyu hapa Imam al-Ash'ariy ameandika maneno yao na madai yao na kuwajibu ndani ya kitabu chake *Maqalatil-Islamiyina Waikhtilaful-Muswalina*, yote hayo ilikuwa ni kabla ya kutimu karne ya tatu.

Katika maudhui hii anafuatiwa na kitabu *al-Faraqu Baynal-Firaqi* cha Abu Mansuri Abdul-Qahir al-Baghdadiy aliyefariki mwaka 429 A.H. alikiadilisha kitabu cha Imam al-Ash'ariy na kukosoa baadhi ya mambo ambayo aliyahusisha na upuizi wa maneno na kwamba ilikuwa ni kunakili itikadi kwa msukumo wa ushabiki binafsi (taasubu).

Na kinafuata kitabu *al-Milalu Wan-Nahli* cha mwana theolojia wa Kiash'ariy Abul-Fat'h Muhammed bin Abdul-Karim as-Shuhrustaniy aliyefariki mwaka 548 A.H.

Makundi haya ambayo wanahadithi wanajitenga nayo yalidhihiri ndani ya karne tatu za mwanzo, itakuwaje sasa Mtukufu Mtume (saww) azisifu karne hizi kuwa ndio karne bora kushinda nyingine na awafanye watu wa karne hizo kuwa ndio kiigizo na mfano wa kuigwa? Na ni kundi lipi kati ya haya ndio kiigizo na mfano wa kuigwa?

Ama kwa upande wa Sharia ni katika karne hizo hizo zilizotajwa ndimo yalimozuka na kudhiihiri madhehebu mengi ya

Kifiqhi, isipokuwa ni kwamba baadhi ya viongozi waliogopa madhehebu haya yasije kuenea hivyo wakayafunga madhehebu katika madhehebu nne na kuyabatilisha mengine.

Al-Maqriziy anasema: "Utarwala wa makadhi wanne ulien-delea kuanzia mwaka 665 A.H. hadi kiasi kwamba katika miji ya Kiislamu hakukubakia madhehebu yoyote ya Kiislamu in-ayotambulika isipokuwa madhehebu hizi nne. Na yejote ali-yejufata madhehebu isiyokuwa moja kati ya hiso nne alifanya-wa adui na kukataliwa na hakupewa ukadhi wala ushahidi wake haukukubaliwa na wala hakutangulizwa kutoa khutba wala kuwa Imam au kumdarisisha mtu, maadamu tu si mfua-si wa moja kati ya madhehebu hizi nne. Wanafiqhi wa miji hii (ya Kiislamu) katika muda wote huu walitoa fatwa iliyosema ni wajibu kufuata madhehebu hizi nne na ni haramu kufuata zisizokuwa hiso, na walifanya kazi hili mpaka leo hii."³⁶

³⁶ *Al-Khututu cha al-Maqriziy*: 2 / 344.

WATAWALA WA KARNE TATU BORA

Umeshatambua ukubwa wa ikhtilafu iliyokuwepo baina ya Watangulizi katika kipindi cha karne tatu bora. Laajabu zaidi ni kwamba watawala wa kipindi hicho ndio watawala madhalimu na mafisadi kushinda watawala wote wa karne kumi na nne, na ndio walioopea zaidi katika kumwaga damu na kuwagandamiza raia wema, kiasi kwamba mmoja wao (naye ni Ubaydullah bin Ziyad bin Abihi) aliwahutubia watu kwa kusema: "Enyi watu wa Basra, hakika Amirul-Muuminina (yaani Yazidi) ukiachia mbali ugavana wa Basra amenipa pia ugavana wa Kufa, nami sasa nakwenda huko.....naapa kwa Mwenyezi Mungu ambaye hapana mungu isipokuwa Yeye, ikiniflikia habari kuwa kuna mtu ye yeyote mionganoni mwenu amekhalifu au kuanzisha machafuko, basi nitamuwa yeye na walii wake, na nitamwangamiza wa chini mpaka wa juu, na mwema mpaka muovu, mpaka mnyooke.³⁷

Kabla hatujaonesha mifano ya dhulma na ukandamizaji wa Bani Umaiyyah na Bani Abbas uliyofanywa ndani ya karne tatu za mwanzo, hebu tutaje hapa tukio la hatari lililotokea siku chache baada ya kufariki Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), nalo linaonesha kwanza ni kiasi gani Watangulizi walivyotofautiana, pili ni jinsi gani walivyoharakisha kufanya dhulma. Mtu atawezaje kufuata nyayo zao na kuhukumu kuwa wao ni bora wakati yamethibiti kwao mambo haya mawili katika maisha ya Watangulizi: Tofauti na dhulma?

³⁷ Abu Hanifa Ahmad bin Daud ad-Daynuriy, al-Akhbar Tuwal: 232.

Tunaposema tukio hatari tunakusudia tukio la kuuawa Sahaba Malik bin Nuwayrah al-Yar'buiy at-Tamimiyy, aliyeuwawa zama za Khalifa wa kwanza. Wanahistoria wanasema:

Hakika Malik bin Nuwayrah alikuwa chifu, mpiganaji na mshairi, ni mmoja kati ya machifu wa zama za Jahiliyah, alikuwa akiitwa Farisu Dhil-Khimari, na na lakabu yake ny-ingine ni al-Jaful, hiyo ni kwa kuwa alikuwa na nywele ny-ingi. Alikwenda kwa Mtukufu Mtume (saww) na akasilimu, na Mtume akampa mamlaka ya kukusanya Zaka za jamaa zake wa Bani Yarbuu, alipofariki Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) na kuchukua ukhalifa Abu Bakr, Malik aliwagawia jamaa zake mali za Zaka, ndipo Khalid bin Walid akamwendea.

Abu Qatadah al-Harith bin Rab'iy al-Ansariy ambaye ni mionganoni mwa walioshuhudia tukio anasema: "Hakika wao alipowajia jamaa waliwatia khofu kwa kuwaendea usiku, jamaa wakachukua silaha, tukasema: 'Sisi ni Waislamu.' Wakasema: 'Na sisi ni Waislamu.' Tukasema: 'Basi silaha mlizonazo ni za nini?' Wakatuambia: 'Nanyi silaha mlizonazo ni za nini?' Tukasema: 'Kama mko kama mlivyosema basi wekeni silaha chini!' Wakaweka silaha chini kisha tukaswali na wao wakaswali."

Kisha walimchukua mateka Malik na masahaba zake, na pamoja naye alimchukua mke wake, naye alikuwa ni mfano wa uzuri, Khalid alipomfuata Malik bin Nuwayrah ili amkate shingo yake, Malik alimgeukia mke wake na akamtazama, kisha akasema: 'Ewe Khalid ni kwa ajili ya huyu waniuwa.' Kisha Khalid alimuoa mke wa Malik baada yake (siku hiyo), naye ni Ummu Tamim binti ya al-Min'hal, na akamwingilia (usiku huo huo), ndipo kundi la Masahaba akiwemo

Umar bin Khattab na Abu Qatadah al-Ansariy likamtuhumu (kwa zinaa).

Umar alipofikiwa na habari za kuuwawa Malik na jamaa zake aliongea mengi mbele ya Abu Bakr, na akasema: "(Khalid) Ni adui wa Mwenyezi Mungu, amemfanyia uadui mwislamu na hatimaye kamuuwa, kisha amemwingilia mke wake!"

Ama Abu Qatadah al-Ansariy, yeeye alighadhibika kiasi kwamba alikula kiapo kwa kumwahidi Mwenyezi Mungu kuwa baada ya tukio hilo kamwe hatashiriki vita pamoja na Khalid.

Alipofika Khalid kama kiongozi wa kikosi, aliiingia msikitini huku akiwa amechomeka mishale kwenye kilemba chake, ndipo aliposimama Umar na kuichomoa mishale toka kichwani kwake na kuivunja vunja, kisha akasema: "Yaani umemuua mwislamu kisha umemwingilia mke wake, Wallahi nitakupopoa kwa mawe yako." Aliyasema hayo huku Khalid akiwa kimya, kisha aliendelea na njia yake mpaka akaingia kwa Abu Bakr, akajitetea kwake naye akakubali utetezi wake na akamsamehe yale yaliyotokea katika vita vyake hivyo.³⁸

Na tukio la msiba wa Karbala linaongoza katika orodha ya misiba iliyowapata Waislamu, na yeьте atakayedurusu na kusoma vipengele vyake viliyyojaa matukio ya kuumiza atagundua ususuavu wa moyo na ukatili waliokuwa nao watawala, huku wakiwa mbali kabisa na maadili ya kiutu, kiasi kwamba waliweza kumchinja mtoto mchanga mikononi mwa mzazi wake, na wakabeba vichwa juu ya ncha za mikuki

³⁸ Tazama *Tarikh Tabari*: 4 / 95 – 99. *Kitabul-Futuh* cha Ibn Aatham al-Kufiy: 1 / 20 -23. *Al-Aghaniy*: 15 / 298 – 307.

kutoka mji mmoja hadi mji mwengine, vilikuwa ni vichwa sabini na mbili, vikiongozwa na kichwa cha ua la Mtukufu Mtume (saww) Abu Shuhadai Husain bin Ali (as).

Huyu hapa al-Mas'udiy mwanahistoria anayetumainiwa anasema: "Husain (as) aliendelea kupigana mpaka akauwawa (r.a). Na aliyechukua jukumu la kumuwa ni mtu mmoja kutoka Madh'haji, na ndiye aliyekata kichwa chake na kwenda nacho kwa Ibn Ziyad huku akisoma beti za shairi:

Jaza kipando changu fedha na dhahabu, mimi nimemuuwa Mfalme aliyeihadhiwa. Nimemuuwa mtu aliye bora kushinda watu wote kwa mama na baba, na ndiye mbora wao zinapotajwa nasaba.'

Ibn Ziyad akamtuma kwa Yazid bin Muawiya akiwa pamoja na kichwa (cha Husain), alipoingia kwa Yazid alimkuta akiwa pamoja na Abu Barzatu al-Aslamiy, kilipowekwa kichwa mbele yake (Yazid) alianza kuingiza kijiti ndani ya kinywa chake huku akisoma ubeti wa shairi: 'Tunapasua kichwa cha mmoja kati ya wanaume waliotusumbua sana, nao alikuwa ni watu wavunja haki na madhalimu.' Ndipo na Abu Barzatu al-Aslamiy akamwambia: 'Ondo kijiti chako, Wallahi nilimuona Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) mara kwa mara akiweka mdomo wake juu ya mdomo wake (wa Husain) na kuubusu.'³⁹

Hakika yaliyotokea Karbala ni tukio kubwa la kusikitisha, ni mara chache sana dunia kushuhudia tukio kama lile. Suyutiy anasema: "Husain aliuawa Karbala, na katika kuuawa kwake kuna kisa kirefu ambacho moyo hauwezi kukitaja.

³⁹ *Murujud-Dhahbi*: 3 / 61. *al-Akhbar Tuwal*: 258 – 261.

Hakika sisi sote ni wa Mwenyezi Mungu na hakika kwake yeye tutarejea.” Kisha alitaja athari zilizotokea baada ya kuuawa Husain (as), kisha akasema: “Alipouawa Husain na watoto wa baba yake, Ibn Ziyad alipeleka vichwa vyao kwa Yazid. Kwanza alifurahia kuuawa kwao, kisha alijutia pale Waislamu walipomjia juu kutokana na tukio hilo na watu wakamchukia, na ilikuwa ni haki yao kumchukia.”⁴⁰

Na katika mwaka wa sitini na tatu Yazid bin Muawiya ali-pata habari kuwa watu wa Madina wamemuasi na kumkataa, akawatumia jeshi kubwa na kulipa amri ya kuwaua, kisha liende Makka kumuua Ibn Zubair. Lilifika Madina na ndipo likatokea tukio la al-Hurah kwenye mlango wa Twiba, ni kitu gani kitakujulisha ni lipi hilo tukio la al-Hurah? Amelitaja Hasan al-Basriy kwa kusema: “Wallahi hakukaribia kuokoka hata mmoja mionganini mwao, waliuawa humo viumbi miongoni mwa Masahaba (r.a.) na wengineo, mali za Madina zikaporwa, na wakabakwa vigori elfu moja. Hakika sisi sote ni wa Mwenyezi Mungu na hakika kwake yeye tutarejea.”

Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: ‘Yeyote atakayewatia khofu watu wa Madina basi Mwenyezi Mungu atamtia khofu, na itakuwa juu yake laana ya Mwenyezi Mungu, Malaika na watu wote.’ Kaipokea Muslimu.

Sababu ya watu wa Madina kumkana Yazid ni kwa kuwa alipindukia katika maasi. Al-Waqidiy ameandika kwa njia kadhaa kwamba Abdullah bin Handhalah alisema: “Wallahi hatukutoka dhidi ya Yazid isipokuwa tulipohisi kuwa sasa tutapigwa na mawe kutoka mbinguni. Hakika yeye ni mtu anayelala (anayewaingilia) na mama zake, mabinti zake na dada zake, anakunywa pombe na kuacha Swala.”

⁴⁰ *Tuarikhul-Khulafai*: 247 – 248, Darul-Jayli, chapa ya mwaka 1408 A.H.

Ad-Dhahbiy amesema: Yazid alipowatendea watu wa Madina yale aliyowatendea – ikiwa ni pamoja na kunywa pombe na kutenda maovu - watu walikuja juu dhidi yake na wakatoka dhidi yake watu zaidi ya mmoja na Mwenyezi Mungu hakutia baraka katika umri wake. Jeshi la al-Hurah lilikwenda Makka kumuua Ibn Zubair, ndipo kiongozi wa jeshi akafariki njiani na nafasi yake ikachukuliwa na kiongozi mwengine, walipofika Makka walimzunguka Ibn Zubair wakamuua na kumshambulia kwa manati. Hiyo ilikuwa ni katika mfunguo tano mwaka sitini na nne, na kutokana na moto wao kitambaa cha Kaaba, paa lake na mapembe ya kondoo aliyoletewa Ibrahim badala ya Ismail ambayo yaliwu kwenye paa, vyote viliungua. Na ndipo Mwenyezi Mungu akamwangamiza Yazid katika mwaka huu huu katika nusu ya mfunguo tano.⁴¹

Hii ni baadhi tu ya mifano ya kuumiza ambayo hukifanya kifua cha mtoto mchanga kiwe cha mtu mzima. Na atakayesoma historia ya watoto wa Abu Sufiyan kisha historia ya watoto wa Mar'wan ataona jinsi Waislamu katika zama za karne bora walivyokutana na watawala madhalimu wenye kuuwa bila huruma na wanyang'anyi wasio na huruma moyoni.

Mtu anawenza kudhani kuwa balaa lilianza baada ya kufariki Muawiya mwaka wa sitini na kuwa zama zake zilikuwa zama za amani, usalama na wema, lakini ukweli ni kwamba tunaposoma katika kurasa za maisha yake tunakuta kuwa yeeye ndiye aliye kuwa msingi wa misiba hii.

Tunasoma katika moja ya kurasa za maisha yake kuwa: Hujri bin Adiy al-Kindiy alikuwa mionganoni mwa Masahaba wakubwa, na mionganoni mwa masahaba wakubwa wa Ali (a.s.),

⁴¹ *Taarikhul-Khulafai*: 249.

Muawiya alipompa ugavana wa Kufa na Basra Ziyada bin Abihi alidhihirisha ukandamizaji na mwenendo mbaya kadiri alivyoweza, Hujri alikuwa akimkosoa na siku moja Hujri na jamaa zake walimrushia changarawe kwa kuchelewesha Swalla (Na inasemekana kuwa waliyemrushia ni Amru bi Huraythi, khalifa wa Ziyad huko Kufa), ndipo Ziyad akamwandikia barua Muawiya kumweleza tukio hilo, naye akamwamuru ampeleke kwake, akampeleka chini ya ulinzi wa askari kumi na wawili, na wakatengeneza ushahidi wa uwongo kuwa Hujri na jamaa zake walimtukana Khalifa na kuwaita watu ili wapambane kivita na Muawiya bin Abi Sufiyan.

Walipofika Maraju Adhrau (eneo ambalo ni umbali wa mai-li kumi na mbili kutokea Damascus) Hujri alisema: "Wallahi mimi ndiye mwislamu wa kwanza kubwekewa na mbwa wake (yaani wa Maraju Adhrau) katika njia ya Mwenyezi Mungu, na leo hii nimeletwa hapa nikiwa nimefungwa minyororo." Kisha Muawiya aliamuru wauwawe, na wakauawa Hujri na jamaa zake hapo Maraju Adhrau, na hiyo ilikuwa mwaka 51 A.H.

Hindu binti ya Zaid bin Mukhrimah al-Ansariyyah also-ma beti hizi pindi alipopelekwa Hujri kwa Muawiya: *Inuka ewe mbalamwezi yenye kutoa nuru uone je unamuona Hujri akitembea. Anakwenda kwa Muawiya bin Harbi ili akamuuwe kama alivyodai Amiri. Wamejikweza majabari baada ya Hujri na wamefurahikia meza ya Mfalme na baraza lake. Mji ume-kuwa mkauu kwake kana kwamba haujahuishwa na mawingu yenye mvua. Fahamu ewe Hujri, Hujri wa Bani Adiy utapokewa na salama na furaha. Nakhofia kuwa sintapata Adiy wala mzee mwenye kumlilia ndani ya Damascus. Anaona ni haki yake ku-wauwa watu bora kutokana na waziri muovu katika ummah*

wake. Na hata akifa, kwani kila kiongozi wa kundi atakufa na kutoweka duniani."

Ibn Abdul-Barri amepokea kwa sanadi yake kutoka kwa Nafiu, amesema: "Ibn Umar alikuwa sokoni pindi zilipomfikia habari za kuuwawa Hujri, aliachia kiremba chake na akasimama huku akiwa kazidiwa na kilio." Al-Hakim amepokea maelezo kama hayo ndani ya *al-Mustadrak*.⁴²

Na ili msomaji ayajue yale aliyyatenda Abu Yazidi ikiwa ni pamoja na kuua watu wasio na hatia na kumwaga damu ovyo za wasio na hatia khususan wafuasi wa Ahlul-Baiti (as), tunakuletea hapa barua ya Abu Shuhadai Husain bin Ali (as) kwenda kwa Muawiya:

"Ama baad, imenifikia barua yako ukitaja humo kuwa yamekufikia mambo kadhaa kutoka kwangu, mambo ambayo hukutarajia mimi kuhusika nayo, na hakika hakuna anayengoza na kuelekeza kwenye mazuri isipokuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Ama yale uliyotaja kuwa yamekufikia kutoka kwangu hakika hayo yamefikishwa na wazandiki, wachonganishi wenye kufarakisha jamii. Wameongopa wapotovu wachupa mipaka, sijakusudia vita wala kuleta mpasuko, na hakika mimi nakhofia kuwa Mwenyezi Mungu hatoacha kushuhudia hayo (vita na kuleta mpasuko) kutoka kwako na kutoka kwenye kundi lako la wachupa mipaka, kundi la madhalimu na wasaidizi wa Shetani maluuni.

"Si ni wewe ndiye uliyemuwa Hujri na jamaa zake wafanya ibada wanyenyeketu ambao walikuwa wakiikana bidaa, wakiamrisha mema na kukataza maovu? Uliwaua kwa kuwadhulumu na kwa uadui baada ya kuwa umewapa ahadi

⁴² *Tabaqat Ibn Saad*: 4 / 94. *al-Akhbar Tuwal*: 223. *al-Istiab*: 2 / 420, namba 599.
Tuarikh Damashqi: 16 / 67, namba 1880.

nzito na kuwahakikishia usalama, ili kuonesha kiburi kwa Mwenyezi Mungu na kudharau ahadi yake.

“Si ni wewe ndiye uliyemuwa Amru bin al-Hamqu ambaye ibada ilichakaza uso wake? Ulimuua baada ya kuwa umempa ahadi ambazo lau jiwe lingezihamu basi lingeporomoka kutoka kwenye kilele cha mlima.

“Si ni wewe ndiye uliyemhalisha Ziyad katika Uislamu, ukadai kuwa yeye ni mtoto wa Abu Sufiyan, wakati Mtume wa Mwenyezi Mungu alishahukumu kuwa: ‘Mtoto ni wa kitanda na mzinifu lake ni jiwe!’ Kisha ukampa mamlaka juu ya Waislamu, anawauwa, anawakata mikono yao na miguu yao kwa kupishana, na anawasulubu kwenye mashina ya mitende. Subhanallah! Ewe Muawiya hakika ni kana kwamba wewe si mmoja kati ya watu wa ummah huu na wao si jamaa zako.

“Si ni wewe ndiye uliyemuwa al-Hadhramiy ambaye Ziyad alikuandikia barua kuwa yeye ni katika wafuasi wa Ali Mungu autukuze uso wake, wakati dini ya Ali ndio dini ya binamu yake (saww) ambaye amekufanya wewe ukae hapo ulipo, kwani bila yeye heshima bora kabisa ambayo mngekuwa nayo wewe na wahenga wako ni tabu za safari za siku za baridi na siku za joto. Lakini Mwenyezi Mungu akawaondoleeni tabu hizo kuititia sisi kwa neema zake juu yenu. Na kati ya yale uliyosema (katika barua yako) ni: ‘Usiurudishe ummah huu katika fitna.’ Hakika mimi sijui fitna kubwa iliyoupata ummah huu kushinda kitendo cha wewe kuwa kiongozi wake.

“Na kati ya yale uliyosema (katika barua yako) ni: ‘Tizama maslahi ya nafsi yako na dini yako na ya ummah wa Mu-

hammad.' Na hakika mimi sijui kitendo chenye maslahi bora kushinda kitendo cha kukupiga jihadi wewe, kwani kama nitafanya basi ni kwa ajili ya kujikurubisha kwa Mola Wangu, na kama sitafanya basi nitamuomba Mwenyezi Mungu msamaha kwa ajili ya maslahi ya dini yangu na nitamuomba aniwafikishe katika lile alipendalo na kuliridhia. Na kati ya yale uliyosema (katika barua yako) ni: 'Ukinifanyia njama nami nitakufanyia njama.' Nifanyie njama ewe Muawiya kadiri uwezavyo, naapa kwa umri wangu ni tangu zamani watu wema hufanyiwa njama, na hakika mimi nataraji kuwa hazitaidhuru isipokuwa nafsi yako na hazitaporomosha isipokuwa amali zako, nifanyie njama kadiri uwezavyo, na mche Mwenyezi Mungu ewe Muawiya.

"Na tambua kwamba hakika Mwenyezi Mungu ana kitabu ambacho hakiachi dogo wala kubwa isipokuwa huliandika. Na tambua kuwa si watu bali ni wewe ndiye unayehusika na kitendo chako cha kuwaua watu kwa dhana, kuwatesa kwa tuhuma na kumpa kwako utawala mtoto mlevi wa pombe na mcheza na mbwa. Nakuona umeiingiza nafsi yako mwenyewe katika maangamio, umeangamiza dini yako na ume-watelekeza raia. Wasalaam."⁴³

Na mionganini mwa mambo yanayothibitisha kuwa watu walikuwa wamezingirwa na dhuulma ya maliwali wa Muawiya na maafisa wake, ni shairi la Aqibah bin Habirah al-Asadiy, yeye alikwenda kwa Muawiya na kumpa karatasi iliyokuwa imeandikwa beti hizi:

"Twendeni, ummah umepotea, Yazidi ndiye kiongozi wake na pia baba Yazidi. Mmekula ardhi yetu hadi mmeiacha tupu bila kitu, je yupo wa kuisimamia au yupo wa kuivuna? Nashangaa

⁴³ *Tarikhul-Khulafai ar-Rashidin, Dawlat Bani Umaiyyah: 1 / 164 – 165.*

unatamani kuishi milele tutakapokufa na hali si sisi wala wewe atakayeishi milele. Acheni kuusaliti ukhalifa na kuwapa ugavana watu wachafu na watumwa (wa dunia) bali simameni sawa sawa. Tupeni nasi kwa usawa na wala msidanganywe na vikosi vya askari.”⁴⁴

Aisha ambaye aliishi zama za Muawiya na akafariki katika zama zake mwaka 58 A.H. alikuwa akisema: “Mwenyezi Mungu amrehemu Labida aliposema: ‘Wameondoka ambao maisha yalipatikana chini ya usimamizi wao, na katika kizazi wamebakia walafi wasio na manufaa. Hawanufaishi wala hakuna kheri inayotarajiwa kutoka kwao, na hudhalilishwa mwenye kuwaua hata kama hakuchochea fitna.’” Kisha husema: “Ingekuwaje kama angeishi katika zama zetu?”⁴⁵

Tuendelee kidogo na historia ya Bani Umaiyyah, na hebu sasa tusome faslu nyingine kupitia maneno ya baadhi ya wanamageuzi wa mageuzi ya wanafiqhi na makurau, maneno ambayo yanaangazia hali halisi iliyokuwepo katika zama za Abdul-Malik bin Maruwan. Alisema Abdurahman bin Muhammad bin al-Ash'ath bin Qays, kiongozi wa mapinduzi hayo:

“Enyi watu! Hivi hamumuoni katili huyu – yaani al-Hajaj – na anayowatendea watu? Hivi hamghadhibiki kwa ajili ya Mwenyezi Mungu? Hivi hamuoni kuwa Sunna imekufa na hukumu hazina kazi, maovu yanatendwa waziwazi na mauaji ya bila hatia yameenea? Ghadhibikeni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na tokeni pamoja na mimi, si halali kwenu kukaa kimya.”⁴⁶

⁴⁴ *Khazanatul-Adb* cha Abdul-Qadir bin Umar al-Baghdadiy: 2 / 229. Beirut, Darul-Fikri al-Alamiyyah, Chapa ya mwaka 1418 A.H.

⁴⁵ *Khazanatul-Adb* cha Abdul-Qadir bin Umar al-Baghdadiy: 2 / 219. Beirut, Darul-Fikri al-Alamiyyah, Chapa ya mwaka 1418 A.H.

⁴⁶ *al-Akhbar Tuwal* cha Abu Hanifah ad-Daynuriy: 317.

Saad bin Jubair alisema: "...Wauweni kwa kufanya kwao dhulma katika serikali, kwa ukatili wao katika dini, kwa kuwadhalilisha kwao wanyonge na kuua kwao Swala."⁴⁷

Aamir as-Shaabiy alisema: "Ewe Waislamu! Wauweni wala hamtakuwa mmefanya kosa kwa kuwaowa wao, wallahi juu ya ardhi hii siwajui watu wanaoijua vizuri dhulma wala makatili katika serekali kushinda wao."⁴⁸

Ni nzuri sana kauli ya Suyutiy pindi anapomzungumzia Abdul-Malik bin Maruwan, anasema: "Hata kama Abdul-Malik asingekuwa na mabaya isipokuwa al-Hajjaj kwa kumpa kwake utawala juu ya Waislamu na juu ya Masahaba (r.a.), huku akiwanyanyasa na kuwadhalilisha kwa kuwauwa, kuwapiga, kuwatusi na kwa kuwafunga. Achilia watu wengine, aliwaua Masahaba na Tabiina wakubwa wengi wasiohesabika, alifikia hadi kupiga muhuri kwenye shingo ya Anas na Masahaba wengine kwa nia ya kuwadhalilisha. Mwenyezi Mungu asimrehemu wala kumsamehe."⁴⁹

Kisha likaingia balaa kubwa na kuupata ummah wa Kiislamu, pale ummah ulipotawaliwa na Walid bin Yazid bin Abdul-Malik, ambaye ni mfano utolewao katika ufasiki na uovu. Abu Ja'far Tabariy amesema: "Hakika ukosefu wa staha na unywaji wa pombe vilidhihiri kwa Walid bin Yazid, na aliopewa uongozi wa kuongoza Hijja na Hisham mwaka 119 A.H, alibeba hema alilotengeneza kwa ukubwa ulio sawa na Kaaba ili akaliweke juu ya Kaaba, na akabeba pia pombe. Alipotaka kuweka hema lake juu ya Kaaba na kukaa hapo masahaba zake walimkhofisha na kumwambia: 'Hutasilimika

⁴⁷ *Taarikh Tabari*: 7 / 255.

⁴⁸ *Taarikh Tabari*: 7 / 254.

⁴⁹ *Taariikhul-Khulafai*: 262, Darul-Jayli, Chapa ya mwaka 1408 A.H.

wewe pamoja na sisi.' Hivyo akaacha, na ilionekana waziwazi kwa watu kuwa ni mwenye kudharau dini na kutokuijali. Walidi alipindukia katika ulevi na starehe."

Kisha akataja sababu za kuuawa kwake, akasema: "Tayari tumeshataja baadhi ya mambo ya Walid bin Yazidi ikiwemo uovu wake na ukosefu wa staha, pamoja na kudharau kwake na kutokujali kwake dini kabla ya ukhalifa wake. Na alipope-wa ukhalifa na kuutawala hakuna kilichozidi katika hali ya upuuzi, starehe, uwindaji, unywaji wa pombe na kuandama-na na mafasiki isipokuwa kifo."⁵⁰

Ibn al-Athir anasema: "Na mionganini mwa mambo mashuhuri kutoka kwake ni kuwa alipofunua msahafu il-itokea Aya: "**Na wakaomba ushindi, na akashindwa kila jabari mkaidi.**" (**Sura Ibrahim: 15**), akautupa na kuanza kuuchoma mikuki, huku akisoma beti hizi: *'Unanitishia kwa ujabari na ukaidi, basi fahamu mimi ndiye huyo jabari mkaidi. Na siku utakapofika kwa Mola wako katika siku ya mkusanyiko, mwambie: Ewe Mola Walidi amenichanachana.'*"⁵¹

Al-Muafiy bin Zakaria al-Jaririy (305 – 390 A.H.) amekusanya sehemu fulani ya habari za Walid ikiwemo ushairi wake uliokusanya uovu alioutenda, ulahidi wake kuhusu Qur'ani na ukafiri wake wa kumkufuru Mwenyezi Mungu.⁵²

Maisha ya Waislamu yalikuwa yamejaa mabalaa hayo katika zama za Bani Umaiyyah mpaka utawala wao ulipoanguka katika mwaka 132 A.H, na watu wakajibashiria kheri kwa kuja Bani Abbas, lakini walipokamata tu hatamu za ukhalifa na ufalme wao kutulia, walianza kufuata nyayo za Bani

⁵⁰ *Taariikh Tabari*: 8/ 82 – 83, na 106.

⁵¹ *Al-Kamil Fiit-Tarikh*: 5 / 290.

⁵² *Taariikhul-Khulafai* cha Suyuti: 301.

Umaiyyah katika dhulma na ukatili na uharibifu, na waka-zama katika kuwakandamiza Waislamu kwa jumla, Waarabu na Alawiya⁵³ kwa njia makhpususi, mpaka malenga mmoja akasema: “*Na tamani dhulma ya watoto wa Maruwani ingedumu kwetu. Na natamani uadilifu wa Bani Abbas ungefikia motoni.*”

Pia malenga mahiri Abu Faras al-Hamdaniy aliyefariki mwaka 357 A.H. amesema mengi katika kaswida ndefu ambayo anaelezea dhulma iliyokipata kizazi cha Ali (as), anase-ma:

“*Hata kama maovu ya watoto wa Harbi (Abu Sufiyan bin Harbi) yalikuwa makubwa lakini yale yaliyoipata jamii kutoka kwao ni chini kuliko yale yaliyoipata kutoka kenu. Ni mambo mangapi katika dini mmeyasaliti waziwazi, na ni damu nydingi kiasi gani ya Mtume wa Mwenyezi Mungu ipo kwenu. Hivi nyinyi ni wenyе kuridhika na haya mnayoyaona na hali katika kucha zenu kuna damu ya watoto wake (Mtume) watakasifu. Wakajihalalishia kumuua Ridha (as) baada ya kumpa kiapo cha utii, hivyo katika baadhi ya siku waliona uongofu wao kisha wakapofuka.*”

Na ufuatao ni muhtasari wa wasifu wa baadhi ya Makhalifa wa Bani Abbas, Suyutiy katika kumzungumzia Abu Ja'far al-Mansuri anasema: “Aliwaa viumbe wengi mpaka ukaimarika ufalme wake, naye ndiye aliyempiga viboko Abu Hanifa (r.a.) kisha akamfunga, akafariki baada ya siku kadhaa. Na inasemekana: Hakika ye ye ali muua kwa sumu kwa sababu alitoa fatwa ya kutoka dhidi yake.”

⁵³ Alawiya ni kizazi chote cha Ali bin Abu Talib (as).

Kisha akasema: "Ni katika mwaka mia moja na arubaini na tano ndipo walipotoka ndugu wawili Muhammad na Ibrahim watoto wa Abdullah bin Hasan bin al-Hasan bin Ali bin Abutalib (as) dhidi ya al-Mansuri, lakini aliwashinda na akawaua wao pamoja na kundi kubwa la watu wa nyumba ya Mtume. Hakika sisi sote ni milki ya Mwenyezi Mungu na hakika sisi ni wenye kurejea kwake.

"al-Mansuri ndiye mtu wa kwanza aliyeingiza fitna baina ya Bani Abbas na Maalawiya, hapo kabla walikuwa kitu kimoja. Al-Mansuri aliwatesa baadhi ya ulamaa mionganini mwa wale waliotoka pamoja nao (Muhammad na Ibrahim) au aliyeamuru kutoka dhidi yake, aliwaua na kuwapiga na kuwatendea mengineyo. Mionganini mwa ulamaa hao ni Abu Hanifa, Abdul-Hamidi bin Ja'far na Ibn Ajlani. Na mionganini mwa waliotoa fatwa ya kuruhusu kutoka pamoja na Muhammad dhidi ya al-Mansuri ni Malik bin Anas (r.a.), alipoambiwa: 'Hakika katika shingo zetu kuna kiapo cha utii juu ya al-Mansuri.' Alisema: 'Hakika mlimpa kiapo cha utii kwa kulazimishwa, na mwenye kulazimishwa hana kiapo.'"⁵⁴

Al-Mansuri alitoa hifadhi kwa Muhammad bin Abdullah katika barua aliyomwandikia alipopata habari za kuishika kwake Madina, Muhammad bin Abdullah akamjibu kwa kusema: "Ni hifadhi ipi unayonipa! Ni hifadhi ya Ibn Habirah, au ni hifadhi ya ami yako Abdullah bin Ali, au ni hifadhi ya Abi Muslim?"⁵⁵

Hebu tuangalie moja kati ya visa vyta hifadhi hizi tatu: Yazid bin Umar bin Habirah alikuwa ameweuka ngome huko Wasita baada ya kuwamaliza Bani Umaiyyah, ndipo Abbas

⁵⁴ *Taarikhul-Khulafai* cha Suyutiy: 315 na 317.

⁵⁵ *Taarikh Tabari*: 8 / 483.

akampeleka ndugu yake al-Mansuri kwenda kumpiga vita, al-Mansuru alibakia Wasita muda mrefu akipigana naye mpaka akachoka, ndipo akamwandikia barua akimpa hifadhi na kutaka sulhu na akasaini barua yake, ndipo Ibn Habirah akardhia na kutii, lakini muuaji huyu alikiuka ahadi yake kwake na akamtumia mtu aliye wenda kumuuwia ndani ya ikulu ya Wasita.⁵⁶

Na mionganoni mwa maelezo yaliyokuwemo katika tamko la hifadhi ni: "Hakika mimi nimekupa hifadhi kwa hifadhi ya Mwenyezi Mungu ambaye hapana mungu isipokuwa Yeye.... hifadhi ya kweli isiyo na hadaa yoyote, isiyochanganyika na batili dhidi ya nafsi zenu, vizazi vyenu na mali zenu. Na nimempa Yazid bin Umar bin Habirah na yule niliyempa hifadhi mwanzoni mwa barua yangu hii kuwa nitatekeleza niliyowaahidi, ambayo ni ahadi ya Mwenyezi Mungu na makubaliano yake....ni dhima ya Mwenyezi Mungu, ni dhima ya Muhammad na ya Makhalifa wake wema waliotangulia... na hakika kama Abdullah bin Muhammad (yaani al-Mansuri) atakwenda kinyume na ahadi aliyokupeni katika hifadhi yenu hii, akawa amevunja ahadi au kuwahadaa... basi Mwenyezi Mungu asipokee fidia yoyote wala badala kutoka kwake....na yeye atajitenga na Amirul-Muuminina na atajivua utiifu wake kwake, na ni juu yake kuhiji Hijja thelathini, kwa kwenda katika Nyumba tukufu ya Mwenyezi Mungu iliyopo Makka kwa mguu peku peku, kutokea sehemu alipo sasa ya mji wa Wasita..."

Dkt. Muhammad Mahir Hamadah anasema: "Lakini haziku heshimiwa dhamana zote hizi na wala hazikuwa na thamani yoyote kwa jamaa hawa na wala hazikumfaa chochote

⁵⁶ *Wafayatul-Aayan*: 6/ 313, namba 818. al-Aalam: 8 / 185.

Ibn Habirah na wala hazikulinda uhai wake. Hiyo ni kwa kuwa jamaa hawa waliokunywa kilevi cha kuwatetea Bani Umaiyyah hawakuacha kutokujali mambo kama haya, na wakaitakidi kuwa wana haki ya kuvunja ahadi na kutotimiza ahadi, jambo ambalo linaonesha jinsi walivyokuwa duni ki-maadili bali hata upande wa dini, kwani kuvunja ahadi ni kukhalifu maamrisho ya Mwenyezi Mungu na mafunzo ya Uislamu.⁵⁷

Pia katika maelezo yake kuhusu kitendo cha Haruna ar-Rashid kuacha urithi wa utawala kwa watoto wake watatu: Amin, kisha Maamun na kisha Qasim, na kupeleka hati hizo za utawala huko Makka na kuzitundika katika Kaaba tukufu ili aweze kuzipa rangi ya kidini katika macho ya watu na kuzipaka rangi ya utukufu, anasema: “ar-Rashid alichukua msimamo mkali na mzito juu ya maamuzi yote ikiwemo ahadi na mikataba, lakini ni lini ahadi na mikataba iliheshimiwa katika dola ya Bani Abbas hadi Amin naye aweze kuiheshimu? Hivyo Amin alipokaribia tu kuwa Khalifa alianza kujaribu kuvunja ahadi, jambo ambalo lilimfanya aingie katika ugomvi na ndugu yake na hatimaye akakosa utawala na uhai wake.”⁵⁸

Ama siasa ya ugandamizaji ambayo ilifuatwa na al-Mutawakil al-Abbasiy, ikiwemo vitendo vya uuwaji alivyofan-ya dhidi ya Waislamu khususan dhidi ya kizazi cha Abutalib, huku akienda kwenye mabaraza ya upuuzi na unywaji pombe, hayo ni maneno marefu hivyo kwa muhtasari tutosheke na baadhi tu ya habari zilizopatikana kuhusu hayo. Abul-Faraj al-Asfahaniy aliyefariki mwaka 356 A.H. anasema:

⁵⁷ *Dirasat Wathiqat Liltarikhil-Islamiy Wamaswadirihu*: 96, Bairuti, Chapa ya mwaka 1408 A.H. ya Muasasatur-Risalah.

⁵⁸ *Dirasat Wathiqat Liltarikhil-Islamiy Wamaswadirihu*: 116 na 118, Bairuti, Chapa ya mwaka 1408 A.H. ya Muasasatur-Risalah.

“al-Mutawakil alikuwa katili sana katika ukandamizaji dhidi ya kizazi cha Abutalib, mkali dhidi yao, mwenye chuki na hikdi dhidi yao, na mwenye dhana mbaya na tuhuma dhidi yao. Na ilitokea kwamba hata Waziri wake Abdullah bin Yahya bin Khaqan naye alikuwa kama yeye kwa kuwa na mtazamo mbaya dhidi yao, hivyo akaona ni zuri kila baya alilokuwa akiwatendea katika muamala wao, kiasi kwamba aliwatendea ubaya katika kiwango ambacho hakuna Khalifa ye yote wa Bani Abbasi wa kabla yake aliyeweza kufikia kiwango hicho. Miongoni mwa hayo ni kuwa alivunja kaburi la Husain na kuodoa athari zake, na akaweka askari wake katika njia zenyenye kuelekea huko, hivyo hakuna aliyepatikana akienda kulizuru isipokuwa alikamatwa na kupelekwa kwake, naye alimuua au kumtesa kwa adhabu.”⁵⁹

Ad-Dhahbiy anapozungumzia hatima yake mbaya iliyomfika anasema: “Na wameafkiana kuwa Waturuki walijitenga na al-Mutawakil kwa kuwa alikuwa mzuijaji wa mambo, muovu na dhalimu, na hivyo ndivyo mambo yalivyokwenda hivyo Waturuki wakaafkiana pamoja na al-Muntasir juu ya kumuua baba yake, watu watano wakamvamia usiku akiwa katika baraza la upuzi wake ikiwa ni mwezi tano Shawal mwaka wa arubaini na saba, wakamuua. Al-Mutawakil alikuwa amepindukia katika starehe na ulevi...japo haijasihu kuwa alikuwa na chuki na Ahlul-Baiti (nasbi).”

Hivyo ndivyo alivyosema ndani ya kitabu *Taarikhul-Islam*⁶⁰, isipokuwa ni kwamba alisahihisha rai yake kuhusu kutokuwa kwake na uadui na Ahlul-Baiti, akasema katika kitabu *Sirat Aalamin-Nubalai*: “Katika mwaka wa (mia mbili) thelathini

⁵⁹ *Maqatilut-Tuvalibina*: 597, kutaja siku za al-Mutawakil.

⁶⁰ *Taarikhul-Islami*: 199 (241 – 250).

na sita al-Mutawakil alibomoa kaburi la Husein (a.s.), al-Basamiy akasoma beti kadhaa zikiwemo: ‘Walisisikitika kwa nini hawakushiriki kumuua (Husein), hivyo wakamfuata baada ya kuwa udongo.’ Na al-Mutawakil alikuwa na chuki dhidi ya Ahlul-Baiti na muovu.”⁶¹

Suyutiy anasema: “Ni katika mwaka wa arubaini na nne ndipo al-Mutawakil alipomuua Ya’qub bin Sikit bingwa wa Kiarabu, hakika yeye alimpa kazi ya kuwafundisha watoto wake na ndipo siku moja al-Mutawakil aliwatazama watoto wake al-Muutaz na al-Muayad, akasema kumwambia Ibn Sikit: ‘Ni akina nani uwapendao sana ni wao wawili au Hasan na Husein?’ Ibn Sikit akasema: ‘Qanbar – mtumishi wa Ali – ni bora kushinda wao wawili (yaani kushinda watoto wa al-Mutawakil: al-Muutaz na al-Muayad).’ Akawaamuru Waturuki wakalikanya kanyaga tumbo lake mpaka akafariki. Na inasemekana kuwa aliamuru ulimi wake ung’olewe akiwa hai hadi akafariki, na akamtumia mwanawe fidia yake.”⁶²

Msomaji pia anaweza kusoma yale yaliyoandikwa na wanahistoria mfano wa Tabari, al-Mas’udiy na Abul-Faraj al-Asfahaniy ili kuona dhalma na ukandamizaji uliofanywa katika karne mbili, ya pili na ya tatu, ambazo imesemekana kuwa ndio karne bora baada ya karne ya kwanza, na ataona ni jinsi gani uharibifu, uovu na ukali ulivyoenea katika miji ya Kiislamu katika muda wa kipindi hicho, na mazingira ya kisiasa na kijamii yakaendelea kuwa mabaya zaidi na kuharibika muda baada ya muda mpaka majeshi ya Kitatar al-Barbariyyah yalipovamia miji ya Kiislamu na kuanza kuiteka mmoja baada ya mwingine, kisha yakaivamia Baghdad huku

⁶¹ *Siratu Aalamun-Nubalai*: 12/ 35, Wasifu wa 7.

⁶² *Tuarikhul-Khulafai*: 409.

watawala wakiwa wamezama katika upuuizi na starehe zao, yakauteka mwaka 656 A.H, na kuumaliza ukhalifa wa Bani Abbas.

Na hapa inafaa kukuletea maelezo aliyoandika Ibn Kathir kuhusu hilo: "Majeshi ya Kitatar yakaizunguka Ikulu ya Khalifa huku yakiishambulia kwa mishale kutoka kila upande mpaka ikampata kijakazi mmoja aliyekuwa akicheza mbele ya Khalifa na akimliwaza, naye alikuwa mionganini mwa vijakazi waliokuwa na hadhi kubwa kwake na alikuwa ni mkunga, jina lake aliitwa Arafa, alipatwa na mshale kutokea dirishani, ukamuua huku akiwa anacheza mbele ya Khalifa, akaudhika Khalifa kutokana na hali hiyo na akaingiwa na khofu kubwa, ulipoletwa mshale uliompata kijakazi yule aliukuta umeandikwa: 'Mwenyezi Mungu atakapokupitisha majaliwa yake na makadara yake huwapokonya akili zao wale wenye akili.' Hapo Khalifa akaamuru ulinzi uongezwe na sitara zikithirishwe katika Ikulu yake. Ni mwezi kumi na mbili ya Muharamu katika mwaka huu ndipo Hulagu Khan alipovamia Baghdad na majeshi yake."⁶³

Ikiwa hii ndio hali ya Khalifa wa Waislamu na ndio hali ya wanaomzunguka, itakuwaje hali ya askari wake na maafisa wake? Ikiwa mwenye nyumba ni mpiga dufu basi tabia ya watu wote wa nyumba hiyo ni kucheza.

Baada ya kuwasilisha muhtasari huu kuhusu hali iliyokuwepo zama za Watangulizi, kuna maswali hujitokeza ambayo yanahitaji majibu yake kutoka kwa Masalafi.

⁶³ *Al-Bidayah Wan-Nihayah*: 13 / 212.

MASWALI AMBAYO YANAHITAJI MAJIBU KUTOKA KWA MASALAFI

SWALI LA KWANZA: Kujisahaulisha Ahlul-Bait (as):

Tkiwa watu wa karne tatu ndio rejea katika Theolojia na Sharia na tafsiri ya Kitabu kitukufu (Qur'ani), basi ni kwa nini Masalafi wa leo wamewapa mgongo Maimamu wa Ahlul-Bait (a.s.), ambao waliishi baina ya Waislamu katika kipindi hicho mpaka mwaka 260 A.H., wakati alipoghibu Imam wa kumi na mbili (a.s.) kwa amri kutoka kwa Mwenyezi Mungu, kama alivyoghibu Masihi (a.s.) katika zama zake.

Jamaa hawa hawarejei kwa Maimamu wa Ahlul-Bait (as), si katika Fiqhi wala si katika riwaya, isipokuwa sehemu chache, licha ya kwamba ulamaa wao wakubwa wanashuhudia uchamungu wao (Maimamu wa Ahlul-Bait (a.s.)) na upana wa elimu yao, wakati ambao wao (Masalafi wa sasa) wanarejea kwa watu ambao huwezi kuwalinganisha na Maimamu wa Ahlul-Bait (a.s.), bali ni kwamba wanarejea hadi kwa watu waovu mionganoni mwao. Ni kana kwamba Mwenyezi Mungu hakufaradhisha kuwapenda Ahlul-Bait (a.s.) katika Kitabu Chake kwa kusema:

قُلْ لَا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ أَجْرًا إِلَّا الْمَوَدَّةُ فِي الْقُرْبَىٰ

“Sema: Kwa haya siwaombi malipo yoyote kwenu isipokuwa mapenzi katika ndugu (Ahlul Bait a.s.).” (Sura Ash-Shura 42 : 23).

Na ni kana kwamba hajausia kushikamana nao na kurejea kwao pindi alipowalinganisha na Kitabu Kitukufu katika hadithi ya vizito viwili, hadithi ambayo Waislamu wote wameafikiana juu ya usahihii wake, pale Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) aliposema: "Ni kana kwamba nimeitwa na ni lazima nitaitikia, hakika mimi ni mwenye kuwaachieni vizito viwili: Kitabu cha Mwenyezi Mungu kamba itokayo mbinguni hadi aridhini, na kizazi changu watu wa nyumba yangu. Na hakika hivyo viwili havitaachana mpaka vitakaponikuta katika Hodhi, hivyo tazameni ni jinsi gani mtaishi navyo baada yangu."⁶⁴

⁶⁴ Ameipokea Tabari ndani ya Kitabu *al-Kabir*, na Abu Ya'la ndani ya Musnad yake kutoka kwa Abu Said al-Khidriy, kama pia ilivyo ndani ya *Kanzul-Ummal* Juz. 1, Uk. 178, Hadithi ya 952. hadithi hii ya vizito viwili imeandikwa na watu zaidi ya mmoja, ukiacha hao tuliovataja, mionganoni mwao ni: Ahmad bin Hanbal, Tirmidhiy, an-Nasaiy, Said bin Mansuri, Ibn Saad, al-Hakim, Ibn Abi Shaybah, Abdu bin Humaydu, Ibn al-Anbariy, al-Barudiy, na al-Khatib al-Baghdadiy. Tazama *Kanzul-Ummal*, Juz. 1, uk. 172 – 173, Hadithi ya 780 – 873, na katika uk. 185 – 187, Hadithi ya 943 – 947, na Hadithi ya 949 – 954.

SWALI LA PILI: KUHUSU KAULI YA SAHABA KUWA HOJA

Hakika Masalafi wanafuata Sunna zilizopokewa kutoka kwa Makhalifa na kuzisifu kuwa ni Sunna za Abu Bakr, Sunna za Umar na Sunna za Uthman, na kuna wakati wanapanua zaidi wigo kwa kufuata Sunna ya kila Sahaba, licha ya kwamba Mwenyezi Mungu alikamilisha dini yake na kufunga mlango wa unabii na utume, sasa inakuwaje kauli binafsi ya Sahaba mwenyewe ambayo haitoki kwa Mtume iwe ni hoja kisharia?

Shawkaniy anasema: "Hakika kauli ya Sahaba si hoja ya kisharia, kwani hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu hakuleta katika ummah huu Nabii isipokuwa Nabii wetu Muhammad (saww), na hatuna isipokuwa Mtume mmoja, na Masahaba na wale waliokuja baada yao wote wako sawa katika ulazima wa kufuata Sharia yake, Kitabu na Sunna. Hivyo ikiwa mtu atasema kuwa hoja ya kisharia katika dini ya Mwenyezi Mungu husimama bila haya (Kitabu na Sunna ya Mtume) basi mtu huyo atakuwa amesema katika dini ya Mwenyezi Mungu yale ambayo hayawezi kuthibiti, na atakuwa amethibiti-sha sharia ambayo hajaamrisha Mwenyezi Mungu."⁶⁵

Ibn Zahrah anasema: "Ukweli ni kwamba maneno ya Shawkaniy yanaafikiana na Qur'ani Tukufu na kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu:

⁶⁵ Irshadul-Fuhul cha Shawkaniy: 214.

أَمْ لَهُمْ شُرَكَاءُ شَرَّعُوا لَهُمْ مِنَ الدِّينِ مَا لَمْ يَأْذَنْ بِهِ اللَّهُ

“Au wana washirika waliowawekea dini asiyoitolea idhini Mwenyezi Mungu?” (Sura Ash-Shura 42 : 21). Na kauli yake:

اَتَخَذُوا اَحْبَارَهُمْ وَرُهْبَانَهُمْ اُرْبَابًا مِنْ دُونِ اللَّهِ

“Wamefanya makuhani wao na watawa wao kuwa ni miungu badala ya Mwenyezi Mungu.” (Sura At-Tawba 9 : 31). Na kauli yake:

وَلَا تَقُولُوا لِمَا تَصِفُ الْسَّنَثُكُمُ الْكَذِبَ هَذَا حَلَالٌ وَهَذَا حَرَامٌ

“Wala msiseme uwongo, kwa kuropokwa na ndimi zenu: Hiki ni halali na hiki ni haramu.” (Sura An-Nahl 16 : 116). Na kauli yake:

وَلَا تَقُولُ مَا لَيْسَ لَكَ بِهِ عِلْمٌ

“Wala usifuatilie ambalo huna ujuzi nalo.”
(Sura Bani-Israel 17 : 36). ”

SWALI LA TATU: JE SHARTI LAO WANAPOSEMA

'Watangulizi wema' ni sharti la kufafanua au ni la kuzuia?

Kwanza: Haliwezi kufuatwa, kwani imeshatangulia huko Nyuma kuwa Bani Umaiyyah na Bani Abbas na watetezi wao waliitapakaza ardhi damu za watu watakatifu wasio na hatia, hivyo itawezekana vipi kuwajumuisha Watangulizi wote kuwa ni wema? Hivyo hakuna njia ya sharti hili 'wema' kuwa ni la kuzuia. Na hivyo kumaizi baina ya mwema na muovu ni jambo gumu, kwa sababu wengi mionganoni mwa wanafiki na madhalimu walikuwa wamejiingiza ndani ya kundi la watu wema. Na bahati mbaya zaidi ni kuwa ulamaa wa fani ya kuelezea mapungufu na makamilifu ya wapokezi wa hadithi hawajawajumuisha Masahaba katika maelezo yao, bali wamewapokea wote kwa kuwazingatia kuwa ni waadilifu wenye kutegemewa, na kwa ajili hiyo wakachanganyikana wema na waovu.

UTETEZI WA AJABU

Umeshajua kuwa hatuwezi kuwasifu kwa wema Watangulizi wote, hiyo ni kutokana na vitendo vyao ambavyo baadhi tayari umeshavijua, ambavyo havioani na uadilifu na usawa, bali hata na imani na Uislamu. Isipokuwa ni kwamba baadhi ya Masalafi wenye msimamo mkali pindi wanapoona mabaya yasiyokubalika ambayo yamejaa ndani ya wasifu wa maisha ya baadhi ya Watangulizi hujaribu kuwatetea kwa kusema: "Hakika Mwenyezi Mungu ametoharisha panga zetu kupitia damu zao, hivyo nasi tutoharishe ndimi zetu kwa kuacha kutaja mabaya yao." Utetezi huu ni sawa na mfano halisi wa methali maarufu isemayo: "Utetezi ni mbaya kuliko kitendo." Hiyo ni kwa kuwa:

Kwanza: Maana ya utetezi huo ni kuwa ugomvi uliyotokea baina ya Ali na wapinzani wake ulikuwa ni fitna iliyofunika haki, na mtu hana uwezo wa kuiona nuru yake ili awe katika ubainifu wa jambo lao, hivyo aache kuzungumzia yale yaliyotokea baina ya pande mbili za ugomvi, na wala asihukumu chochote juu yao.

Haya ndio maneno yao mbele ya yale yaliyotokea baina ya Ali na wapinzani wake. Ama kauli yao kuhusu Makhalifa wengine (hata wale walizoutawala ummah huu kwa nguvu ya upanga, kama asemavyo Hasan al-Basriy) inatofautiana kabisa na ile wasemayo kuhusu Ali, katika hilo wana haki ya kutamka bayana ubaya wa wagomvi wao. Ni kana kwamba vumbi la vita vya Jamal na Suffin, na vumbi la tofauti iliyozushwa baina ya Ali na wapinzani wake lilifunika nyuso za watu wote, hivyo wakawa hawawezi kumaizi mambo baina

yao, lakini vumbi hilo baadaye likaondoka kwenye nyuso za wapinganaji katika zama za Makhalfa wengine, na hivyo wakamtambua ni nani mwenye haki na ni nani aliye katika batili, na ni nani mtengenezaji na ni nani mharibifu.

Hakika muumini mtambuzi wa mambo, ambaye yuko huru dhidi ya utumwa wa kuiga na kuwaabudu watu, hayajifichi mambo mbele yake katika mazingira mbalimbali, naye huyatambua mambo kwa yakini kama mwanga wa juu, la sivyo basi ni kama alivyosema mshairi: "Itakuwa na faida gani dunia kwa ndugu yangu pindi anapoitizama, ikiwa nuru na giza kwake yeye vyote viko sawa?" hakika muumini mtambuzi wa mambo pindi anapotaka kuamiliana na watu huhukumu mambo kwa vigezo vya Uislamu vilivyo thabiti na bayana, na huwapima watu kwa uadilifu, na wala hahukumu kwa vigezo vya kijamii vya kimakosa, ambavyo hujumuisha cheo, utajiri, mamlaka, ubinafsi na mengineyo mionganoni mwa vigezo visivyo na maana.

Ikiwa kurejea tu katika vigezo hivi peke yake kunatosha kuwatambua wale wenye kupita katika njia ya haki dhidi ya wale walio nje ya njia ya haki, je itakuwaje kama maelezo ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) yatatuongoza katika haki ya Ali (as) na katika matukio ambayo atakabiliana nayo? Bila shaka sura itakuwa bayana zaidi, wazi zaidi na dhahiri zaidi, isiyo na vumbi wala giza wala kivuli.

Yafuatayo ni baadhi ya maelezo hayo: al-Hakim amepokea kwa njia yake kutoka kwa Abudhari al-Ghafariy kuwa aliseema: Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alisema: "Yeyote atakayenitii mimi atakuwa amemtii Mwenyezi Mungu, na yeyote atakayeniasi mimi atakuwa amemuasi Mwenyezi Mungu, na yeyote atakayemtii Ali atakuwa amenitii mimi

na yejote atakayemuasi Ali atakuwa ameniasi mimi." Al-Hakim amesema hadithi hii ni sahihi kwa mujibu wa sharti za masheikh wawili Bukhari na Muslim, na Dhahbiy amem-wafiki katika hilo.⁶⁶

Nasema: Miiongoni mwa mifano halisi ya kumtii Ali (as) ni kutekeleza amri yake katika hali ya amani na isiyo ya amani, na kwa mujibu wa hadithi iliyotajwa hapo nyuma, inakuwa kupigana mbele yake (as) ni kumtii Mtukufu Mtume (saww) na ni kumtii Mwenyezi Mungu. Hivyo ilikuwa ni wajibu juu ya hawa kusoma dua hii: "Tunatamani kuwa tungekuwa pamoja na Ali na askari wake ili tufuzu kufuzu kukubwa." Kwani walipitwa na neema ya kumtetea na kusimama katika safu yake. Hiyo ni badala ya kuchukulia kuwa kutokushiriki kwao katika damu hizo ni neema ya Mwenyezi Mungu juu yao, na pia waziache ndimi zao huru katika kuwataja wali-omuasi Mwenyezi Mungu na Mtume, na waweke wazi misimamo yao dhidi ya Ali mpaka asiyeijua haki aijue, hivyo amtii yule atakayemuongoza na ajiepushe na yule atakayempoteza. Hiyo ni badala ya kuzuia ndimi zao zisiweze kuwataja, na hatimaye wakawa mashetani bubu kwa kuikalia kwao kimya haki.

Ibn Haban amepokea ndani ya Sahih yake kwa njia yake itokayo kwa Abu Said al-Khidriy kuwa alisema: "Nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akisema: 'Hakika miiongoni mwenu yupo atakayepigania tafsiri ya Qur'ani kama nilivyopigania kuteremka kwake.' Abu Bakr akasema: 'Ni mimi mtu huyo ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu?' Akasema: 'Hapana.' Umar akasema: 'Ni mimi mtu huyo ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu?' Akasema: 'Hapana, lakini ni mshona

⁶⁶ *Al-Mustadrak Alas-Sahihayn*: 3 / 121.

kiatu.' Wakati huo alikuwa ameshampa Ali kiatu chake, naye akikishona."⁶⁷

Imepokewa kutoka kwa Ali kuwa alisema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) aliniahidi kuwa nitawauwa watengua kiapo, wachupa mipaka na waaasi." Na katika riwaya nyininge: "Aliniamuru kuwauwa watengua kiapo, wachupa mipaka na waaasi."

Al-Haythamiy anasema: "Ameipokea al-Bazar na Tabaraniy katika al-Awsat, na njia moja kati ya njia za al-Bazar wapokezi wake ni watu sahihi isipokuwa Rabiu bin Said. Lakini Ibn Haban kasema ni mtu mwaminifu."⁶⁸

Al-Hakim amepokea kwa njia yake kutoka kwa Hubat al-Uraniy, amesema: "Tuliingia pamoja na baba yangu Mas'ud al-Ansariy kwa Hudhayfah bin al-Yaman ili nimuulize kuhusu fitna, akasema: 'Zungungeni na Kitabu popote kitakapokwenda na tizameni ni kundi lipi yumo mtoto wa Samiyyah basi lifuateni, kwani hakika yeye huzunguka pamoja na Kitabu cha Mwenyezi Mungu popote kiendapo!' Nikamwambia: Ni nani huyo mtoto wa Samiyyah? Akasema: 'Ammar, kwani nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akimwambia: Hautakufa mpaka likuuwe kundi ovu, utakunywa maziwa yaliyochanganyikana na maji, na hayo ndiyo yatakuwa riziki yako ya mwisho duniani.'" Al-Hakima anasema ni hadithi sahihi kwa mujibu wa sharti za Mashekehe wawili (Muslim na Bukhari), na amemuwafiki katika hilo ad-Dhabbiy.⁶⁹

⁶⁷ *Sahih Ibn Haban*: 15/ 385.

⁶⁸ *Maj'mauz-Zawaaid*: 7 / 238.

⁶⁹ *Al-Mustadrakus-Sahihayn*: 3 / 391.

Na mionganini mwa mambo yaliyothibiti kihistoria ni kwamba Ammar alikuwa mionganini mwa wafuasi wakubwa wa Ali na mionganini mwa waandamizi wake, na alimtetea katika kila jambo, na alihudhuria pamoja naye katika vita viwili vya Jamal na Suffiin, na ndipo alipokufa kishahidi katika vita vya pili kwa kuuliwa na panga za kundi ovu lililokuwa likimpiga vita Imam halali kisheria aliyesimikwa na Mtukufu Mtume wa mwisho (saww).

Na hapa tunajiuliza: Baada ya maelezo haya bayana ya Mtukufu Mtume ambayo yanaonesha njia sahihi na kuainisha alama zake na kuongoza katika njia hiyo, ilikuwaje hawa wanaojiita Masalafi wakaridhia kuwa mionganini mwa watu waliopotea wasiojua wapi waelekee, wasiojua ni ipi njia iliyo bayana na ni zippi zenyenye kupoteza?

Na hakika wao kwa kauli yao hii: "Hivyo nasi tutoharishe ndimi zetu kwa kuacha kutaja mabaya yao." Wamezidhulu mu nafsi zao kwa kufuata matamanio yao katika hilo na kwa kuyapa mgongo maelekezo ya Mtume (saww), na wamewad-hulumu pia wafuasi wao wasiojua kitu kwa kuwachanganya na kuwaficha haki.

Jambo la Masalafi halikukomea katika kukhalifu maelezo thabiti ya Mtukufu Mtume (saww) tu, bali wamemkhalifu hata yule wanayejigamba kujinasibisha naye, yaani Ahmad bin Hanbal, kwani hakika Imam Hanbal alikuwa amemjumuisha Ali katika Makhalfi, kuwa ni Khalifa wa nne, na hii inamaanisha kuwa ana haki ya watu kumtii katika aliloamrisha na kukataza, na pia haki ya kuitikia wito wake, sawa na Makhalfi waliomtangulia. Ikiwa hivyo ndivyo, basi ni kwa nini Ali peke yake (kati ya Makhalfi wanne) ndiye

anyang'anywe haki hii? Alinganishwe sawa na wahaini walioasi dhidi ya serikali yake halali, na kisha kisa chake pamoja nao kiwe ni jambo lisilo bayana ambalo ni haramu kulichunguza na kufichua undani wake?!

Al-Qadhi Ibn Abi Ya'la al-Hanbaliy ametaja katika waasifu wa Wurayzah bin Muhammad al-Hamswiy kuwa alisema: "Niliingga kwa Abu Abdullah Ahmad bin Hanbal pindi alipom-jumuisha Ali miongoni mwa Makhalfa na kumfanya Khalifa wa nne, nikamwambia: 'Ewe Abu Abdullah! Hakika kufanya hivi ni kumtia dosari Talha na Zubair' Akasema: 'Ni jambo baya ulilosema, inatuhusu nini sisi vita vya jamaa hawa hata tuvitaje?' Nikamwambia: 'Mwenyezi Mungu akutengenezee mambo yako, hakika nimevitaja pale ulipomfanya Ali Khalifa wa nne, na ukampa haki ya ukhalifa na kila kilichokuwa wajibu kwa Makhalfa wa kabla yake.' Akaniambia: 'Ni lipi linanizuia kufanya hivyo?' Nikamwambia: 'Hadithi ya Ibn Umar'⁷⁰ Akaniambia: 'Umar ni bora kushinda mwanawe, naye aliridhia Ali awe Khalifa wa Waislamu hivyo akamjumuisha katika Shura, na Ali mwenyewe alijiita Amirul-Muuminin, je mimi ndio niseme: Si Amiri wa Waumini?' basi nikaondoka kwake."⁷¹

Hivyo ndivyo yanavyofichuliwa madai ya wanaojiita Masalafi katika kuchukua kauli za Ahmad bin Hanbal na (Al-Qadhi Ibn Abi Ya'la al-Hanbaliy) kujitenga naye pindi al-

⁷⁰ Anakusudia kauli ya Ibn Umar: "Katika zama za Mtukufu Mtume (saww) tulikuwa tunapomchagua mbora basi tunamchagua Abu Bakr, kisha Umar bin Khatab, kisha Uthman bin Affan." Hivyo ndivyo ilivyo ndani ya *Sahih Bukhari*: 2 / 451, Hadithi namba 3655. Ama katika *Musnad Ahmad* Juz. 2, uk. 14: "Wakati Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akiwa angali hai na Sahaba zake wapo, tulikuwa tunapohesabu aliye bora tunamtaja Abu Bakr, Umar na Uthman, kisha tunanyamaza."

⁷¹ *Tabaqat al-Hanabilah*: 1 / 393, namba 510.

ipokhalifu kauli yake. Na inaonekana ni suala la matamanio na chuki binafsi na rai za kufuata waliotangulia, kisha ili ku-ziunga mkono wanaokota kauli dhaifu na habari dhaifu toka huku na kule.

Tatizo hili halikuzalika katika zama za sasa bali mizizi yake inarudi mpaka zamani sana, pale wenye misimamo mikali kati ya wafuasi wa Imam Ahmad walipoamua kuunda fitna na matatizo dhidi ya wafuasi wa madhehebu nyingine za Kisunni na zisizo za Kisunni, na kuuzamisha ummah ndani ya dimbwi la ugomvi na mizozo isiyo na sababu isipokuwa ubishi, chuki binafsi na ujeuri, na haya yafuatayo ni sehemu tu ya mifano:

MSIBA ULIOMPATA TABARI ALIYEFARIKI MWAKA 310 A.H

Muhammad bin Jarir Tabari alikuwa mmoja kati ya maulamaa, ambaye kauli yake hufuatwa, na kutokana na maarifa yake na ubora wake rai yake ilikuwa ikifuatwa, alikuwa amekusanya elimu ambayo hakuna yejote katika watu wa zama zake aliyeweza kulingana naye.⁷²

Na alikuwa mwaminifu, hafidh, kinara katika tafsiri, Imam katika Fiqhi, Ijma'i na Ikhtilafu, mjuzi wa historia na siku za watu, mjuzi wa Qur'an na lugha, na mengineyo.⁷³

Hivyo ndivyo al-Khatib al-Baghdadiy na ad-Dhahbiy walivyomwelezea Abu Ja'far Tabari. Lakini hebu njoo pamoja nami tuone yale yaliyompata aalimu huyu bingwa ikiwa ni pamoja na adha na ukandamizwaji uliyompata kupidia mikono ya Mahanbali wenyewe msimamo mkali, hii ni kwa ushahidi wa Mashafi wawili wakubwa walioishi katika zama zake.

Husaynak bin Ali an-Nisaburiy anasema: "Jambo la kwanza aliloniuliza Ibn Khuzaymah, alisema: 'Je umeandika kutoka kwa Muhammad bin Jarir Tabari?' Nikasema hapana, akasema: 'Kwa nini?' Nikasema: Kwa sababu alikuwa haonekani, na Mahanbali walikuwa wakizuia kuingia kwake. Akasema: 'Ni jambo bayo sana ulilofanya, natamani kwamba usingeandika kutoka kwa yejote kati ya hao ulioandika kutoka kwao, ukasikia tu kutoka kwa Abu Ja'far'"⁷⁴

⁷² *Taarikh Baghdad*: 2/ 163, Wasifu wa 589.

⁷³ *Siyrat Aalamun-Nubala*: 14/ 270, Wasifu wa 175.

⁷⁴ *Taarikh Baghdad*: 2/ 164. *Taarikhul-Islami* (311 – 320 A.H.): uk. 281 – 282.

Abu Bakr bin Baluwayhi anasema: "Nilimsikia Imam wa Maimamu Ibn Khuzaymah akisema: 'Simjui yeyote juu ya ardhi hii mwenye elimu kuliko Muhammad bin Jariri, na hakika Mahanbali walimdhulumu.'"⁷⁵

Ad-Dhahbiy amesema: "Alipopata habari kuwa Abu Bakr bin Daud alizungumza yasiyofaa kuhusu hadithi Ghadir Khum, alibeba kitabu cha fadhila na akaanza na fadhila za Makhalifa wema. Na akaongea kuhusu usahihi wa hadithi ya Ghadir Khum, na akatoa hoja kuthibitisha usahihi wake."⁷⁶ Mahanbali walikuwa kundi la Abu Bakr bin Abi Daud, hivyo walikithiri na kumwanzishia matatizo Ibn Jariri, akapatwa na adha na hivyo akawa hatoki nyumbani kwake. Tunajikinga kwa Mwenyezi Mungu dhidi ya matamanio."⁷⁷

Na kamwe Tabari hakujisalimisha kwa sababu ya shari za wajinga hata baada ya kufa kwake. Ibn Athir ametaja kuwa baadhi ya Mahanbali walikuwa na chuki binafsi dhidi yake, hivyo wakamshambulia, na waliokuja baada yao wakawafuta katika hilo, wakazuia kumzika mchana peupe, na akazikwa nyumbani kwake usiku.⁷⁸

⁷⁵ *Taariikh Baghdaad*: 2/ 164. *Taarikhul-Islami* (311 – 320 A.H.): uk. 281 – 282.

⁷⁶ *Taarikhul-Islami* (311 – 320 A.H.): uk. 281 – 282.

⁷⁷ *Siyrat Aalamin-Nubalaai*: 14/ 277.

⁷⁸ *Al-Kamilu Fit-Tariykh*: 8/ 134.

FITNA YA MAHANBALI HUKO BAGHDAD KATIKA MWAKA WA 323 A.H. NA KUPINGWA NA AR-RADHI

Ibn Athir amesema: "Katika mwaka huo lilikua jambo la Mahanbali na wakapata nguvu na wakawa wakivamia nyumba za viongozi na watu wa kawaida na wakikuta pombe wanaimwaga, na wakimkuta mwanamuziki wanampiga na kuvunja ala ya muziki, wakapinga kuuza na kununua, na kutembea wanaume pamoja na wanawake na watoto, hivyo ilikuwa wanapoona hilo (mwanaume na mwanamke wako pamoja) wanamuhoji ni nani aliye naye, naye ni lazima awaeleze, la sivyo wanampiga na kumpeleka kwa mkuu wa polisi na kumtolea ushahidi wa zinaa. Hivyo wakaitia Baghdad katika misukosuko... shari yao na fitna yao ikaongezeka, na wakapata nguvu kupitia wale wasiojua kitu waliokuwa wakijaa misikitini. Na ilikuwa anapopita mbele yao mfuasi wa madhehebu ya Shafi basi wale wasiojua kitu wanamvamia na kumpiga kwa fimbo zao mpaka anakaribia kufariki.

"Ndipo likatoka tamko la ar-Radhi la yale ambayo Mahanbali wanapaswa kusomewa, katika tamko hilo alipinga vitendo vyao na kuwafokea kwa kuitakidi kwa tashbihi (Mungu kushabihiana na viumbe) na mengineyo, sehemu ya nakala hiyo ni: "Mara nyinyi mnadai kuwa sura za nyuso zenu mbaya zinafanana na Mola wa walimwengu wote..... na mnataja (kuwa Mungu ana) 'kitanga, vidole, miguu, viatu

vya dhahabu, nywele, anapanda mbinguni na kushuka duni-ani.' Ametakasika Mwenyezi Mungu mbali na yale wasemayo madhalimu na wapingaji. Kisha nyinyi mnawatia dosari wale walio bora katika ummah, Amirul-Muuminin anaapa kwa Mwenyezi Mungu....kama hamtaacha madhehebu yenu isi-yokubalika na njia yenu iliyopinda, basi mtapata kipigo na kufukuzwa, kuuawa na kubadilishwa.."⁷⁹

⁷⁹ *Al-Kamilu Fit-Tariykh*: 8/ 307 – 309.

FITNA YA KUSOMA BISMILLAH KWA SAUTI, ILIYOTOKEA KATIKA MWAKA 447 A.H

Ibn Athir amesema: "Katika mwaka huu ilitokea fitna baina ya mafaqih wa Kishafi na wa Kihanbali huko Baghdad, viongozi wa Mahanbali walikuwa ni Abu Ali bin al-Farau na Ibn Tamimiy, na walifuatwa na kundi kubwa la watu wa kawaida, na wakakataa kusoma Bismillahi kwa sauti, na wakazuia kusoma katika adhana: 'Hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu na kwake yeye tutarejea!' Na pia kukunuti ndani ya Swala ya Alfajri...Mahanbali walikwenda kwenye mlango wa msikiti wa Shairi wakamzuia Imam wa msikiti huo asisome Bismillahi kwa sauti, akatoa msahafu na kusema: 'Iondoeni basi kutoka ndani ya msahafu ili nisiaisome!'"⁸⁰

Nasema: "Umemsikilizisha kama ungemwita aliye hai."

⁸⁰ Al-Kamilu Fit-Tariykh: 9/ 614.

FITNA BAINA YA MAASHAIRAH NA MAHANBALI KATIKA MWAKA WA 469 A.H

Ibn Athir amesema: "Katika mwaka huu Abu Nasri mtoto wa ustadhi Abul-Qasim al-Qushayriy alifika Baghdad akiwa alhaji, akaketi katika chuo cha mafunzo ya kijeshi akiwawaidhi watu na akiwa katika cheo cha Sheikh mkuu, na ikatokea baina yake na Mahanbali fitna, kwa sababu alizungumzia madhehebu ya Ashairah na kuyatetea, na hivyo wakakithiri wafuasi wake na pia wale wenye kumchukia, na hatimaye maadui zake pamoja na wale wenye kuwafuata mionganoni mwa Mahanbali wakaenda katika soko la chuo cha mafunzo ya kijeshi na wakaua kundi kubwa."

Pili: Hakika utetezi uliotolewa si katika maneno ya Mwenezezi Mungu wala maneno ya Nabii wake au ya mmoja kati ya Mawasii wake, bali ni utetezi aliouzua Umar bin Abdul-Aziz ili aweze kujinasua na suala la kutoa hukmu kuhusu haki ya Masahaba na Tabiina.

Hakika rai hii alijichagulia Khalifa wa Bani Umajiyah, na inajulikana wazi kuwa rai ya mujtahidu ni hoja juu ya nafsi yake na si juu ya mtu mwingine, hii ni kama tutasema kuwa Khalifa alikuwa mionganoni mwa mujtahidina.

SWALI LA NNE: JE AKILI NI HOJA KWA MASALAFI

Ikiwa rejea ya kielimu ni Watangulizi, kauli zao, Sunna na athari walizopokea, basi akili ina nafasi gani kwao? Na je yenyewe ni hoja au hapana?

Kwa mujibu wa kauli ya kwanza (Ndiyo): Ni wajibu katika baadhi ya mas'ala kurejea kwenye akili ambayo Mwenyezi Mungu amieipusha na upande, mtikisiko na umbile, na si kwenye riwaya zilizojaa mambo haya.

Na kwa mujibu wa kauli ya pili (Hapana): Ni wajibu kum-chukulia Mwenyezi Mungu kwa mujibu wa yale yaliyomo ndani ya Sahih mbili na Sunan, kwa kufuata tafsiri sisisi katika sifa zake ambazo kwa tafsiri hiyo hazikosi umbile, mtikisiko, upande, jaala na mengineyo.

Na kama una shaka na haya tuliyosema kuhusu jambo la pili basi rejea kwenye tauhidi ya Ibn Khuzaymah utaikuta imejaa hayo tuliyosema. Katika hili yeye na mashekhe zake wamedanganyika na yale yaliyopokewa na Ahlul-Kitabi mionganoni mwa Mayahudi na Wakristo waliojifanya Waislamu.

Wanawezaje Masalafi kuifukuza akili kutoka kwenye mlango wa maarifa wakati neno akili limepatikana ndani ya Qur'ani tukufu mara 49 katika minyembuko tofauti. Na Qur'ani inatuhimiza kwa kusema: **“Basi je, hamtumii aki-li?”** au **“Basi je, hawatumii akili?”** na kuna wakati inayahoji maumbile yetu kwa kusema:

أَفَنَجْعَلُ الْمُسْلِمِينَ كَالْمُجْرِمِينَ مَا لَكُمْ كَيْفَ تَحْكُمُونَ

“Kwani tutawafanya Waislamu kama wakosefu? Mna nini? Mnahukumu vipi?” (Sura Al-Qalam 68 : 35 – 36).

Hakika kuifukuza akili kutoka kwenye mlango wa maarifa yaliyopatikana ndani ya Kitabu kunalazimu kuzifunga Aya nyingi ambazo haiwezekani kujua maana yake isipokuwa kwa hoja ya akili na dalili yake, khususan katika majina na sifa.

Hakika Mwenyezi Mungu kupitia Aya zifuatazo anatoa dalili kuthibitisha umoja wake na kubatilisha dhana ya uwe-po wa miungu mingi:

لَوْ كَانَ فِيهِمَا آلِهَةٌ إِلَّا اللَّهُ لَفَسَدَتَا ۝ فَسُبْحَانَ اللَّهِ رَبِّ الْعَزِيزِ
عَنِّيَّا يَصْفُونَ

“Lau wangelikuwemo humo waungu wengine isipokuwa Mwenyezi Mungu basi zingefisadika. Ametasika Mwenyezi Mungu, Mola wa arshi, na hayo wanayoyasifu.”

(Sura Al-Anbiyaa 21 : 22).

إِذَا ذَهَبَ كُلُّ إِلَهٍ بِمَا خَلَقَ وَلَعَلَا بَعْضُهُمْ عَنِّيَّا بَعْضٍ
سُبْحَانَ اللَّهِ عَنِّيَّا يَصْفُونَ

“Ingelikuwa hivyo basi kila Mungu angelichukua alivyoviumba. Na baadhi yao wangeliwashinda wengine. Ametakata Mwenyezi Mungu na wanavyomsifu.” (Sura Al-Mu’minun 23 : 91).

أَمْ خَلَقُوا مِنْ غَيْرِ شَيْءٍ أَمْ هُمُ الْخَالِقُونَ أَمْ خَلَقُوا السَّمَاوَاتِ
وَالْأَرْضَ بِلَّا يُؤْمِنُونَ

“Au wao wameumbwa pasipo kutokana na chochote; au wao ndio waumbaji? Au wameziumba mbingu na ardhi? Bali hawana yakini.” (Sura At-Tur 52 : 35 – 36).

Je mtu wa kawaida aliye mbali na hoja za kiakili anaweza kutafsiri Aya hizi? Hapana labda lengo liwe ni kuzisoma tu na si kuzifahamu na kuzifuata kiroho. Hakika elimu ya sasa imefichua undani wa baadhi ya Aya zinazozungumzia mfumo wa ulimwengu, Aya ambazo hapo kabla zilikuwa hazifahamiki, mfano ni kauli ya Mwenyezi Mungu:

وَالسَّمَاءَ بَنَيْنَاهَا بِأَيْدٍ وَإِنَّا لَمُوسِعُونَ

“Na mbingu tumezifanya kwa nguvu na uwezo na hakika Sisi bila ya shaka ndio wenye kutanua.”

(Sura Adh-Dhariyat 51 : 47).

Na Mwenyezi Mungu anasema:

وَمِنْ كُلِّ شَيْءٍ خَلَقْنَا زَوْجَيْنِ لَعَلَّكُمْ تَذَكَّرُونَ

“Na katika kila kitu tumeumba dume na jike ili mzingatie.”

(Sura Adh-Dhariyat 51 : 49).

Nasema: Kwa manufaa ya Uislamu na Waislamu, na pia ni kwa manufaa ya Masalafi kwamba watupilie mbali minyororo ya chuki binafsi na wajiepushe mbali na fikra za Ibn Taymiyah na za mwanafunzi wa njia yake Muhammad bin Abdul-Wahab, na wautazame ulimwengu kwa elimu, ujuzu, hoja na dalili, ili yaweze kuwapambanukia yale maarifa yalyomo ndani ya Qur'ani tukufu.

SWALI LA TANO

Masalafi wa leo na tabia yao ya kuwakufurisha Waislamu:

Hakika mwenendo wa Watangulizi wema ulikuwa ukipidhihirisha kwa upendo, kuwa radhi na kumkaribisha kila anayepata heshima ya kuwa mwislamu. Walikuwa wakimuhesabu yule aliyetoa shahada mbili, akaamini siku ya mwisho, akasimamisha Swala na kutoa Zaka, kuwa ni mionganini mwa Waislamu. Ana haki kama walijonayo Waislamu wengine, hiyo ni kwa kufuata mwenendo wa Mtukufu Mtume (saww) pale alipoulizwa na Ali (as) kuhusu mwisho wa kupigana jihadi dhidi ya mushrikina, Mtume (saww) alisema: "Wapigeni mpaka washahidilie kuwa hapana mungu isipokuwa Allah, na kwamba hakika Muhammad ni Mtume wa Allah. Wakifanya hivyo watakuwa wamekuzuia kumwaga damu yao na kuchukua mali zao isipokuwa kwa haki ya shahada mbili, na hesabu yao ni kwa Mwenyezi Mungu."⁸¹

Na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alipomsikia Khalid bin Walid akisema: "Ni mara ngapi mwenye kuswali hutamka kwa ulimi wake yale yasiyokuwemo moyoni mwake." Alisema: "Hakika mimi sijaamrishwa kuzipasua nyoyo za watu wala kupasua matumbo yao."⁸²

⁸¹ *Sahih Bukhar*: Juz. 2, Mlango wa Fadhila za Ali (as). *Sahih Muslim* Juz. 6, Mlango wa fadhila za Ali (as).

⁸² *Sahih Muslim*: 3/ 111, Mlango unaowataja Makhawariji na sifa zao.

Ikiwa huu ndio mwenendo wa Watangulizi basi ni kwa nini Masalafi wa leo wamekhalifu mwenendo wao, na wakaukataa kwa kuwakufurisha Waislamu makundi kwa makundi na mtu mmoja mmoja. Na wala hawakubali Uislamu isipokuwa wa yule mwenye kujengeka katika misingi ya U wahabi, ikiwa ni pamoja na kumzuru Mtukufu Mtume (saww) au kuharamisha kutawasali kupitia Manabii na Mawalii, na mengineyo.

HATARI ZA UCHOCHENI WA KIMADHEHEBU

Katika hatua hii hatari ambayo ummah wetu wa Kiislamu Kunakabiliana na matatizo mengi na changamoto hatari, baadhi ya taasisi za kidini na kisiasa za walinganizi wa uwahabi na wenyewe kijiita Masalafi, zimetengeneza chumba cha kuzalisha mfarakanano baina ya Waislamu na kuwagawa kupitia kitendo cha kueneza fikra hatari zinazokhalifu madhehebu ya Sunni na Shia. Na kwa kushikilia tofauti za kimadhehebu na kuzikuza, na kuanzisha makundi mbalimbali yaliyojazwa chuki na hikdi dhidi ya Waislamu khususan Shia.

Wakati tukiwa tunataraji kuona mwendelezo wa juhudzi zilizofanywa na ulamaa wema wa madhehebu mbili (Sunni na Shia) katika kipindi cha mwishoni ili kuimarisha hali ya kuaminiana baina ya makundi mawili, na kuhimiza kushikamana na maeneo yanayowakutanisha pamoja na kutupilia mbali mas'ala wanayotofautiana, na kuleta fursa ya kukaribiana, kufahamiana na kuzungumza kwa faida, wakati tukiwa tunataraji hilo hasa baada ya juhudzi hizo njema kutoa matunda yenye kuonekana katika mambo hayo tuliyoyataja, mara ghafla kimekuja kikosi chenye sumu cha taasisi za kidini na kisiasa tulizoziashiria ili kiongee uwongo kwa jina la Sunna na jamaa, hivyo kupitia vyombo vyaya habari na machapisho kinafanya kazi ya kuchochaea ugomvi na fitna za kimadhehebu na kuyasambaratisha mazingira ya ndani ili iwe ni utangulizi wa mashambulio ya kijeshi ya msalaba na uzayuni dhidi ya nchi za Kiislamu, na ili kiweze kutengeneza mazingira mazuri ya kushambuliwa.

Kisha imeongezeka sumu ya kikosi hiki baada ya kumvamia adui kwa lengo la kuwazuia Waislamu wasitekeleze wajibu wao katika mapambano na kuzilinda nchi zao na matukufu yao, bali wapoteze nguvu zao na juhud zao katika mambo yasiyo na faida na wao, hivyo wakazijaza bongo fikra hatari, na vifua wakavijaza hikdi na chuki, na nafsi wakazijaza roho ya uadui na mabavu dhidi ya wengine, na wakaziacha huru ndimi zao ziweze kutukana na kukashifu, ziwaite wengine kwa majina mabaya na kuwasingizia bidaa na ukafiri.

Mazingira yote hayo yametengeneza hali ya kisaikolojia iliyowapelekea baadhi ya vijana waliodanganyika, kuwauwa watu wasio na hatia, kujilipua au kulipua mabomu kupitia magari yao, tena katikati ya watu wenyewe kuswali au waliopo sokoni au waliopo katika kazi zao za kujitafutia tongue lao. Hayo yote yanatokana na sura iliyochafuliwa mtazamo uliopotoshwa na fikra ya kimakosa.

فَدَّخَسُرُوا أَنْفُسَهُمْ وَضَلَّ عَنْهُمْ مَا كَانُوا يَفْتَرُونَ

“Hakika wamejitia hasarani nafsi zao na yamewapotea wali-yokuwa wakiyazua.” (Sura Al-A'raf 7 : 53).

TUTAKABILIANA VIPI NA HATARI HIZI?

Hakika wakati huu ambao ummah wetu unakabiliana na hatari kubwa ya juhudzi zinazofanywa za kutengeneza mazingira mazuri ya kivita kwa kuchochea moto wa vita vya kimadhehebu, bila shaka wajibu wa kisharia na kimaadili unawalazimisha ulamaa wa Kiislamu wenye nia safi, wanafikra wao na wasomi wao kufanya kazi ya kupambana na mbinu na mipango hii ya makundi yenye chuki binafsi na juhudzi zao katika kuwagawa Waislamu na kuondoa umoja wao wa kijamii, kupambana na mbinu hizo kwa kusambaza fatwa na makala zinazoonesha madhara ya kusingiziana bidaa na ukafiri, kuamsha hisia za uadui na chuki, na kuwahimiza watu kutumia nguvu na ubabe.

Nataraji kuwa hatua zifuatazo zitachangia katika kuondoa hatari hii na kuzuia kimbunga chake:

1. Kuwafichua viongozi wa kikosi hiki chenye sumu, ambaao wanapaza sauti zao kwa jina la Sunni, ilihali wao ni watu baki wasiokuwa Sunni. Imeshatangulia huko nyuma kusema kuwa wafuasi wa kundi hili jipya wanafuata rai za watu wenye misimamo mikali inayotokana na chuki binafsi na hivyo wamepindukia mipaka, na tumetaja mifano ya baadhi tu ya matendo yao ya kinyama na kiuadui dhidi ya wafuasi wa madhehebu za kifiqhi na ki-theolojia za Kisunni (achilia mbali Shia na Mu'utazilah), kama vile Mashafi, Mahanafi na Maashairah, bali ni kwamba katika mas'ala kadhaa ya

kiitikadi wamekhalifu hata rai za Ahmad bin Hanbali ambaye wanadai kuwa wao ni wafuasi wake.

Pamoja na kwamba ulamaa kadhaa wa Kisunni wametamka wazi kuwa madhehebu yao ya Sunni ni tofauti na kundi la Mawahabi na wanaojiita Masalafi, lakini bado hilo halitoshi kwani maslahi ya Uislamu yanahitaji sauti zaidi ya hapo, sauti ya juu kabisa katika kufichua na kupinga matendo maovu yanayotendwa na mikono hiyo inayotumia jina la Sunni ili kuwadanganya watu wasiokuwa makini, ili kuwaangamiza na kuwavurugia dini yao, na ili wawafanye kuni za ugomvi wa ndani, ugomvi ambao una khasara kwa wote wawili mshindi na mshindwa.

2. Kuwaelimisha na kuwajengea uelewa sahihi Waislamu juu ya hatari zinazowakibili na njama zinazopangwa na mihimili ya uovu duniani, ambayo kinara wake ni kundi la kigaidi la kizayuni (Serikali ya Israel), linalofanya hivyo ili liweze kupora matakatifu ya Waislamu, kuvunja heshima yao, kuwanyang'anya utashi wao na kutawala rasilimali zao.

Katika hili, na ili kukuza na kuimarisha uwelewa juu ya uhalisia wa maadui, inapasa kuitangaza bayana historia ya Mayahudi katika zama zilizopita kwa kuptitia Qur'ani Tukufu na vitabu vya Sira ya Mtume, na pia kuitangaza historia yao katika zama za sasa, ili vizazi vitambue tabia yao ya uasi ulijoyengeka katika dhulma, ujisadi na uharibifu. Na pia kuonesha hila zao na mikakati yao mibaya katika kuamiliana na mataifa mengine khususan mataifa ya Kiislamu, wanafanya hivyo ili wafikie malengo yao duni ya kutaka kumiliki uchumi wa dunia, kutawala rasilimali za nchi na kueneza fujo, uharibifu, machafuko na ujisadi ulimwenguni.

Pia inapasa kuonesha historia ya wakoloni katika kuvamia na kuzishambulia kijeshi na kitamaduni nchi za Kiislamu, kuzipora mali zake na kuwagawa, kama njia ya kufikia lengo lao wanilotangaza: "Wagawe uwatawale."

3. Kuarifisha maslahi ya juu ya Uislamu na Waislamu, na kuainisha vipaumbele kupitia hali halisi na kuzuia sura ya uovu na ubaya. Bila shaka juhudzi za kutaka kuonesha uhalisia wetu na kujituma katika kutaka kurekebisha na kunyoosha mambo, hakika juhudzi hizo zitakula muda wote na hazitaacha nafasi ya kufikiria mambo mengine ya daraja la pili, kama vile Ziyara, Tawasuli, Uombezi na mengineyo mionganoni mwa mas'ala ambayo hawa wenye chuki binafsi wasiotumia akili wamekuwa wakiyapa kipaumbele katika kuyapinga, kana kwamba ni mionganoni mwa mas'ala ambayo ni wajibu kupambana nayo na kuyazuia.

Wanafanya hivyo wakati ambapo hali yetu ipo katika hatari kubwa na tatizo hatari, likiwemo suala la Magharibi na Uzayuni kuzitawala nchi zetu, uwepo wa uharibifu mkubwa katika serikali zetu, vyombo vya dola kuwakandamiza wasiokuwa na hatia, uwepo wa jinai ndani ya jamii kama vile mauwaji ya watu wasio na hatia, kupora na kuzuia haki za wengine, kuenea kwa utapeli, rushwa, ujilimbikiziaji mali na bidhaa ili kumiliki soko. Na pia kuongezeka uharibifu katika jamii kama vile uhuru usio na mipaka, unywaji wa pombe, utumiaji wa mihadarati, kuenea kwa filamu na tamthilia zilizo kinyume na maadili, na mengineyo kama hayo.

Je hawa watu wa misimamo mikali wenye kuwagawa Waislamu wamemaliza kurekebisha hali hii mbaya na hatari na kuondoa na kuzuia madhara yake? Au nyuma yao kuna

mikono ya siri ya Shetani inayoendesha harakati hizo ili kuutenga ummah wa Kiislamu mbali usiweze kujali mambo yake muhimu na maslahi yake ya juu?

4. Kutilia mkazo misingi inayozikutanisha na kuziunganisha pamoja madhehebu za Kiislamu, na kusaidiana katika sehemu ambazo twakubaliasa sote, na kuimarisha hali ya kuaminiana na kusameheana baina ya wafuasi wa madhehebu zote, na kuwaonesha wafuasi mazuri ya udugu, kupendana na kuungana, na madhara ya kutengana, kuzozana na kufanyiana hila. Na madhara ya hali hiyo juu ya usalama na amani ya jamii, juu ya miradi ya kimaendeleo, ya ujenzi na ustawi, miradi ambayo itauletea ummah wetu ustawi, raha na maendeleo.

(Ewe Mola! Hakika sisi tuna hamu mno na dola ya heshma toka Kwako, ambayo kwayo Uislamu na watu wake utapata nguvu, na unafiki na watu wake utadhalilika, na utujaalie humo tuwe walinzi kwenye utii Wako, na viongozi kwenye njia Yako, na uturuzuku kwayo heshima ya Dunia na Akhera).

Ja'far Subhani

**Muasasat Imam as-Sadiq (as) – Qum,
28 Shaban muadhamu,
1430 A.H.**

ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA AL-ITRAH FOUNDATION

1. Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzuuy ya kwanza mpaka Thalathini
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo Juzuuy ya Kwanza
4. Uharamisho wa uwongo Juzuuy ya Pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhanga wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (A.S.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashari
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swala
16. Misingi ya Maarifa
17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia

18. Bilal wa Afrika
19. Abudharr
20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi
25. Yajue Madhehebu ya Shia
26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu
27. Al-Wahda
28. Ponyo kutoka katika Qur'an.
29. Uislamu mfumo kamili wa maisha ya kijamii
30. Mashukio ya Akhera
31. Al Amali
32. Dua Indal Ahlul Bayt
33. Udhuu kwa mujibu wa Kitabu na Sunna.
34. Haki za wanawake katika Uislamu
35. Mwenyeesi Mungu na sifa zake
36. Kumswalia Mtume (s)
37. Nafasi za Ahlul Bayt (a.s)
38. Adhana.
- 39 Upendo katika Ukristo na Uislamu

40. Tiba ya Maradhi ya Kimaadili
41. Maana ya laana na kutukana katika Qur'ani Tukufu
42. Kupaka juu ya khofu
43. Kukusanya swala mbili
44. Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahaha
45. Kuwaongoza vijana wa kizazi kipyta
46. Kusujudu juu ya udongo
47. Kusheherekeea Maulidi Ya Mtume (s)
48. Tarawehe
49. Malumbano baina ya Sunni na Shia
50. Kupunguza Swala safarini
51. Kufungua safarini
52. Umaasumu wa Manabii
53. Qur'an inatoa changamoto
54. as-Salaatu Khayrun Mina -'n Nawm
55. Uadilifu wa Masahaba
56. Dua e Kumayl
57. Sauti Ya Uadilifu wa Binadamu
58. Umaasumu wa Mitume - Faida Zake Na Lengo Lake
59. Umaasumu wa Mitume - Majibu Ya Aya Zenye Utata
60. Umaasumu wa Mitume - Umaasumu wa Mitume Muhammad (s)

61. Nahju'l-Balaghah - Juzuuy ya Kwanza
62. Nahju'l-Balaghah - Juzuuy ya Pili
63. Kuzuru Makaburi
64. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Kwanza
65. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Pili
66. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tatu
67. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Nne
68. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tano
69. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Sita
70. Tujifunze Misingi Ya Dini
71. Sala ni Nguzo ya Dini
72. Mikesha Ya Peshawar
73. Malezi Ya Mtoto Katika Uislamu
74. Ubora wa Imam 'Ali Juu ya Maswahaba Na Ushia ndio njia iliyonyooka
75. Hukumu za Kifikihi zinazowahu su Wanawake
76. Liqaa-u-llaah
77. Muhammad (s) Mtume wa Allah
78. Amani na Jihadi Katika Uislamu
79. Uislamu Ulienea Vipi?
80. Uadilifu, Amani na Mtume Muhammad (s)
81. Mitala na Ndoa za Mtume Muhammad (s)

82. Urejeo (al-Raja'a)
83. Mazingira
84. Utokezo (al - Badau)
85. Hukumu ya kujenga juu ya makaburi
86. Swala ya maiti na kumlilia maiti
87. Uislamu na Uwingi wa Dini
88. Mtoto mwema
89. Adabu za Sokoni
90. Johari za hekima kwa vijana
91. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Kwanza
92. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Pili
93. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Tatu
94. Tawasali
95. Imam Mahdi katika Usunni na Ushia
96. Hukumu za Mgonjwa
97. Sadaka yenyе kuendelea
98. Msahafu wa Imam Ali
99. Ngano ya kwamba Qur'ani imebadilishwa
100. Idil Ghadiri
101. Kusoma sura zenye Sijda ya wajibu
102. Hukumu zinazomuhusu mkuu wa kazi na Mfanyakazi
103. Huduma ya Afya katiika Uislamu

104. Sunan an-Nabii
105. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Kwanza)
106. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Pili)
107. Shahiid Mfiadini
108. Kusalia Nabii (s.a.w)
109. Ujumbe -Sehemu ya Kwanza
110. Ujumbe - Sehemu ya Pili
111. Ujumbe - Sehemu ya Tatoo
112. Ujumbe - Sehemu ya Nne
113. Mariamu, Yesu na Ukristo kwa mtazamo wa Kiislamu
114. Hadithi ya Thaqlain
115. Maarifa ya Kiislamu
116. Ukweli uliopotea sehemu ya Kwanza
117. Ukweli uliopotea sehemu ya Pili
118. Ukweli uliopotea sehemu ya Tatoo
119. Ukweli uliopotea sehemu ya Nne
120. Ukweli uliopotea sehemu ya Tano
121. Johari zenyе hekima kwa vijana
122. Safari ya kuifuata Nuru
123. Fatima al-Zahra
124. Myahudi wa Kimataifa
125. Kuanzia ndoa hadi kuwa Wazazi

126. Visa vya kweli sehemu ya Kwanza
127. Visa vya kweli sehemu ya Pili
128. Muhadhara wa Maulamaa
129. Mwanadamu na Mustakabali wake
130. Imam Ali ('a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s)
(Sehemu ya Kwanza)
131. Imam Ali ('a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s)
(Sehemu ya Pili)
132. Khairul Bariyyah
133. Uislamu na mafunzo ya kimalezi
134. Vijana ni Hazina ya Uislamu.
135. Yafaayo kijamii
136. Tabaruku
137. Taqiyya
138. Vikao vya furaha
139. Shia asema haya Sunni asema haya Wewe wasemaje?
140. Visa vya wachamungu
141. Falsafa ya Dini
142. Azadari-Kuhuzunika na Kuomboleza
143. Sunna katika Kitabu Fiqhi al-Sunnah
144. Mtazamo Mpya - Wanawake katika Uislamu
145. Kuonekana kwa Allah

146. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Kwanza)
147. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Pili)
148. Ndugu na Jirani
149. Ushia ndani ya Usunni
150. Maswali na Majibu
151. Mafunzo ya hukmu za ibada
152. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisusunni No 1
- 153 Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisusunni No 2
154. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisusunni No 3
155. Abu Huraira
156. Vipengee kadhaa katika Swala ya Jamaa na Msikiti.
157. Mazingatio kutoka katika Qur'an - Sehemu ya Kwanza
158. Mazingatio kutoka kaitka Qur'an - Sehemu ya Pili
159. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya kwanza
160. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya Pili
161. Qur'ani Tukufu – Pamoja na Tarjuma ya Kiswahili
162. Falsafa ya Mageuzi ya Imam Husein (a.s)
163. Amali za Mwezi Mtukufu wa Ramadhani
164. Elimu ya Tiba za Kiislamu - Matibabu ya Maimamu
165. Uislamu Safi
166. Majlisi za Imam Husein Majumbani

167. Mshumaa.
168. Uislam wa Shia
169. Amali za Makka
170. Amali za Madina
171. Asili ya Madhehebu katika Uislamu
172. Sira ya Imam Ali kuhusu Waasi
173. Ukweli uliofichika katika neno la Allah
174. Uislamu na Mifumo ya Uchumi
175. Umoja wa Kiislamu na Furaha
176. Mas'ala ya Kifiqhi
177. Jifunze kusoma Qur'ani
178. As-Sahifatul Kamilah as-Sajjadiyyah
179. Hayya 'Alaa Khayri'l-Amal Katika Adhana
180. Ukweli kuhusu Funga ya Siku ya Ashura
181. Dua za Miezi Mitatu Mitukufu (Rajabu, Shaabani na Ramadhan)
182. Uadilifu katika Uislamu
183. Mahdi katika Sunna
184. Jihadi ya Imam Hussein ('as)
185. Kazi na kujituma ni njia ya maendeleo
186. Abu Talib – Jabali Imara la Imani
187. Ujenzi na Utakaso wa Nafsi

188. Vijana na Weledi juu ya Mustakabali
189. Usalafi – Historia yake, maana yake na lengo lake
190. Ushia – Hoja na Majibu
191. Mateso ya Dhuria wa Mtume (saww)
192. Maombolezo – Msiba wa Bwana wa Mashahidi (a.s.)
193. Shahidi kwa Ajili ya Ubinadamu
194. Takwa
195. Mwonekano wa Upotoshaji katika Hazina ya Kiislamu

KOPI NNE ZIFUATAZO ZIMETAFSIRIWA KWA LUGHA KINYARWANDA

1. Amateka Na Aba' Khalifa
2. Nyuma yaho naje kuyoboka
3. Amavu n'amavuko by'ubushiya
4. Shiya na Hadithi

MUHTASARI

MUHTASARI

MUHTASARI